# Mwongozo Wa Uperembaji Masuala Ya Kiuchumi Na Kijamii Wa Wasimamizi Wa Ukanda Wa Pwani Wa Magharibi Mwa Bahari Hindi

## SocMon WIO









Aprili, 2006

Delphine Malleret-King, Alison Glass, Innocent Wanyonyi, Lea Bunce na Bob Pomeroy

kwa ushirikiano na Kundi la wataalam wa Masuala ya Kiuchumi na Kijamii wa Ukanda wa Pwani wa Magharibi mwa Bahari Hindi ambao ni:
Delphine Malleret-King (Mwenyekiti)
Leah Bunce
Alison Glass
Modesta Medard
Jason Rubens
Rodney Quatre
Marco Noordeloos
Joseph Tunje
Innocent Wanyonyi
Simon Harding
Anna Blomberg
John Muturi
Joshua Cinner

Mwongozo umetafsiriwa na Hassan Kalombo, John Kabamba, Kessy M. Mvugaro, Shehoza S. Mhina, Zahoro M. Chomoka, na kuhaririwa na Joseph Tunje

WCPA World Commission on Protected Areas
NOAA
ICRI
CORDIO
GCRMN Global Coral Reef Monitoring Network

# Mwongozo Wa Uperembaji Masuala Ya Kiuchumi Na Kijamii Wa Wasimamizi Wa Ukanda Wa Pwani Wa Magharibi Mwa Bahari Hindi

## SocMon WIO









Aprili, 2006

Delphine Malleret-King, Alison Glass, Innocent Wanyonyi, Lea Bunce na Bob Pomeroy

kwa ushirikiano na Kundi la wataalam wa Masuala ya Kiuchumi na Kijamii wa Ukanda wa Pwani wa Magharibi mwa Bahari Hindi ambao ni:
Delphine Malleret-King (Mwenyekiti)
Leah Bunce
Alison Glass
Modesta Medard
Jason Rubens
Rodney Quatre
Marco Noordeloos
Joseph Tunje
Innocent Wanyonyi
Simon Harding
Anna Blomberg
John Muturi
Joshua Cinner
Mwongozo umetafsiriwa na Hassan Kalombo, John Kabamba, Kessy M. Mvugaro, Shehoza S. Mhina, Zahoro M. Chomoka, na kuhaririwa na Joseph Tunje

WCPA World Commission on Protected Areas
NOAA National Oceanic and Atmospheric Administration U.S. Department of Commerce
ICRI
CORDIO
GCRMN Global Coral Reef Monitoring Network

Mwongozo huu wa Uperembaji wa Masuala ya Kiuchumi na Kijamii Ukanda wa Pwani Magharibi mwa Bahari Hindi (SocMon WIO) umetayarishwa na mradi wa CORDIO wa Afrika Mashariki kwa msaada wa fedha kutoka shirika la Kimataifa linaloshughulikia Matumbawe, pamoja na mradi-dada unaofadhiliwa na SIDA- Ushirikiano wa Kimataifa na Maendeleo wa Sweden; Chombo cha Kitaifa cha Utawala wa Anga na Bahari (NOAA); Tuzo namba NA05NOS4631010; Idara ya Biashara ya Marekeani; na Ofisi ya Umoja wa Hifadhi wa Mazingira Duniani katika Kanda ya Afrika Mashariki (IUCN-EARO). Maelezo, uvumbuzi, maana na mapendekezo ni yale ya wahariri, si lazima yaowane na wafadhili.

(c) Haki za kunakili zimehifadhiwa na Mradi wa CORDIO, Afrika Mashariki, 2006
*(CORDIO: Coral Reef Degradation in the Indian Ocean)*

Uchapishaji wa taarifa hii kwa madhumuni ya elimu au malengo mengine yasiyo ya kibiashara yanaruhusiwa hata bila ya ruhusa ya maandishi kutoka kwa mwenye haki za kunakili, mradi tu chimbuko la taarifa yenyewe linatajwa au linadhihirishwa.

Nakala za mwongozo huu (SocMon WIO) na nakala zile za GCRMN (2000) zinaweza kupekuliwa katika tarakilishi kupitia NOAA SocMon site http://ipo.nos.noaa.gov/socioeconomic/, kutoka WIOMSA SocMon Website: http://www.wiomsa.org, na kutoka www.cordio.org

**Machapisho (Hardcopies) yanaweza kuombwa kutoka kwa:**

Innocent Wanyonyi
CORDIO East Africa
8, Kibaki Flats, Kenyatta Beach, Bamburi
P.O. Box 10135, Mombasa, 80101
Kenya
Simu/Fax: +254-41-5486473
socmon@cordioea.org
www.cordio.org

Melita Samoilys
Marine & Coastal Ecosystems Programme
IUCN Eastern Africa Regional Office
P.O. Box 68200, Nairobi, 00200
Kenya
Simu/Fax +254 2 890605-12
melita.samoilys@iucn.org
htt://www.iucn.org/themes/marine/

Maoni juu ya mwongozo huu na marejesho ya jinsi ulivyotumika yatathaminiwa sana. Tafadhali tuma kwa Delphine na Innocent kwa barua pepe socmon@cordioea.org

*Picha za jalada la mbele, kulia kutoka juu:*

Miti ya mikoko ikingojea kusafirishwa, Lamu, Kenya - Innocent Wanyonyi
Uvuvi wa malema, Pemba, Tanzania - Alison Glass
Ukusanyaji wa takwimu za uperembaji wa maswala ya kiuchumi na kijamii, Msambweni, Kenya - Innocent Wanyonyi
Ramani ya nchi kunakofanywa uperembaji wa maswala ya kiuchumi na kijamii kanda ya Magharibi mwa Bahari Hindi - CORDIO GIS
Uwasilishaji wa matokeo ya uperembaji, Diani-Chale, Kenya - Innocent Wanyonyi
Bidhaa za uvuvi-Ukaushaji wa pweza, Baladiron, Rodrigues, Mauritius - Joseph Tunje

*Picha za jalada la nyuma, kulia kutoka juu:*

Warsha ya wataalam wa maswala ya kiuchumi na kijamii kutoka ukanda wa Pwani wa Magharibi mwa Bahari Hindi, Kenya - Alison Glass
Maburudisho ya pwani, Mombasa - Sara Ater
Mafunzo ya ukusanyaji wa takwimu za uperembaji wa kiuchumi na kijamii, Tana Delta, Kenya - Innocent Wanyonyi
Uundaji wa mashua, Lamu, Kenya - Innocent Wanyonyi
Mafunzo ya uperembaji wa kiuchumi na kijamii, Msambweni, Kenya - Innocent Wanyonyi
Bidhaa za uvuvi, Msambweni, Kenya - Innocent Wanyonyi

*Picha ya funzo halisi:* Wanawake wakivua samaki wakitumia nyavu ya mbu "tandilo" Mnazi Bay, Tanzania - Melita Samoilys

*Mchoro:* unawakilisha chombo "mtumbwi" kinachotumiwa sana na wavuvi katika Afrika Mashariki - Patrick Kimani

*Kunukuu:*
Malleret-King D, Glass A, Wanyonyi I, Bunce L, Pomeroy B. 2006. Mwongozo wa uperembaji masuala ya kiuchumi na kijamii wa wasimamizi wa ukanda wa pwani wa magharibi mwa Bahari Hindi (SocMon WIO), CORDIO East Africa publication, (toleo 1), pp 108.

# YALIYOMO


**UTANGULIZI** 1

**NIUTUMIEJE MWONGOZO HUU** 2

**1. MWONGOZO UNAHUSU NINI KIMSINGI?** 3

1.1 Kwa nini kufuatilia masuala ya kiuchumi na kijamii? 3
1.2 Uperembaji wa kiuchumi na kijamii maana yake nini ? 3
1.3 Jinsi gani mwongozo huu unavyofanya kazi? 4
1.4 Mwongozo huu ni kwa ajili ya nani? 4
1.5 Ipi mipaka ya mwongozo huu? 4

*Funzo Halisi: Uchumi Wa Jamii Za Ghuba La Mnazi Na Hifadhi Ya Bahari Kwenye Mlango Wa Mto Ruvuma.* 5

**2. KWA NINI NIFANYE HAYA ?** 8

2.1 Kutambua vitisho, matatizo, utatuzi na uwezekano 8
2.2 Kuonyesha umuhimu, thamani na maana za kimila za rasilimali na matumizi yake 8
2.3 Kupima uzuri na ubaya wa mikakati ya usimamizi 8
2.4 Kupima ufanisi wa bodi ya usimamizi 8
2.5 Kujenga ushirikishwaji wa wadau na mipango muafaka ya elimu ya uelewa 9
2.6 Kudhihirisha na kuweka kumbukumbu madhanio ya hali ya kiuchumi na kijamii katika eneo, mabadiliko ya kijamii na ufahamu wa wadau 9
2.7 Kuanzisha kumbukumbu za kimsingi za kaya na jamii 9

**3. INAJUMUISHA NINI?** 10

3.1 Nani wafanye uperembaji ? 10
3.2 Ni upi mchakato wa kufanyia uperembaji? 10
3.3 Namna gani nikusanye takwimu? 11
3.4 Nani ahojiwe wakati wa uchunguzi? 13
3.5 Muda gani utumike kufuatilia? 14
3.6 Uperembaji utagharimu kiasi gani? 14
3.7 Uperembaji ufanyike mara ngapi? 14
3.8 Uperembaji ufanyike wapi? 15
3.9 Ni ipi hadhira ya matokeo? 15
3.10 Mambo yapi mengine nawajibika kujua? 15

**4. NIKUSANYE TAKWIMU ZIPI?** 16

4.1 Vigezo ni vipi? 16
4.2 Nitumie vigezo vipi? 16

**5. NIFANYE NINI NA TAKWIMU HIZI?** 24

5.1 Uchambuzi wa takwimu 24
5.2 Mawasiliano 24
5.3 Kurekebisha usimamizi 26
5.4 Jedwali la mawasiliano na mabadiliko na mabadiliko ya usimamizi 26

**KIAMBATANISHO A: VIGEZO** 29

**KIAMBATANISHO B: CHANZO PILI/MWONGOZO WA KUHOJI WATOA HABARI MAALUM NA MAKUNDI MAALUM YA WAHOJIWA** 79

**KIAMBATANISHO C: MWONGOZO WA UCHUNGUZI** 87

**KIAMBATANISHO D: KARATASI YA UCHAMBUZI WA WATOA HABARI MAALUM/VYANZO PILI** 91

**KIAMBATANISHO E: UCHAMBUZI WA UCHUNGUZI** 99

# UTANGULIZI

Mwongozo wa uperembaji wa masuala ya kiuchumi na kijamii Magharibi mwa Bahari Hindi (WIO) ,na ule wa usimamizi wa matumbawe (GCRMN) imetengenezwa kutokana na haja ya kuwa na uelewa mpana wa tofauti za fikra za watu wa pwani katika masuala ya rasiliamali za pwani na baharini. Mwongozo wa usimamizi wa Matumbawe (GCRMN) ulitolewa mwaka 2000 katika mkutano wa nane wa Kimataifa kuhusu Matumbawe huko Kisiwa cha Bali. Miongozo ya uperembaji wa kiuchumi na kijamii ya Caribbean (SocMon Caribbean) na Kusini Mashariki mwa Asia (SocMon SEA) iliyotolewa 2003, na huu wa magharibi mwa Bahari Hindi (SocMon WIO) uliotolewa 2006 ilitengenezwa ili kuongezea ule wa (GCRMN) kwa kuufanya uwe rahisi wenye mpangilio mzuri na ambao unaweza sasa kufanyiwa kazi kwa matakwa ya kikanda. Miongozo ya kikanda na ule wa (GCRMN) inalengwa kutumika kwa pamoja - miongozo ya SocMon ni kwa ajili ya kutoa vipaumbele vigezo vya kupima, maswali ya kuhoji na majedwali ya kuchambua takwimu, ambapo Mwongozo wa GCRMN ni kwa kutoa maelezo ya kina namna ya kufanya.

Mwongozo huu wa uperembaji wa masuala ya kiuchumi na kijamii (SocMon WIO) ni matunda ya ushirikiano miongoni mwa wanasayansi, na wasimamizi wa pwani katika kanda hii. Na hasa, kundi la wanasayansi ambao walitayarisha mwongozo huu (SocMon WIO) ndio walioonyesha mwelekeo wa kazi ya mradi huu na mchango wa kitaalam. Malengo ya (SocMon WIO) kuhusu habari za uperembaji wa kiuchumi na kijamii, vigezo, na mpangilio umejengeka kutokana na ule mwongozo wa Caribbean wakati wa matayarisho ya warsha ya Juni 2005 kule Mombasa, Kenya. Delphine Malleret-King na Alison Glass baadaye walichangia mawazo katika mwongozo huu. Walioandika nakala ya kwanza ni:

Delphine Malleret-King (Mwenyekiti, CORDIO, Africa Mashariki), Alison Glass (CORDIO, Afrika Mashariki), Modesta Medard (WWF, EAME, Tanzania), Rodney Quatre (SCMRT-MPA, Seychelles), Jason Rubens (Seascape Project, WWF, Tanzania), Joseph Tunje (CORDIO, Kenya), Innocent Wanyonyi (CORDIO, Kenya), Simon Harding (WCS, Madagascar), Anna Blomberg (WIOMSA), John Muturi (Idara ya Uvuvi, Kenya), na Joshua Cinner (WCS).

Muswada wa (SocMon WIO) ulipitiwa na kusahihishwa na mtandao wa wataalam wenye uzoefu mbalimbali. Hasa shukrani zetu ziwaendee wafuatao kwa michango yao na maoni muafaka: Anju Nihilani na Blue Ventures, Narriman Jiddawi, Josh Cinner, na Jennifer Simbua.

Mwongozo huu utakuwa ukifanywa upya kila baada ya miaka 5 katika utaratibu wa marejesho kwa wasimamizi wa pwani, taasisi na mashirika ya kijamii yanayotumia mwongozo huu.

Mwongozo huu (wa SocMon WIO) ni sehemu ya Programu katika kanda hii inayoendelea ili kuzielewa zaidi jamii na uhusiano wao na rasilimali za pwani na baharini. Mkakati wa SocMon WIO unaandaliwa na kanda, ukiratibiwa na CORDIO Afrika Mashariki. Mafunzo na ufadhili utatolewa kwenye maeneo kulengana na mahitaji ili kuanzisha mtandao wa mwongozo huu wa SocMon. Haja ya kupanua uperembaji wa masuala ya kijamii na kiuchumi (SocMon) kutumia mwongozo huu ilionyeshwa na wanasayansi 29 wakereketwa na wasimamizi kutoka kanda hii walioshiriki katika warsha ya pamoja, kwa lengo la kupima maendeleo yaliyofikiwa katika shughuli za kiuchumi na kijamii, na mbinu zinazotumika kufikia sasa, kujifunza mambo mema yaliyojitokeza, na kuweka vipaumbele vya uperembaji wa kiuchumi na kijamii katika kanda, na vile vile kuchangia mawazo kwa kundi lililoandaa mwongozo huu wa SocMon WIO.

*David Obura & Innocent Wanyonyi*
*CORDIO Afrika Mashariki, Mombasa*
*Novemba, 2005*

# NIUTUMIEJE MWONGOZO HUU?

Soma kila sehemu (1-5) ya mwongozo huu ili upate picha jinsi utakavyofuatilia katika eneo lako.
Sehemu zilizo na rangi ya kijivu ndiyo muhimu za kutengenezea mpango wako wa uperembaji wa kuchagulia vigezo vinavyohusiana na lengo lako kuu, mbinu, uchambuzi na mawasiliano ya matokeo.

**UTANGULIZI**

Soma sehemu 1-3:
- *Malezo yanahusu nini?*
- *Kwa nini nilazimike kufanya haya?*
- *Inajumuisha nini*

...**Kujua kikamilifu maana ya SocMon**, namna ya uperembaji wa kiuchumi na kijamii ulivyo na manufaa kwako, na vitendo vyote vya uperembaji (nani, vipi/jinsi, mbinu, kwa muda gani, kiasi gani, mara ngapi, hadhira)...

**KUCHAGUA VIGEZO VYAKO**

- *Sehemu 4 - Takwimu zipi nikusanye?* Inaelezea vigezo vya mwongozo vile ambavyo vinaweza kutumika kwenye lengo kuu la usimamizi, na jinsi ya kuweka vipaumbele
- *Sehemu 2* - soma tena, na **amua malengo makuu ya uperembaji wa kiuchumi na kijamii katika eneo lako.**
- *Fomu 4.1* - vigezo vilivyopendekezwa vimeorodheshwa hapa, pamoja na maelezo ya msingi na namba za wapi pakurejea. (Mfano KI, S15)
- *Kiambatanisho A* - Kimeorodhesha vigezo vyote na namba zake, na kuzielezea kwa kirefu.
- Jedwali 4.2 - Limeorodhesha malengo makuu yote katika mraba wa kwanza wa jedwali na halafu kuonyesha vigezo vyote unavyohitaji kupimia kila lengo. Kwa kutumia jedwali hili, **weka orodha ya vigezo unavyohitaji kufuatilia ili kufanikisha malengo makuu ya eneo lako.**

*Uperembaji ni mchakato usio na mwisho. Unaweza ukatumia orodha yako ya vigezo kulingana na muktadha wa kiuchumi na kijamii unavyobadilika.*

**KUANZA UPEREMBAJI**

- *Sehemu 5 - Nizifanyieni nini hizi takwimu?* - Kabla hujaanza uperembaji, soma sehemu 5.1 na Viambatanisho D na E. Unaweza kuhitaji kuongeza vigezo vingine katika mpango wako kwa ajili ya uchambuzi, na kwa kutambua jinsi matokeo yatakavyotumika huenda ikasaidia jinsi ya kufanya huo uperembaji.
- *Viambatanisho B na C* - hizi ndizo taratibu za uperembaji zenye sampuli za maswali ya mahojiano/vyanzo pili/ makundi ya walengwa na mbinu za uchunguzi. Tengeneza karatasi zako mwenyewe za maswali ya kuhoji ukitumia maswali unayoona yanafaa kwa vigezo ulivyovichagua
- *Viambatanisho D na E* - karatasi za sampuli za uchambuzi zitakazokusaidia kupambanua utakachohitaji kwa kutumia takwimu ili kupata matokeo yenye maana. Tengeneza karatasi zako za sampuli kwa ajili ya vigezo ulivyovichagua.
- *SocMon WIO database* - Karatasi za takwimu, ambazo zitakusaidia kujaza takwimu katika database ya eneo.

*Sehemu 5.2, 5.3, na 5.4* Uwasilishaji wa matokeo na jinsi ya kuyatumia ili kuboresha usimamizi - hatimaye, sehemu muhimu ya uperembaji ni kutumia kwa **kuingiza matokeo katika usimamizi,** na **kuwasilisha matokeo kwa wadau wote.**

# SEHEMU YA 1: MWONGOZO UNAHUSU NINI KIMSINGI?

## 1.1 KWA NINI KUFUATILIA MASUALA YA KIUCHUMI NA KIJAMII?

Wasimamizi wa rasilimali za pwani wanatambua kuwa haiwezikani kusimamia rasilimali kwa kuangalia viumbe vyenye uhai na uasili wao peke yake. Fikra za jamii juu ya, na matumizi ya rasilimali za pwani vina athari kubwa kwa hali na afya ya vitu vyote vya pwani na baharini. Usimamizi wa rasilimali za pwani vilevile una athiri hali ya kiuchumi na kijamii ya watu. Kwa hivyo, habari za kiuchumi na kijamii ni muhimu mno kwa kufanikisha usimamizi wa rasilimali. Kwa mfano:

- Kama eneo fulani sehemu ya bahari limependekezwa kupigwa marufuku uvuvi wa aina yoyote kwa lengo la aina fulani za samaki kuzaliana, na kutoharibu mazingira. Wavuvi wanalalamikia utaratibu huo kwa kuhofu kupoteza kazi zao. Hivyo, kukusanya habari za aina ya uvuvi, idadi ya wavuvi, na tabia na uelewa wa wavuvi vinaweza kuwasaidia wasimamizi kuamua kwa uhakika kina nani wataathirika, na wataweza kutambua mibadala inayokubalika kuendelea na kazi zao.
- Uma na watunga sera wanahitaji kujua kama ile "Hifadhi ya Bahari imefanikiwa?" Kwa hivyo, taarifa za mabadiliko ya tabia za watu kukubali na kutii sheria zitaonyesha kufaulu au kutofaulu kwa usimamizi na kukubalika au kutokubalika kwa hifadhi ya eneo hilo.
- Mpango mkubwa wa elimu ya uelewa unapendekezwa kwa jamii ya pwani. Kwa kuelewa mbinu za mawasiliano kwa jamii (mfano: mikutano, runinga au magazeti), elimu ya watu wazima, na elimu ya makundi mbalimbali na tofauti za uelewa wao, wasimamizi wanaweza kuandaa mpango mdogo (programu ndogo) na kutumia mbinu rahisi za kuwasiliana na kuhakikisha ujumbe unaofaa kwa walengwa.

*SocMon WIO ni mkusanyiko wa maelekezo yaliyounda mwongozo wa kuanzisha mpango wa uperembaji wa masuala ya kiuchumi katika eneo la usimamizi na kijamii pwani ya magharibi ya bahari Hindi.*

*Ni muhimu kufafanua ya kwamba uperembaji wa kiuchumi na kijamii taratibu zake sio msahafu usiobadilika. Watumiaji wa mwongozo huu na hasa timu* ***ya uperembaji wa masuala ya kiuchumi na kijamii inatazamiwa kujichagulia vigezo, na mbinu zinazofaa kwa mujibu wa mahitaji ya eneo.*** *Kama inavyoelezwa katika sehemu 4.2 (angalia mfano halisi mwisho wa sehemu hii).*

Inaonyesha waziwazi kuwa kusimamia kikamilifu rasilimali za pwani wasimamizi lazima waoanishe hifadhi ya rasilimali na matumizi endelevu pamoja na upatikanaji chakula cha kutosha, kazi na ruhusa ya matumizi ya kiwango muafaka cha rasilimali hiyo. Ni muhimu kutambua uiano wa karibu uliopo baina ya jinsi jamii inavyotumia rasilimali na jinsi hali halisi ya uchumi wa jamii ulivyo. Kwa kuelewa uwiano huu ni msaada mkubwa kwa ajili ya kupima, kutabiri na kudhibiti matumizi ya rasilimali. Habari za kiuchumi na kijamii huwezesha kuelewa hali ya watu, desturi na tabia zao, uchumi, masuala ya kisiasa na hali za mtu mmoja mmoja, familia, makundi, taasisi na jamii. Inaweza kuwasaidia wasimamizi kutambua matatizo yatakayokabiliana na kuzingatia vipaumbele muafaka vya usimamizi. Vile vile usimamizi wa rasilimali za pwani na baharini unaweza kuwa madhubuti kama wasimamizi watashirikiana na kumiliki kwa pamoja taarifa za kiuchumi na kijamii. Watumiaji hutembea ufukoni kama vilevile rasilimali zinavyotembea ufukoni. Aidha uperembaji wa kiuchumi na kijamii ni mtandao wa hao wafuatiliaji na wasimamizi ambao kwa pamoja huwa ni kundi la washauri ambalo mara kwa mara huhusishwa kutoa maelekezo ya kuendeleza mchakato wa uperembaji wa masuala ya kiuchumi na kijamii na vilevile utaalam. Uperembaji hujengeka katika msingi wa ushirikiano baina ya mashirika katika kanda, ambayo yatahakikisha mawasiliano mazuri ya juhudi za kusimamia rasilimali za pwani na baharini.

## 1.2 UPEREMBAJI WA KIUCHUMI NA KIJAMII MAANA YAKE NINI?

SocMon WIO ni mkusanyiko wa maelekezo ya kuanzisha programu ya uperembaji ya masuala ya kiuchumi na kijamii pwani ya Magharibi mwa Bahari Hindi. Uperembaji wa kiuchumi na kijamii unafaa sana kwenye eneo husika. Mwongozo unatoa orodha ya vipaumbele vinavyofaa kwa wasimamizi, na maswali ya kukusanyia takwimu, na vilevile fomu za kuchambulia hizo takwimu. Hivyo, inatazamiwa mwongozo utatumiwa kwa mahitaji ya maeneo mbali mbali. Mwongozo huu wa kiuchumi na kijamii ni uandamane na ule mwongozo wa GCRMN ambao unatumika katika usimamizi wa matumbawe.

Mwongozo huu umekusudia:

- Kutoa mbinu za kukusanya kwa nyakati mbalimbali takwimu za msingi za kijamii na kiuchumi zinazofaa kwa usimamizi wa pwani katika kiwango cha eneo maalum; na,

*Uperembaji wa masuala ya kiuchumi na kijamii unatumika kupima na kutambua mabadiliko kulingana na nyakati ili maamuzi ya usimamizi yafanyike wakati muafaka. Inajumuisha ukusanyaji wa muda mrefu wa habari za jamii, mila na desturi, uchumi na utawala wa watu, makundi, jamii na mashirika kwa vipindi maalum, ambazo zinachambuliwa na kufanyiwa marejesho katika mchakato wakupanga na kutoa maamuzi. Uperembaji siyo jambo la mwisho bali ni njia ya kuboresha au kutathmini usimamizi.*

- Kutoa msingi wa mfumo wa kanda ambao takwimu za kimaeneo zinaweza kujumuishwa na takwimu za kitaifa, kikanda au kimataifa kwa ajili ya kulinganisha.
- Kutoa jukwaa kwa ajili ya kuboresha ushirikiano wa kikanda katika usimamizi wa rasilimali za pwani na baharini kupitia kwa mtandao wa wataalam husika.

Mwongozo huu pia unadhamiria kutoa ufahamu kwa wasimamizi, wengi wao wakiwa na misingi ya elimu ya biolojia, waelewe maana ya "masuala ya kiuchumi na kijamii", jinsi habari za kiuchumi na kijamii zilivyo muhimu kwa usimamizi wao, na vile jinsi takwimu za kiuchumi na kijamii zinavyoweza kuwa za manufaa katika usimamizi wa maeneo yao.

## 1.3 JINSI MWONGOZO HUU UNAVYOFANYA KAZI?

Mpango wa uperembaji wa masuala ya kiuchumi na kijamii kama unavyoelezwa katika kitabu hiki, na katika mwongozo wa (GCRMN) Matumbawe unajumuisha awamu muhimu sita: (1) shughuli za maandalizi (Mwongozo wa GCRMN sura ya 1), inajumuisha utambuzi wa malengo makuu ya uperembaji wa kiuchumi na kijamii, uchaguzi wa vigezo muhimu, kuelezea mchakato wa uperembaji, kutambua na kushauriana na wadau, na kuitambua timu ya uperembaji; (2) ukusanyaji wa takwimu kupitia vyanzo pili (tazama sura ya 2); (3) ukusanyaji wa takwimu kupitia wahojiwa na makundi mbalimbali maalum (tazama sura 3); (4) Ukusanyaji wa takwimu kupitia uchunguzi (tazama sura 3); (5) ukusanyaji wa takwimu kupitia kwa uangalizi (tazama sura 3); (6) ujazaji wa takwimu katika mitambo ya kompyuta, uchambuzi wa takwimu, uwasilishaji wa matokeo na kuyatumia katika usimamizi (tazama sura 4). Huu ni mchakato unaokubali marekebisho, kwa hivyo, matokeo ya awamu mbalimbali bila ya shaka yatahitilafiana na maamuzi ya awali, na hivyo kuhitaji kurudiarudia hatua fulani za nyuma. Hali hii itahitaji kuruhusu kukubali marekebisho.

Vigezo vya mwongozo (tazama sehemu 4 na Kiambatanisho A) vinawasilishwa kulingana na sehemu zake husika na vile vile kulingana na njia zilizotumika kukusanyia: Chimbuko la vyanzo pili, wahojiwa maluum, na/au makundi maalumu ya wahojiwa na uchunguzi. Ziligawanywa namna hii ili kuwiana na aina mbili za miongozo ya mahojiano:- ya kwanza kwa ajili ya vyanzo pili, wahojiwa maluum, na makundi maalum ya wahojiwa ya pili kwa ajili ya uchunguzi. Vigezo pia viko katika makundi kulingana na umuhimu wake wa kukusanywa (tazama Sehemu 4.2.2).

Ni muhimu kufafanua tena kuwa mwongozo huu siyo msahafu usiobadilika. Mtumiaji wa mwongozo huu, timu ya uperembaji wa kiuchumi na kijamii inatazamiwa kuchagua vigezo (vya kuviongezea, na kuvifutilia vile vilivyopewa kipaumbele katika mwongozo huu) na mbinu zifaazo kwa mahitaji ya maeneo kama ilivyojadiliwa katika sehemu ya 4.

## 1.4 MWONGOZO HUU NI KWA AJILI YA NANI?

Hadhira iliyolengwa na mwongozo huu ni wasimamizi wa pwani, wakijumuisha watumishi wanaosimamia maeneo ya pwani, mamlaka ya serikali za mitaa, mashirika yasiyokuwa ya kiserikali na wakazi wa sehemu hizo (kwa mfano, mashirika ya kijamii, vyama vya uvuvi, watumiaji wa rasilimali). Hadhira ya pili ni pamoja na vyuo mbalimbali, na mashirika ya kimataifa na ya kikanda.

## 1.5 IPI MIPAKA YA MWONGOZO HUU?

Mwongozo huu ni mlolongo wa maelekezo ya msingi. Haujakamilisha vigezo vyote vya lazima kwa ajili ya uperembaji wa masuala ya kiuchumi na kijamii (kwa mfano: haujadili kwa kikamilifu utendaji wa uchumi). Umetengenezwa kuwa mlolongo wa wastani wa vigezo vilivyopewa kipaumbele na rahisi kuelewa katika kuvifanyia kazi, na vilevile kuwa vigezo andamizi na mwongozo ule wa matumbawe (GCRMN) ambao unatoa kwa undani vigezo vinavyowezekana kwa ajili ya upimaji wa kiuchumi na kijamii. Kwa hivyo inatazamiwa timu itahusisha mwongozo wa matumbawe (GCRMN) (hususani Kiambatanisho A: Vipengele vya kiuchumi na kijamii) kama inaamuliwa kuingia kwa undani zaidi ya vigezo vilivyopewa kipaumbele katika mwongozo huu.

Mwongozo huu pia hautoi kwa undani namna ya kukusanya takwimu (mfano, namna ya kuendesha mahojiano). Undani unatolewa katika mwongozo ule wa matumbawe (GCRMN) ambao unajumuisha maelezo ya kina namna ya kukusanya takwimu za kiuchumi na kijamii, pamoja na mahojiano, mahojiano na makundi maalum ya wahojiwa, uangalizi na ukusanyaji takwimu kutokana na chanzo pili (tazama sura 3: Ukusanyaji wa takwimu). Kwa hivyo inashauriwa kuwa msomaji atumie miongozo yote miwili (SocMon) kwa ajili ya vigezo vilivyopewa kipaumbele kupimia, maswali ya kuhojia, na majedwali ya kuchambulia takwimu, na mwongozo wa (GCRMN) kwa jinsi ya kufanya.

Mwisho, uperembaji wa kiuchumi na kijamii kwa kutumia mwongozo huu hautatoa majibu kwa maswali yote ya msingi ya usimamizi wa pwani. Hatahivyo, utawapa wasimamizi hawa ufahamu mzuri zaidi wa hali ya jamii kwa wakati ule, namna hali hiyo inavyobadilika, na watazamie mabadiliko gani wakati ujao.

Kwa mfano, takwimu za mapato ya samaki na thamani ya rasilimali zitatoa taarifa isiyo na thamani kwa wasimamizi, hata hivyo hii ni mipango migumu kuianzisha, na haikujumuishwa katika mwongozo huu. Habari kutoka mipango kama hiyo ya uperembaji itakuwa ni ya kuongezea tu ile mipango ya uperembaji inayotolewa na mwongozo huu.

# Funzo Halisi: UCHUMI WA JAMII ZA GHUBA LA MNAZI NA HIFADHI YA BAHARI KWENYE MLANGO WA MTO RUVUMA[1]

**Delphine Malleret-King**[2]




*Map 1: MBREMP Kazi zinazofanywa katika ngazi ya jamii*

Ghuba la Mnazi Hifadhi ya Bahari ya eneo la kuingilia Baharini mto Ruvuma (MREMBP), iliyoanzishwa mwaka 2000, iko katika Mkoa wa Mtwara kwenye pembe ya Kusini mwa pwani ya Tanzania. Ina ukubwa wa kilomita mraba 650 kwa 430 ambazo ni bahari, mto na mikoko. Zilizobakia 220 km mraba ni nchi kavu. Ina utajiri wa bainuai, mialo, upeo mpana wa bahari kama vivutio, matumbawe, idadi ya kutosha ya kasa na viumbe jamii ya mamalia kama nyangumi, wanaohama katika misimu fulani fulani kupita eneo hilo. Sababu za kujumuisha eneo hilo kubwa la nchi kavu katika Hifadhi ya Bahari ni kuwa na eneo la kutenganisha hiyo hifadhi ili kuzuia shughuli za watu zinazoathiri mazingira ya na vilevile kushirikisha watumiaji wa rasilimali za pwani katika mchakato wa usimamizi na mipangilio. Hatahivyo, ilimaanisha kwamba vijiji 11 na vitongoji 3 vikiwa na jumla ya watu 28,000 vilijumuishwa katika hifadhi hiyo. Katika muktadha wa Tanzania, Hifadhi ya Bahari (Marine Park) ni eneo tengefu ambalo kwa kiasi fulani shughuli za binadamu kwa kibali zinakubalika.

Upimaji wa bainuai zilizopo ulifanyika kuanzisha kumbukumbu ya takwimu muhimu na hali halisi ya ustawi wa misitu ya mikoko, matumbawe, ufuko wa bahari na maeneo yenye nyasi. Wakati huo huo, mambo ya kiuchumi na kijamii yalipimwa. Hii ilionekana muhimu kufanyika kutokana na eneo kuwa na watu wengi wanaoishi hapo. Kwa hivyo malengo ya upimaji wa mambo ya kiuchumi na kijamii yalikuwa:



*Women using Tandilo' (by M. Samoilys)*

1) Kutambua na kuelewa hali halisi ya kiuchumi na kijamii ya MBREMP na kuhusisha matumizi ya maliasili zilizopo na hali zake.

2) Kutoa habari za maendeleo kwa mpango wa jumla wa usimamizi wa MBREMP.

3) Kuanzisha msingi wa muktadha wa kiuchumi na kijamii kwa ajili ya uperembaji wa baadaye wa athari za Hifadhi kwa hali ya kijamii na kiuchumi ya wadau.

4) Kuanzisha mpango wa uperembaji ili kuiwezesha Hifadhi (MBREMP) kufuatilia maendeleo yake katika kutimiza malengo yake, na kuwezesha mabadiliko ya usimamizi. Kwa kuongezea, lengo lengine la kupima mambo ya kiuchumi na kijamii ilikuwa ni kuwazoesha watumishi wa Hifadhi kufanya uchunguzi wa kijamii na kiuchumi na waanze kujenga uhusiano na wadau.

[1] *Uchunguzi huu uligharamiwa na UNDP/GEF/MPRU Development of Mnazi bay Ruvuma Estuary Marine Park Project.*
[2] *CORDIO - Mshauri wa kitaalam wa uperembaji wa kiuchumi na kijamii kanda ya Magharibi mwa Bahari Hindi.*

Ili kufikia malengo haya, mapendekezo ya *mwongozo wa kiuchumi na kijamii wa wasimamizi wa matumbawe* (Bunce na wengine 2000) ulifuatiwa na kuiga kutoka mwongozo wa *uperembaji wa masuala ya kiuchumi na kijamii wa wasimamizi wa pwani ya magharibi mwa bahari ya Hindi* (Malleret-King na wengine, 2006). Yaliyoangaliwa yakiwa ni mfumo wa kazi, utaratibu wa matumizi, wadau, migongano, ufahamu wa mamlaka za usimamizi, na mtindo wa maisha kwa vitu. Timu ya upimaji ilikuwa na kiongozi wa mradi (mwanasayansi wa kijamii na kichumi anayefanya kazi na CORDIO, ni mkazi wa eneo la mradi wa Hifadhi ya Ghuba la Mnazi), mwanasayansi kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salam, watumishi 2 kutoka mradi wa Ghuba la Mnazi, kitengo cha Hifadhi za Bahari na maeneo tengefu cha Tanzania. Timu ya watu 6 wawezeshaji, timu ya watu 8 wajumbe wa jamii toka mradi wa Ghuba ya Mnazi walisaidia uchunguzi. Timu ilikuwa kubwa kiasi kulingana na ukubwa wa idadi ya vijiji katika Hifadhi. Huu ukiwa ni uchunguzi wa kwanza, upimaji wa mambo ya kijamii na kiuchumi ulilazimu uwe mgumu na wa kina, kukusanya habari nyingi zaidi, kinyume na mambo yatakavyokuwa wakati wa uperembaji.

Jedwali lifuatalo hapa chini ni muhtasari wa mchakato wa ukusanyaji wa takwimu.

| AWAMU YA UKUSANYAJI TAKWIMU | MUDA | VIGEZO AU MALENGO | NINI KILIFANYIKA |
|---|---|---|---|
| **Upimaji wa takwimu kutoka vyanzo vya pili** | Miezi 2 kabla upimaji kuanza iliendelea hadi mwisho wa zoezi | Vigezo vyote isipokuwa mitazamo na ufahamu | Mahojiano na wawakilishi kutoka kwa wakala wa serikali, vyuo vikuu, mashirika yasiyo ya serikali, sekta binafsi, na taasisi za utafiti, halikadhalika mapito ya maandiko mbalimbali, taarifa, majalada na maeneo ya tovuti. |
| **Safari za Uchunguzi** | Siku 2 | Kujuana na viongozi wa jamii, mamlaka husika, kamati ya uratibu wa mradi wa Hifadhi ya Ghuba la Mnazi | Kujuana na mahojiano yasiyo rasmi yamefanyika na viongozi wa jamii, wawakilishi wa Kamati ya uratibu ya mradi wa Hifadhi ya Ghuba la Mnazi (iliyoundwa na wajumbe wa jamii, na mchanganyiko wa watendaji mbali mbali). |
| **Upimaji** | Mwezi 1 | Eneo, wadau, vigezo vyote vya shughuli za baharini, vyanzo vya mikopo, ufahamu juu ya usimamizi | Kwa kupitia mahojiano na wahojiwa maalum, orodha ya kaya na kazi mbali mbali ilifanywa. Wahojiwa maalum kotoka vijiji vyote walichaguliwa wakiwamo wake kwa waume. Kutokana na kilichoonekana juu ya kazi za wanajamii, makundi kwa mtazamo wa aina ya matumizi yalichaguliwa kuanzisha kumbukumbu za mbinu, mfumo wa matumizi, migongano kulingana na matumizi, hali za rasilimali na mabadiliko yake, tabia za wadau n.k. Washiriki walichaguliwa bila ya mpango maalum kulingana na makundi ya shughuli zao (kwa mfano: wavuvi kulingana na zana zao, wachuuzi wa samaki kulingana na bidhaa yao). Utengenezaji wa ramani kama ulivyoelezwa katika Mwongozo wa kiuchumi na kijamii wa wasimamizi wa Matumbawe (Bunce na wengine 2000) ulifanyika kutambua sehemu muhimu za uvuvi na biashara ya samaki. |
| **Uchunguzi wa mtindo wa maisha kwa vitu** | Wiki 2 | Mitindo ya maisha kwa vitu demografia, utaratibu wa matumizi, Mbinu, kazi za wanavijiji, shughuli za baharini, kipato | Karatasi ya mahojiano iliandaliwa kwa misingi ya kilichojitokeza kutoka kwa wahojiwa maluum (habari muhimu za mtindo wa maisha kwa vitu katika eneo lile), na vilevile kulingana na kilichojitokeza kutokana na upimaji wa wadau, mbinu na utaratibu wa matumizi n.k.<br>Baadaye vilitumiwa kwa sampuli za kaya katika vijiji 5 vilivyoteuliwa kulingana na jiografia ya eneo katika Mradi wa Hifadhi ya Ghuba la Mnazi. Kaya 2810 zilitumika kama sampuli (karibu asilimia 56% ya kaya za mradi wa MBREMP).<br>Kwa kuongezea mahojiano ya mpangilio kupitia mawasiliano yasiyo rasmi pamoja na uangalizi vilitumika kuboresha matokeo yaliyopatikana katika karatasi za mahojiano, na kulinganisha na matokeo hayo na mawazo ya waliohojiwa wakati wa zoezi. Kumbukumbu ya takwimu mahususi iliandaliwa kwa kutumia karatasi ya namba (coding sheet). |

Uchambuzi wa takwimu ulijumuisha kuchanganya matokeo pamoja na kutengeneza majedwali na mahesabu na kazi ya kupiga mahesabu ya ufafanuzi. Uchambuzi pia uliwekea nafasi kwa ajili ya kuelezea sehemu zenye matumizi makubwa. Taarifa ya maandishi iliandaliwa na kuwasilishwa kwa mamlaka ya (Mradi wa Hifadhi ya Ghuba la Mnazi) na IUCN. Taarifa inatoa habari ya utegemezi wa rasilimali za baharini kwa upande wa jamii kwa jinsi wanavyotumia rasilimali za pwani na baharini, na jinsi mradi wa MBREMP unavyoelekea kuathiri maishilio yao, na ya vikundi ambavyo vitadhuriwa na hatua za upigwaji marufuku uvuvi bila ya vibali.

Taarifa inapendekeza mpango wa uperembaji ambao umebuniwa kwa msingi wa matokeo ya upimaji wa mambo ya kiuchumi na kijamii. Orodha ya mapendekezo na utafiti wa ziada pia umejumuishwa katika taarifa.

Upimaji wa mambo ya kiuchumi na kijamii ulionyesha kuwa:-

a) Idadi ya watu wanaojihusisha katika uvunaji wa rasilimali za baharini (inakadiriwa kuwa 1400).

b) Utegemezi wa jamii kwa jumla katika rasilimali za baharini kwa maishilio; katika ngazi ya vijiji, zaidi ya asilimia (60%) ya kaya zilionekana kujihusisha na rasilimali za pwani na baharini, uvuvi ukiwa ndiyo chanzo kikubwa cha mapato ya wavuvi waliochunguzwa; katika ngazi ya Hifadhi, asilimia 35 ya kaya zinajihusisha na shughuli za pwani na baharini.

c) Umasikini/ukosefu wa mitaji ya fedha ulilazimisha watu kutumia rasilimali ambazo ziko karibu na ufuko wa bahari na wakitumia nyavu za macho madogo.

d) Ongezeko la mahitaji ya bidhaa za baharini na kiwango cha biashara cha bidhaa maalum za baharini (kwa mfano,majongoo-bahari, pweza na kamba mti ambao kwa sasa wanaelekea kupungua kwa wingi na ukubwa).

e) Mbinu za uvuvi haribifu (hususani nyavu za macho madogo).

2. Zana mojawapo ya uharibifu mkubwa ni '*tandilo*' ambayo ni mbinu iliyoenea sana na inatumiwa na kinamama. '*Tandilo*' ni nyavu ya macho madogo sana (mara nyingi ni chandarua au nguo) ambayo wanawake 3 hadi 6 hukokota kuelekea ufukoni.

3. Biashara ya samaki wakavu ni moja wapo yenye faida kubwa katika shughuli za rasilimali za baharini, na imeendelea kutokana na mahitaji mengi kutoka bara.

4. Makombe ni chanzo muhimu cha chakula na kipato (biashara ya mapepe na mapambo), ingawaje kulikuwa na ufahamu mdogo wa kibiolojia. Wadau katika biashara hii ni watu tofauti tofauti kuanzia wavuvi wenyewe wa Mtwara hadi wasafirishaji nje hasa wale wa Mashariki ya Kati. Kuna haja ya kufanya uchunguzi zaidi ili kuonyesha kiwango kinachofaa cha uvunaji wa makombe na changizo la nyama ya makombe kwa upande wa protini katika kaya. Hii itatoa msingi kwa Hifadhi kutoa maamuzi ya jinsi ya kudhibiti uokotaji/uvuvi wa makombe.

5. Hifadhi ya Ghuba la Mnazi ipo karibu na mpaka wa nchi ya Msumbiji. Imegundulika kuwa kadiri rasilimali zinavyodhibitiwa katika MBREMP, ndivyo wavuvi wanavyozidi kuvua upande wa nchi ya Msumbiji ambako udhibiti ni mdogo.

6. Ustawi wa rasilimali za Hifadhi hii ya Mnazi unategemea ushawishi mkubwa wa mtandao wa kilimwengu, kimataifa, kitaifa, kikanda na kienyeji, yanayotegemea vitu kama mahitaji ya chakula, ladha, uzuri wa mazingara , mila/desturi mambo yahusuyo dini. Hifadhi haina uwezo wa mambo yote haya, ila kwa kufanya kazi na mchanganyiko mkubwa wa wadau ambao wanaathiri rasilimali na ambao pia wataathirika na utekelezaji wa sheria na kanuni za Hifadhi, kwa hiyo Hifadhi itachangia kubadili matakwa ya watumiaji (kwa mfano, yanayohusu aina ya rasilimali zinazotishiwa kupungua pamoja na wasafirishaji bidhaa nje).

7. Imegundulika kuwa mawasiliano hafifu na utoaji habari zisizokweli mara nyingi ndiyo kiini cha jamii kuwa na mtazamo hasi kwa hifadhi ya MBREMP. Ingefaa kutilia nguvu shughuli za MBREMP za ufahamu na uhamasishaji wa jamii.

Takwimu hizi za msingi zitatumika kuanzishia mpango wa uperembaji wa kiuchumi na kijamii (kazi mbalimbali, matumizi mbalimbali, mbinu, uelewa wa wadau kuhusu Hifadhi, bei za bidhaa muhimu, majongoo bahari na idadi ya wachuuzi madondo na idadi inayosafirishwa nje) ambayo ni sehemu muhimu ya Mpango wa Usimamizi wa MBREMP. Wafanyakazi wa Hifadhi ya Mnazi wanapima kiwango cha manufaa ya mikakati ya Mpango wa Usimamizi kwa mujibu wa habari hizi za kiuchumi na kijamii. Upimaji huu wa mambo ya kiuchumi na kijamii ulionyesha vipengele mbalimabli ambavyo Hifadhi ya Mnazi lazima kuvizingatia wakati itakapobuni mpango wa usimamizi. Vile vile ulionyesha mahali ambapo habari zaidi zinahitajika ili kufanya maamuzi.

# SEHEMU YA 2: KWA NINI NIFANYE HAYA?

Habaari za kiuchumi na kijamii zinaweza kutumiwa na wasimamizi wa pwani kwa malengo mengi. Ni muhimu wasimamizi na timu ya uperembaji wa masuala ya kiuchumi na kijamii kuamua yale malengo muhimu yanayofaa kwa uperembaji ili waweze kuteua vigezo husika kwa ajili ya ukusanyaji wa takwimu. Sehemu ya 4 ambapo vigezo vinaelezwa na utaratibu wa kuviteua unaelezwa, inajumuisha jedwali linaloonyesha ni vigezo vipi vikusanywe na kwa lengo lipi. Ingawa mwongozo huu umeandikwa kutoka kwa mtazamo wa "msimamizi", ni vizuri kutambua kuwa uperembaji wa masuala ya kiuchumi na kijamii vile vile unafaa kwa wadau wengine. Hii itasisitizwa kwa kila kigezo katika Kiambatanisho A.

*Malengo haya yanahusu kanda nzima. Msimamizi wa pwani na timu ya uperembaji wachague yale malengo tu muafaka kwa mahitaji ya eneo lao.*



## 2.1 KUTAMBUA VITISHO, MATATIZO, UTATUZI, NA UWEZEKANO.

Zinapokusanywa mara kwa mara, kuliko upimaji wa mara moja tu, habari za kiuchumi na kijamii zinaweza kutumika kutambua mienendo na mabadiliko ya kijamii na watu wa kaya, na sifa za kiuchumi wao, shughuli za pwani na ufahamu wa watu kuhusu jamii na masuala ya pwani. Haya yanaweza kutumika kutambua matishio, matatizo, masuluhisho, na nafasi ya usimamizi wa rasilimali za pwani. (kwa mfano, kuongezeka kwa uhamiaji wa watu katika eneo kunaweza kuonyesha dalili za hatari za kuongezeka kwa kiwango cha uvuvi na maendeleo ya matumizi ya ardhi, kama vile ukataji wa mikoko.

*"Mdau" ina maana ya watu wanaotumia moja kwa moja rasilimali za pwani pamoja na watu ambao hatua zao zinaweza kuathiri rasilimali za pwani.*



## 2.2 KUONYESHA UMUHIMU, THAMANI NA MAANA ZA KIMILA ZA RASILIMALI NA MATUMIZI YAKE.

Habari za kiuchumi na kijamii zinaweza kutumika kudhihirisha umuhimu na thamani ya rasilimali na huduma za pwani kama vile matumbawe yanavyotumika kiutamaduni kwa jamii, makundi ya wadau na watoaji wa maamuzi, ambao husaidia kuweka msukumo wa mipango ya usimamizi wa rasilimali za pwani. Kwa mfano, ufahamu wa thamani ya matumbawe unaweza kutumiwa kutathmini faida na hasara za mbadala wa maendeleo, mambo ya usimamizi na uhifadhi (kwa mfano,uamuzi wa kuruhusu kuzamia katika eneo fulani kunaweza kujikita kwa misingi ya kazi na kipato kinachotarajiwa kwa jamii kutoka kwa shughuli za kitalii).

## 2.3 KUPIMA MAZURI NA MABAYA YATOKANAYO NA MIKAKATI YA USIMAMIZI WA RASILIMALI

Habari za kiuchumi na kijamii zinaweza kutumiwa kutambua athari za maamuzi ya usimamizi kwa wadau, ambazo zinaweza kuboresha sera za kupunguza mabaya na kuzidisha mazuri kwa wadau. Kwa mfano: uamuzi wa kuzuia aina fulani ya mtego wa uvuvi unaweza kuathiri kazi za jamii na thamani ya samaki sokoni. Kuweka kumbukumbu ya maandishi kuhusu mabadiliko ya kazi za jamii na thamani ya sokoni kabla na baada ya sera haijatekelezwa, wasimamizi wanaweza kuyakinisha athari za sera hiyo. Vile vile wasimamizi wanaweza kutumia habari za uchumi wa jamii kutabiri athari za sera mbadala kwa jamii. Kwa mfano, kwa kujua idadi ya watu wanaovua katika maeneo mbalimbali, wasimamizi wanaweza kutabiri idadi ya wavuvi watakaoathiriwa kwa kupendekeza kuwepo kwa eneo lisiloruhusiwa kuvuliwa.

## 2.4 KUPIMA UFANISI WA BODI YA USIMAMIZI

Habari za uperembaji kiuchumi na kijamii zinaweza kutumika kupima ufanisi wa mipango ya usimamizi wa rasilimali za pwani katika kufikia malengo na madhumuni yao. Kwa mfano, kama lengo kuu la mpango wa usimamizi wa rasilimali za pwani ni kuboresha ushirikishwaji wa wadau waliopo katika mchakato wa usimamizi, ili bodi ya usimamizi iweze kuambiwa ilifaulu, lazima kuwe na ufahamu mzuri wa watu katika kushiriki kwenye maamuzi ya usimamizi wa rasilimali za pwani.

Uperembaji wa masuala ya kiuchumi na kijamii unaweza kuboresha usimamizi wa rasilimali za pwani kupitia kwa mafunzo, kuiga na kubaini masuala maalum yanayoshawishi mafanikio ya mpango wa usimamizi wa rasilimali za pwani katika kufikia malengo na madhumuni yake. Kwa mfano, mabadiliko ya ufahamu wa watu katika kutii na kutilia nguvu sheria na kanuni, kunaweza kuashiria kufanikiwa au kutofanikiwa kwa shughuli za usimamizi na uwezekano wa kuhitajika kwa mabadiliko katika shughuli za kutilia nguvu sheria.

## 2.5 KUJENGA USHIRIKISHWAJI WA WADAU NA MIPANGO MUAFAKA YA ELIMU YA UELEWA.

Habari za kiuchumi na kijamii zinaweza kutumika kuongoza ushirikishwaji wa kundi la wadau katika kujihusisha katika mchakato wa usimamizi. Kushiriki katika uperembaji, hasa kwa kutoa habari kutaweka msingi wa ushirika bora wa wadau katika mchakato wa usimamizi. Vile vile habari za kiuchumi na kijamii (kwa mfano, uelewa wa wadau kuhusu usimamizi wa rasilimali) kutawafanya wadau wapate nafasi ya moja kwa moja ya kutoa marejesho juu ya usimamizi.

Vile vile zinaweza kutumika katika kupanga na kuelekeza mipango ya elimu na uelewa ya usimamizi wa rasilimali za pwani. Kwa mfano, kubaini mashirika ya kijamii na ya wadau katika eneo husika kunaweza kusaidia wasimamizi wa pwani kuhakikisha kwamba wadau muhimu wanapata nafasi ya kushiriki katika mchakato wa usimamzi wa raslimali za pwani.

Wakati huo huo, habari za kiuchumi na kijamii zitawapa nafasi wasimazi kujifunza kutoka kwa utaalamu wa kienyeji na mifumo ya usimamizi ya jadi, ambayo inaweza kujumuishwa katika usimamzi rasmi wa rasilimali za pwani.



## 2.6 KUDHIHIRISHA NA KUWEKA KUMBUKUMBU MADHANIO YA HALI YA KIUCHUMI NA KIJAMII KATIKA ENEO, MABADILIKO YA KIJAMII NA UFAHAMU WA WADAU.

Ukusanyaji wa takwimu za kiuchumi na kijamii na uchambuzi wake ni muhimu kudhihirisha kisayansi na kuweka kumbukumbu hali za kijamii. Katika mpango wowote wa usimamizi wa rasilimali za maliasili, mara nyingi hutokea ufahamu mpana wa hali za mahali hapo. Kwa mfano, kwa jumla inaweza kukubalika kuwa ustawi wa mikoko unadidimia. Wasimamizi huhitaji takwimu za kisayansi kuthibitisha na kuwekea kumbukumbu hali hiyo. Bila ushahidi wa kisayansi maelezo yatakuwa ni ya kubahatisha tu. Kwa hivyo, kudhihirisha na kuwekea kumbukumbu ufahamu wa watu ni muhimu vile vile kwa hali za kiuchumi na kijamii kwani huwa ni rahisi kuzipendelea kulengana na matitizo na thamani ya watu. Kwa kuwa na lengo, uchunguzi wakufanywa mara kwa mara, msimamizi anaweza kuona hali halisi ya kiuchumi na kijamii, pamoja na utaratibu wa matumizi ya rasilimali, mabadiliko ya hali ya kijamii na ufahamu wa wadau.

## 2.7 KUANZISHA KUMBUKUMBU ZA KIMSINGI ZA KAYA NA JAMII .

Habari za kiuchumi na kijamii zilizokusanywa mwanzo wa mpango wa uperembaji wa usimamizi wa rasilimali za pwani, ambao mara nyingi hujulikana kama tathimini ya kiuchumi na kijamii, huonyesha taswira ya jamii na hali halisi ya kaya katika muda fulani, na inaweza kumsaidia msimamizi kufahamu jamii na kaya zote, na kuanzisha hali za msingi kwa mlinganisho wa siku za baadaye. Habari hii ya msingi inaweza kuwa ya umuhimu katika kuleta marekebisho ya usimamizi. Kadiri malengo na shughuli zinavyobadilika, msimamizi anaweza kulinganisha hali za sasa na habari za msingi kubaini sababu za mabadiliko pamoja na athari  za mabadiliko hayo. Kwa mfano, kama “kuunga mkono mila na desturi za kienyeji” halikuwa moja ya malengo asilia ya mpango wa usimamzi wa pwani, basi hali ya mila na desturi hazingeweza kufuatiliwa kwa muda.

Hata hivyo, kwa kuwa na habari za kimsingi za mila na desturi, wasimamizi wanaweza kufanya urejeshi kwa habari hizi za kwanza kutathimini jinsi hali zilivyobadilika kulingana na muda.

# SEHEMU 3: INAJUMUISHA NINI?

## 3.1 NANI WAFANYE UPEREMBAJI?

Uperembaji wa masula ya kiuchumi na kijamii unaweza kufanywa na mtu binafsi, lakini kwa kawaida hufanywa na timu ikiongozwa na mtumishi kutoka usimamizi wa pwani (kwa mfano, mratibu wa uperembaji kutoka hifadhi ya bahari au mamlaka ya uvuvi, ofisa wa elimu kutoka shirika la mazingira) mwenye uelewa wa nyanja mojawapo ya sayansi ya jamii (somo la migawanyiko ya watu, somo la sayansi binadamu, uchumi, sayansi ya kisiasa, somo la mawazo na hisia za watu au Jiografia). Kumshirikisha mtumishi katika uperembaji wa kiuchumi na kijamii ni muhimu katika kuanzisha uthabiti wa muda mrefu na kuhakikisha kwamba mtumishi wa usimamizi wa pwani anaweza kupata takwimu na kuzitumia katika kuboresha usimamizi wa pwani.

Kiongozi wa timu anawajibika katika kupanga uperembaji; ukusanyaji, uchambuzi, na uwasilishaji wa takwimu, na kuhakikisha mpango unaendelea kwa muda mrefu. Wengine katika ile timu wasaidie katika ukusanyaji takwimu hasa mahojiano, uchambuzi, uandikishaji wa taarifa na uwasilishaji.

Kwa kawaida, wanatimu wawe na uelewa katika mojawapo ya masomo ya sayansi ya jamii na ufamu wa eneo la uchunguzi. Vilevile ni vuzuri kama wanatimu watafundishwa na kuwa na uzoefu wa kufanya mahojiano katika eneo la uchunguzi. Ama wana elimu ya sayansi ya jamii au hawana, ni vizuri wanatimu wawe na ujuzi wa kuingiliana na aina mbali mbali za watu, wawe na ari ya kazi, na wenye uwezo wa kuchambua mambo, na wenye mapenzi na mradi. Kwa vile watumishi wengi wa mipango ya usimamizi wa pwani wana shahada za sayansi katika masomo ya maliasili,mwongozo huu wa uperembaji wa masuala ya kiuchumi na kijamii umeandikwa kwa kufikiria kwamba wanatimu wana uelewa mdogo, lakini angalau kiwango cha elimu cha shule ya upili. Kwa nyongeza, ni vizuri kuwajumuisha wanajamii ili kusaidia katika mchakato wa ukusanyaji wa takwimu. Hali hii itaongeza uhusikaji wa jamii na kuupenda mradi, na hivyo kusaidia kujenga uhusiano kati ya watumiaji wa rasilimali na wasimamizi.

Kama kiongozi/au wanatimu wana utaalam mdogo wa kiuchumi na kijamii, ni vizuri wapitie *mwongozo wa GCRMN*, ambao unatoa maelezo ya kina jinsi ya kufanya tathimini za kiuchumi na kijamii. *Mwongozo wa GCRMN Sura 1: Shunguli za Maandalizi, Kutambua timu ya kutathimini*, na pia kutoa vidokezo vya kuijenga timu hiyo.

Kama hakuna mtaalamu wa sayansi ya jamii katika timu, uperembaji wa kiuchumi na kijamii bado unaweza kufanyika. Kuna vifaa, ikiwemo *mwongozo wa GCRMN*, ambao upo kwa ajili ya kujenga umahiri (pia tazama mwongozo wa GCRMN, maeneo ya vyanzo vya nyongeza). Kwa kuongezea, watafiti wa taasisi za elimu taasisi ya kanda ya kuratibu uperembaji wa kiuchumi na kijamii magharibi mwa bahari ya Hindi inaweza kusaidia kutoa maelekezo ya kitaalam/au kuelekeza wapi watapatikana wataalam husika. Kama ilivyoelezwa hapo juu, kuwa na motisha na kuupenda mradi ni vitu vya msingi mno kwa wanatimu.

## 3.2 NI UPI MCHAKATO WA KUFANYIA UPEREMBAJI?

Kama ilivyoelezwa katika *Sehemu 1.3,* kuna hatua sita za kufanyia uperembaji wa kiuchumi na kijamii, zikiwa ni pamoja na:-

1. Shughuli za maandalizi, pamoja na kutambua malengo ya uperembaji wa kiuchumi na kijamii, kuchagua vigezo vinavyofaa, kuelezea mchakato wa uperembaji wa kiuchumi na kijamii, kutambua na kushauriana na wadau, na kutambua timu ya uperembaji.
2. Ukusanyaji wa takwimu kupitia vyanzo vya pili
3. Ukusanyaji wa takwimu kupitia watoaji habari maalum na makundi maalum ya wahojiwa
4. Ukusanyaji wa takwimu kupitia uchunguzi
5. Ukusanyaji wa takwimu kupitia uangalizi
6. Ujazaji wa takwimu, uchambuzi wa takwimu, mawasiliano na kurekebisha usimamizi.




Huu ni mchakato wa kujirudia-rudia unaohitaji kurudiwa nyakati kwa nyakati ili kuweka sawa na kuongeza takwimu na habari mpya. Pia ni mchakato unaokubali kubadilika kwa vile hatua zinazohusika katika uperembaji wa masuala ya kiuchumi na kijamii mara nyingi hazifuati mchakato huu moja kwa moja, na mara nyingi huhitaji kurudiwa. Habari mpya zinaweza kusababisha mahitaji mapya, hivyobasi timu lazima iangalie maendeleo na kubadili mipango kulengana na hali mpya, pamoja na kurekebisha orodha ya vigezo vya ukusanyaji na uchambuzi wa takwimu.



## 3.3 NAMNA GANI NIKUSANYE TAKWIMU?

Orodha ya vigezo vilivyomo katika mwongozo huu wa SocMon vimegawanyika katika mbinu nne za ukusanyaji.

1. Vyanzo vya pili (Sec).
2. Wahojiwa maalum (KI)/Makundi maalum ya kuhojiwa (FGI).
3. Uchunguzi (S)
4. Uangalizi

Kwa kawaida, takwimu lazima zikusanywe kupitia vyanzo vya pili kwanza, wafuatie wahojiwa maalum katika mahojiano, na makundi maalum. Kama takwimu zilizokusanywa toka wahojiwa maalum na vyanzo vya pili zinatosheleza kukidhi mahitaji ya timu kwa upande wa malengo yao, hakutakuwa na haja ya kufanya uchunguzi mbalimbali. Hatahivyo, mara nyingi uchunguzi hufanyika kupata takwimu maalum zenye uhakika kuwahusu watu binafsi na kaya katika eneo la uchunguzi (tazama Jedwali 4.1 kwa orodha ya vigezo vya watoa habari maalum/makundi maalum ya wahojiwa/vyanzo vya pili vya ukusanyaji wa takwimu na uchunguzi, mtawalia). Uangalizi unaendelea katika jamii. Mbinu hizi zinaelezwa kwa undani katika *Mwongozo wa GCRMN Sura ya 3: Ukusanyaji wa takwimu* ugani, ambako mapungufu na mazuri ya kila mbinu yanasisitizwa. Utafiti wa ndani na sahihi ni muhimu kufanyika ili kufanya kufanikisha mpango wa uperembaji, pamoja na kupunguza upendeleo, kujenga uaminifu kwa jamii n.k., yote haya yanazungumzwa katika Mwongozo wa GCRMN.

*Timu lazima kuzingatia masharti yafuatayo wakati wote wa ukusanyaji wa takwimu.*

- *Heshimu wadau na jamii, kama vile ratiba ya kazi, mila na desturi, na dini*
- *Tambua upendeleo wa wahojiwa*
- *Zingatia masuala ya jinsia*
- *Yafikie maeneo yasiyofikiwa kwa urahisi*
- *Zingatia utofauti wa lugha (mfano pata wakalimani)*
- *Andika maelezo kwa undani*
- *Zichunguze habari kwa mapana yake.*

*Haya na maelekezo mengine ya ukusanyaji wa takwimu za ugani yanaelezwa kwa kirefu zaidi katika Mwongozo wa GCRMN, Sura 3: Ukusanyaji wa takwimu za ugani.*



### 3.3.1 VYANZO VYA PILI

Timu ya uperembaji lazima ianze kwa kufanya tathimini kamili ya vyanzo vyote vya pili vya takwimu kupitia vigezo vilivyochaguliwa. Vyanzo vya pili (Sec) ni vile ambavyo tayari takwimu zilikusanywa, zilichambuliwa, na zimechapishwa katika fomu mbalimbali, zikijumuisha :

- Nyaraka rasmi na zisizo rasmi
- Taarifa za takwimu

- Kumbukumbu za miradi ya awali au inayoendelea ikijumuisha taarifa za uperembaji na tathimini
- Ramani
- Taarifa za tathimini na uchunguzi wa awali
- Taarifa za tafiti mbalimbali
- Picha za maeneo kutoka angani, na vivuli vya satalaiti
- Nyaraka za kihistoria na maelezo
- Tovuti za intaneti.

Tathimini ya takwimu kutoka vyanzo vya pili vinahusisha kuweka pamoja, kutathmini na kupitia takwimu zinazohusika na vigezo vilivyochaguliwa.

### 3.3.2 WAHOJIWA MAALUM NA MAKUNDI MAALUM YA KUHOJIWA

Wahojiwa maalum (KI) ni watu binafsi ambao wana uzoefu au uelewa, kwa sababu ya nafasi zao, wanaweza kutoa mawazo na habari juu ya watu au kundi fulani katika jamii. Kwa mfano, kiongozi wa jamii anaweza kutoa maelezo ya uelewa fulani ndani ya jamii, kiongozi mkuu wa chama cha wavuvi anaweza kutoa hoja katika shughuli za wavuvi, na mchungaji wa kanisa la wenyeji anaweza kutoa hoja kwa waumini wa kikristo katika jamii. Kwahivyo, wahojiwa maalum wanaweza kutoa elimu ya kawaida, elimu ya ubia na elimu maalum. Kwa sababu mara kwa mara haiwezekani kuzungumza na kila mtu katika eneo la uchunguzi, watu hawa wenye uzoefu na elimu mara nyingi hutafutwa. Mara nyingi hutumika wakati timu haihitaji kujua mambo katika kiwango cha mtu binafsi. Kwa mfano, timu haihitaji kuhoji jamii kujua kama kuna mpango wa usimamizi wa shughuli za uvuvi, badala yake timu inaweza kuuliza Mkurugenzi wa Ofisi ya Uvuvi. Vigezo vingi vilivyokusanywa kwa kutumia wahojiwa maalum vimesaidia kujibu hoja nyingi za kimsingi (kwa mfano, sensa za watu katika jamii, kuwapo kwa bodi rasmi ya usimamizi).

*Kuna maana nyingi za neno kaya. Ni muhimu kuelezea kinagaubaga **kaya ni nini** tangu mwanzo wa uperembaji na kuendelea kutumia maana hiyo. Hii ni muhimu katika Kanda hii ambako kuna familia zenye wake wengi ni kawaida na familia pana zinaishi katika nyumba moja. Maana ya kawaida ni ile ya "chungu kimoja cha kupikia", yaani "watu wanaokula na kutumia kipato kwa pamoja." Ni muhimu kukubaliana na wahojiwa juu ya maana kabla kuanza mahojiano.*



Ni muhimu kuhoji watu maalum walio wengi kupata undani wa hali halisi. Matumizi ya kanuni ya dole gumba itumike kubaini kama idadi inayofaa imepatikana kuhusu waliokwisha hojiwa kuhusiana na kigezo fulani. Hii inafanywa kama majibu ya maswali yanayoulizwa yanajirudiarudia. Mfano: kama timu inauliza kuhusiana na aina ya shughuli katika eneo la uchunguzi na wahojiwa wote wanatoa majibu yaliyosawa, hivyo timu itaacha kuulizia juu ya kigezo hiki.

Mahojiano na kundi maalum la wahojiwa (FGIs) inahusisha makundi maalum yaliyoteuliwa kama wahojiwa (mara nyingi 4 hadi 10) ambao wana ufahamu na utaalam mmoja (kwa mfano: matumizi mamoja ya rasilimali, lugha moja, umri/rika moja au ni wanachama wa shirika moja). Washiriki wa makundi maalum wanaweza kuchaguliwa kama wale watu maalum kwa misingi ya ujuzi au elimu yao, kazi zao, au mapenzi yao katika shughuli. Vile vile wanaweza kuchaguliwa bila ya utaratibu maalum kutoka katika kundi la watumiaji. Kama ilivyo kwa wahojiwa maalum, makundi maalum pia yanahusishwa kutoa uelewa wao au habari za kundi kubwa la watu kwa jumla wanaloliwakilisha. Mahojiano na kundi maalum la wahojiwa (FGIs) mara nyingi huchaguliwa kutokana na kilichodokezwa kutoka kwa mijadala. Utaratibu huu ambao unakubali mabadiliko humsaidia muwezeshaji kuhoji kupata majibu, na kufuatilia yale maswali ya awali na kufuatilia maeneo mapya ya maswali wakati wa mahojiano. Mbinu hii ya uwazi inaruhusu kubadilishana habari baina ya muwezeshaji na muhojiwa. Wahojiwa kutoka makundi maalum kama wamewezeshwa vizuri hutoa habari zenye uhakika zaidi kuliko muhojiwa kutoka wahojiwa maalum.

Ni muhimu timu kuelewa vizuri makundi ya wadau (hali hii inaweza kuchunguzwa katika mahojiano ya watu maalum na uangalizi), mambo yenye vipaumbele na uendeshaji wa mambo ya ndani. Timu inaweza kutumia ujuzi huu kumulika mahojiano na kundi la wahojiwa (FGIs) kwa ajili ya masuala maalum, na kuhakikisha washirika muafaka wanaitwa.

### 3.3.3 UCHUNGUZI

Uchunguzi katika mwongozo wa SocMon unahusisha hojaji au karatasi yenye mpangilio wa maswali na majibu mafupi. Karatasi hii ina maswali yaliyopangwa yakitaraji majibu mafupi mafupi (kwa mfano ya kuchagua, ndiyo/hapana), yakilenga kutoa takwimu zinazoweza kuchambuliwa kwa kufanya hesabu.

Uchunguzi ni muhimu kwa kuelewa hali za kaya na watu binafsi. Kwa mfano, kama timu inahitaji kujua mawazo ya watu kuhusu shughuli za usimamizi wa pwani, basi inabidi kuuliza watu mbalimbali. Vigezo vingi vilivyo pitiwa katika uchunguzi vinaonyesha uelewa (kwa mfano, thamani zisizouzika na zisizotumika, ufahamu wa matatizo ya kijamii). Uchunguzi una uzuri wa kuwa hauhitaji msomi wa hali ya juu kufanya mahojiano, ni rahisi kuushughulikia, na huhitaji muda mchache kuliko ule wa wahojiwa maalum. Hata hivyo, uchunguzi una ubaya kwamba ni vigumu kubaini kama wahojiwa wanatoa habari ambazo anayehoji anataka kusikia tu, na ni vigumu kuuliza maswali nyeti yanayohusu kipato.Wahojiwa pia hawawezi kuuliza maswali mengine.

Maelekezo ya uchunguzi katika mwongozi huu wa SocMon (Kiambatanisho C), yametayarishwa kwa madhumuni ya kuwa muhojiwa azungumze kwa niaba ya kaya yake. Matokeo yake, kwahivyo yanakuwa katika ngazi ya kaya. Hatahivyo, timu kama inapendelea ngazi ya watu binafsi, inaweza ibadilishe maswali waulize yanayohusu watu binafsi. Kwa mfano, kwa kigezo cha *Shughuli za baharini (S12)*, muhojiwa ataje matumizi yake yote yanayohusu rasilimali za pwani na baharini (siyo matumizi ya watu wa kaya yake).

Kupata undani zaidi wa baadhi ya vigezo, ingefaa kuingiza maswali yenye majibu ya ndiyo/hapana, na yale ya nusu mpangilio. Maswali haya yanaweza kuongezwa moja kwa moja kwenye maelekezo ya kuhoji. Katika kuandaa maswali haya, ni vizuri kufikiria "nani, nini, lini vipi, na kwa nini". Kwa mfano, kigezo *himasheria (S23)* kinauliza kwa kiasi gani sheria na kanuni zinatiliwa nguvu. Maswali ya nusu mpangilio yangekuwa "Nani hutilia nguvu sheria na kanuni?" na "Kwa nini sheria na kanuni hazitiliwi nguvu ipasavyo?" (tazama *Mwongozo wa GCRMN, Sura ya 3, mahojiano ya nusu mpangilio*).

### 3.3.4 UANGALIZI

Katika masuala fulani takwimu zinaweza kukusanywa kupitia uangalizi. Uangalizi unatoa maelezo kuhusiana na sifa/tabia na mara nyengine, wingi/ukubwa wa yale ambayo mwanatimu anayaona, na maelezo haya yanapatikana kwa kuangalia kwa makini na kulinganisha na hali ya mazingira yanayohusika. Kwa mfano, mwanatimu anaweza kukusanya habari juu ya mtindo wa maisha kwa vifaa kwa kuangalia nyumba ya mtu fulani, kuanzia paa, ukuta sakafu na vifaa vilivyotumika kutengenezea madirisha. Uangalizi ni mbinu inayofaa kwa sababu timu inaweza kujifunza habari halisi ya masuala magumu au yanayotatanisha, kama vile marika ya watu wanaovua. Tabia nyingi katika shughuli hizi zinaeleweka si kwa kusema/kuelezwa ila kwa kuangalia na kutenda, kwahivyo ni vigumu kuzielezea. Kwa mfano, ni vigumu kwa wavuvi kueleza kila kitu wanachofanya wakiwapo baharini.

Uangalizi unafanyika wakati wote wa kukusanya takwimu ugani ingawaje uangalizi mwanzoni mwa ukusanyaji takwimu ni muhimu kwa kuandaa maswali ya mahojiano na ya uchunguzi. Nafasi ya uangalizi mara nyingi hujitokeza wakati wa uchunguzi na mahojiano.



## 3.4 NANI AHOJIWE WAKATI WA UCHUNGUZI?

Timu ya uperembaji lazima ibuni mbinu yake ya kubaini watu gani wahojiwe wakati wa kufanya uchunguzi. *Mwongozo wa GCRMN, Kiambatanisho B: Mbinu za kupata sampuli* unatoa maelezo ya kutosha namna ya kuchagua idadi zifaazo za watu wa kuhojiwa na namna ya kuwabaini (bila ya utaratibu maalum na hata kwa utaratibu maalum). Uchaguzi wa watoa habari wakati wa uchunguzi utategemea lengo kuu la uperembaji wa kiuchumi na kijamii. Kwa mfano, kama lengo ni kuelewa masuala ya uvuvi, basi sampuli ya wavuvi itachunguzwa. Kama lengo ni kuelewa mawazo ya jamii kwa jumla kuhusu masuala ya pwani, basi sampuli ya kaya itachunguzwa. Timu inaweza kujadili mipango ya sampuli na ukubwa wa sampuli wakiwa na wataalam wa mahesabu katika Ofisi ya wataalam au chuo Kikuu kilichopo karibu.

Uamuzi muhimu ni kama kuhoji sampuli ya watu isiyo na utaratibu maalum au yenye utaratibu maalum. Uamuzi huu utategemea kama matokeo yatahitaji uiano wa uwakilishi wa jamii. Kama jibu ni ndiyo, basi itafaa kukusanya hesabu yenye uiano wa uwakilishi kama sampuli ya watu kwa kuchukua watu bila ya utaratibu maalum (tazama *Mwongozo wa GCRMN, Kiambatanisho B: Mbinu ya kufanya sampuli uk.233*, kwa Jedwali la sampli.

| Idadi kamili ya Watu | Ukubwa wa Sampuli |
|---|---|
| 100 | 25 |
| 200 | 40 |
| 300 | 60 |
| 400 | 70 |
| 500 | 80 |
| 1000 | 100 |

Katika hali ambayo timu haihitaji namba yenye uaino wa uwakilishi wa jamii nzima, basi sampuli ndogo zinaweza kutumika. Ingawa uiano uwakilishi wa jamii nzima haupo, matokeo yatatoa uelewa unaofaa wa jamii. Katika hali hizi, ukubwa wa sampuli zifuatazo unapendekezwa.

Kwa sampuli zisizo na utaratibu maalum ni vizuri kuchukuwa sampuli kutoka kwa makundi ya wadau wa aina mbalimbali kuhakikisha undani wa hali zote unapimwa.

Habari zilizokusanywa kutoka kwa vyanzo vya pili, na zile kutoka kwa mahojiano na wahojiwa maalum zinaweza kuwa na manufaa kwa ajili ya kuhakikisha undani wa watu katika jamii unahojiwa. Habari na takwimu za upili na zile kutoka kwa wahojiwa maalum zitajumuisha habari kutoka wadau mbalimbali katika jamii, na vilevile mtawanyiko wa watu mbalimbali kiumri, kijinsia, kielimu, kikabila, na dini. Timu inahitaji kuhoji watu katika uiano wenye usawa katika maeneo hayo. Kwa mfano, kama kuna 30% wakatoliki, 40% wabaptisti na 30% waevanjelika katika jamii, timu inahitaji kufanya mahojiano na karibu uwiano sawa na asilimia hizo za watu.

## 3.5 UPEREMBAJI UCHUKUE MUDA GANI?

Muda utakaohitajika kwa kufanyia kila tathimini ya kiuchumi na kijamii utatofautiana kulingana na hali na ukubwa wa jamii, ujuzi na vifaa vya kazi vya timu, ukubwa wa timu na idadi ya vigezo vilivyochaguliwa. Mara ya kwanza itachukuwa muda mrefu zaidi kwa vile utaratibu ni mpya na idadi ya vigezo inaweza kuwa ndefu zaidi kuliko ile itakayochaguliwa kwa ajili ya uperembaji wa baadaye. Kwa jumla, inakisiwa inaweza kuchukuwa kati ya wiki 3 mpaka 6 (yaani siku 17 hadi 30) za kufanya kazi ya uperembaji kama ifuatavyo:

*Shughuli ya Maandalizi* : siku 3-5
*Ukusanyaji wa takwimu kupitia vyanzo vya pili*: siku 3-5
*Ukusanyaji wa takwimu kupitia wahojiwa maalum na/makundi maalum ya wahojiawa*: siku 3-5
*Ukusanyaji wa takwimu kupitia uchunguzi*: siku 5-10
*Ujazaji wa takwimu siku*: 3-5
*Uchambuzi wa takwimu, uandikaji wa taarifa, uwasilishaji, na ushauriano: siku* 5-10.

Siku hizi za kazi halisi zinaweza kuongezeka zaidi ya muda huo kwani kila shughuli haitafuata moja kwa moja baada ya shughuli nyengine.

## 3.6 UPEREMBAJI UTAGHARIMU KIASI GANI?

Bajeti pia itategemea mahitaji, rasilimali zilizopo na gharama za mahali penyewe. Kwa jumla inatazamiwa vipengele vya bajeti vitajumuisha bila ya kusahau:

- Usafiri kwenye maofisi ya serikali kwa ukusanyaji wa takwimu kutoka vyanzo vya pili.
- Malipo ya wahojiwa 3-4
- Kalamu, karatasi na vifaa vya ofisi
- Ramani na ramani za chini ya bahari
- Usafiri wa kwenye eneo la uchunguzi (boti, gari)
- Utoaji wa nakala
- Kompyuta na vifaa vya msingi vya mchakato wa maneno
- Muda wa watendaji kwa ajili ya kuingiza takwimu, kumbukumbu, usimamizi wa takwimu, na maandalizi katika kompyuta na katika mafaili mbalimbali
- Vifaa ambavyo sio vya lazima: Kamera, kionambali, kinasa sauti, video kamera, mtambo wa kupimia mwelekea wa kijiografia.

## 3.7 UPEREMBAJI UFANYIKE MARA NGAPI?

Kwa kawaida, mpango wa uperembaji wa masuala ya kiuchumi na kijamii huanza kwa tathimini ya kimsingi ya kiuchumi na kijamii kutumia vigezo vyote, ambavyo hutoa msingi wa takwimu za kufanyia marejeleo baadaye. Uperembaji wa baadaye unaweza kutumia orodha ndogo ya vigezo kuliko ile ya mpango mzima kwa vile baadhi ya vigezo lazima vikusanywe katika msingi wa mara nyingi zaidi kuliko vingine. *Jedwali 4.1* na *4.2* katika *Sehemu 4*, mahali ambapo vigezo vinaelezwa, yanatoa mapendekezo ya mara ngapi ukusanyaji wa takwimu ufanyike kwa kila kigezo, kiwango cha chini kuanzia baada ya kila miaka 2 hadi 5. Timu itahitaji kubaini kiwango kinachofaa kutegemea hali na takwimu zinazohitajika kwenye eneo. Kwa mfano, katika maeneo ambayo kuna mabadiliko makubwa ya watu na ya kiuchumi, takwimu zitahitajika kukusanywa katika msingi wa mara kwa mara ili kupima welekea, ambapo katika maeneo yasiyo na mabadiliko ya kijamii, takwimu siyo lazima kukusanywa mara kwa mara. Misimu huathiri sana shughuli za pwani katika Kanda ya Magharibi mwa Bahari Hindi. Hii lazima izingatiwe katika uperembaji, na ni vyema kufuatilia baadhi ya vigezo katika misimu tofauti, kwa kila mzunguko wa uperembaji (kwa mfano, utaratibu wa matumizi, shughuli za watu).

### 3.8 UPEREMBAJI UFANYIKE WAPI?

Ukusanyaji wa takwimu kwa jumla utafanyika katika maeneo mawili:

- Nje ya eneo la uchunguzi  chanzo cha pili cha takwimu hasa hasa hupatikana katika maofisi ya kiserikali, vyuoni kwenye tafiti mbalimbali, mashirika yasiyo ya  kiserikali, na ofisi nyenginezo, ambazo mara nyingi ziko nje ya eneo la uchunguzi.
- Ndani ya eneo la uchunguzi  Uchunguzi, uangalizi, na idadi kubwa ya mahojiano na wahojiwa maalum na makundi maalum ya wahojiwa yatafanyika katika eneo la uchunguzi.

### 3.9 NI IPI HADHIRA YA MATOKEO?

Kabla hujafanya juhudi ya uperembaji wa kiuchumi na kijamii, ni muhimu kutambua nani mlengwa wa/hadhira ya matokeo ya zoezi hilo. Kwa kuwafamu walengwa wa matokeo ya kiuchumi na kijamii,  mchakato na matokeo yanaweza kufanywa kwa njia ambayo italeta ufanisi katika kuwasilisha matokeo.

Katika kubaini hadhira lengwa, ni vizuri kufikiria ni nani atakaye athirika na matokeo, kwa uzuri na ubaya. Nani atakeyeathirika itategemea malengo makuu ya habari za kiuchumi na kijamii kama ilivyoelezwa katika *Sehemu 2*. Kwa mfano, kama kusudio la uperembaji ni kutathimini utendaji wa bodi ya usimamizi, hivyo hadhira lengwa itakuwa hiyo bodi, pamoja na yeyote anayeyevutiwa na utenda kazi wake, kama vile watu na taasisi zinazosimamia bodi hiyo ya usimamizi (kwa mfano, Idara ya Hifadhi za Bahari, umma, hususan makundi mbalimbali ya wadau (mfano-wavuvi, wanaoendesha utalii).

Ni muhimu pia kufikiria nani watachukuwa hatua kuhusiana na matokeo. Kwa mfano, kama lengo ni kuwafanya wadau washiriki, basi wadau ni muhimu kuwa sehemu ya hadhira.

Mwisho, ni vizuri kufikiria nani watahitajika kila mara kuelezwa shughuli za usimamizi wa pwani na hali za kiuchumi na kijamii. Katika hali nyengine hii inaweza kuwa jamii nzima, katika hali nyengine taasisi za kiserikali au bodi za ushauri

### 3.10 YAPI MENGINE NINAWAJIBIKA KUJUA?

Ni muhimu kutambua miradi yoyote ya kimaendeleo au tafiti zilizofanyika hivi karibuni ambazo zinaweza kuwa zilijumuisha tathimini ya kiuchumi na kijamii. Mchakato wake na matokeo yake lazima yapitiwe kama takwimu na habari ya kulinganishia na kabla kuanza kukusanya takwimu za *uperembaji wa kiuchumi na kijamii* ili kuepuka kurudia kwa mara ya pili. Kama kuna shughuli zozote zinazoendelea katika eneo la uchunguzi zinazofanya uchambuzi wa kiuchumi na kijamii, ni vizuri kuchunguza kama uchambuzi huo unafaa kwa *uperembaji wa kiuchumi na kijamii* na kujaribu kujumuisha au kuunganisha shughuli hiyo. Hii ni muhimu kupunguza mwingiliano katika jamii husika. Mara kwa mara jamii huchoshwa na mahojiano mengi.

Kama ilivyodokezewa katika *Sehemu 1*, mwongozo huu unalengwa kutumika kwa pamoja na ule *Mwongozo wa GCRMN*. Ni vyema kupitia tena *Sura ya 1:  Maandalizi ya shughuli* na *Sura ya 2:  Kupeleleza na Kupanga* kabla ya kuanza ukusanyaji wa takwimu. *Sura ya 3: Ukusanyaji wa takwimu ugani* ni muhimu mno ili kuelewa namna ya kufanya mahojiano.

Mwisho, ni muhimu kwa mpango wa uperembaji kutumia mbinu thabiti ili kuruhusu mlinganisho wa matokeo ya muda husika. Kwa mfano, kama baadhi ya vigezo vilifuatiliwa katika msimu mmoja, ni vizuri kila mara kufuatilia vigezo hivi hivi katika muda mwengine kama ule. Sawa na hivyo, kama maana ya "kaya" imekubalika pale mwanzoni mwa mpango wa uperembaji, maana hii lazima itumike hata badaye, ili takwimu ziwakilishe kipimo kile kile cha jamii, na ziweze kulinganishwa baadaye.

# Sehemu Ya 4: NIKUSANYE TAKWIMU ZIPI?

## 4.1 VIGEZO NI VIPI?

Mwongozo huu wa uperembaji wa masuala ya kiuchumi na kijamii unaangazia vigezo 54 vya kiuchumi na kijamii, ambavyo vimewasilishwa kulengana na njia/mbinu za kukusanyia takwimu: Vyanzo vya pili/mahojiano na wahojiwa maalum/kuhoji makundi maalum ya wahojiwa na uchunguzi mbalimbali (*Jedwali 4.1*). *Kiambatanisho A* kinatoa maelezo ya kina juu ya kila kigezo, ikijumuisha kigezo hiki ni nini, na jinsi ya kukusanywa takwimu zake, jinsi inavyotakiwa kukichambua, na jinsi habari zake zinaweza kutumiwa na wasimamizi na wadau wengine. Kwa maelezo ya kina juu ya hivi vigezo na jinsi ya kufanya mahojiano angalia *Mwongozi wa GCRMN, Kiambatanisho A: Vipengele vya kiuchumi na jamii*, na *Sura ya 3: Kukusanya takwimu ugani*, mipangilio ya kuhojia, na mahojiano na makundi ya wahojiwa maalum.

*Kuweka muktadha wa ukusanyaji wa takwimu, kwanza timu inatakiwa kulielewa vyema eneo la uchunguzi (K1), Wadau (K2), Idadi ya watu (K4), Idadi ya kaya (K5) na shughuli zao (K18). Vigezo hivi vinaweza kuchunguzwa zaidi wakati wa mahojiano; hata hivyo, ili kuelewa sehemu ya kufanyia uchunguzi na watu wangapi wa kuwahoji, vigezo hivi vine lazima vidhihirishwe mwanzoni kabisa.*

*Kwa uchunguzi wa awali, timu inahitajika kukusanya takwimu juu ya vigezo vingi kuliko uchunguzi utakaofuata. Kwa kawaida, uchunguzi wa kimsingi unaohusisha vigezo vyote unafanywa, ili kuwa msingi wa takwimu za marejeo ya baadaye..Uperembaji wa baadaye utahusisha vigezo vichache kuliko uperembaji wa msingi kwa kuwa vigezo vyengine vitakusanywa mara nyingi zaidi kuliko vyengine Tazama Jedwali 4.1 kwa marejeo ya lini takwimu zikusanywe kwa vigezo vipi.*

Baadhi ya vigezo vichache, ikiwa ni pamoja na miaka, jinsia, na elimu vinakusanywa kupitia njia ya kuhoji watu maalum, kuhoji makundi maalum, pamoja na uchunguzi. Haya yanafanywa ili kuthibitisha matokeo na kwa sababu takwimu hizo mbili zinakamilishiana. Takwimu za wahojiwa maluum, makundi maluum ya wahojiwa na vyanzo vya pili hutoa mkusanyiko wa habari katika kiwango cha jamii au kiwango cha kundi ambazo hutumika kupima mabadiliko na mienendo kulengana na muda; ambapo, takwimu za uchunguzi hutoa maelezo mazuri na sawa kuhusu kaya, na watu binafsi katika eneo la uchunguzi. Kwa mfano, habari juu ya shughuli za kijamii na idadi ya watu (demografia) hutoa ufahamu wa jumla wa asilimia ya jamii ambayo imeajiriwa katika kila shughuli, na ni asilimia ngapi ya jamii ambayo iko katika umri fulani, kiwango cha elimu, n.k. Kinyume, habari za uchunguzi juu ya kazi na idadi ya watu zinaweza kutumika kukisia uasili (kabila) wa wadau, kama vile wavuvi, waelekezaji wa utalii.

Kwa vigezo vya uchunguzi inatakiwa ieleweke kwamba nusu ya vigezo hivi huuliza juu ya habari za kaya na shughuli za pwani na baharini za wahojiwa, ilhali ile nusu nyengine inaulizia ufahamu wa mhojiwa binafsi. Hii imefanyika ili kupata habari nyingi iwezenavyo kuhusu jamii hiyo kutoka kwa wahojiwa huku tukitilia maanani ya kwamba muhojiwa anaweza kuzungumza kwa usahihi kuhusu ufahamu wake na si wa watu kutoka kaya nyengine.

*Uangalizi hautiliwi mkazo sana kwa kila kigezo kwa sababu ni muhimu kwa vigezo vyote. Timu ya uperembaji inatarajiwa kutumia uangalizi kama njia ya mwanzo ya kufamu eneo la uchunguzi na kuthibitisha takwimu zilizokusanywa kupitia kwa vyanzo vya pili, wahojiwa maalum, na uchunguzi.*

## 4.2 NITUMIE VIGEZO VIPI?

Haiwezikani kufanya uchunguzi wa vigezo vyote katika mwongozo huu wa *SocMon*, hivyo basi inapendekezwa kwamba timu ya uperembaji ivipe kipaumbele vigezo kwa msingi wa mambo ya kuzingatia yafuatayo:

### 4.2.1 MALENGO YA HABARI ZA KIUCHUMI NA KIJAMII

La umuhimu ziadi, timu lazima ifafanue kwa nini takwimu zinakusanywa, na hasa jinsi zitakavyotumika baada ya kukusanywa. Kwa mfano, kama timu inahusika zaidi na kutambua matishio, basi lazima itazame vigezo vilivyoorodheshwa vya kutambua matishio. *Sehemu 2* inaelezea zaidi juu ya malengo mbalimbali ya kukusanya habari za kijamii na kiuchumi. Vigezo ambavyo vimepewa kipaumbele katika ukusanyaji wa takwimu ndani ya mwongozo huu vilichaguliwa kwa sababu vinafikia malengo hayo. *Jedwali 4.2* linaelezea ni vigezo vipi ambavyo ni muafaka kwa malengo yapi ili timu iweze kutambua kwa urahisi ni vigezo vipi vinafaa kwa mahitaji yake. Maelezo juu ya jinsi vigezo vinavyoweza kutumika kuelewa kila mojawapo ya malengo haya yametolewa katika sehemu ya *Umuhimu wa habari hizi kwa wasimamizi na wadau wengine* kwa kila kigezo katika Kiambatanisho A.

### 4.2.2 UMUHIMU WA UKUSANYAJI WA TAKWIMU KWA UJUMLA.

Inakubalika kwamba vigezo vyote vya demografia vilivyoorodheshwa ni vya muhimu, na kama takwimu zinapatikana, vinatakiwa kuchunguzwa kama ikiwezekana. Kama habari za kuaminika za demografia hazipatikani, na rasilimali zinatakiwa kupewa kipaumbele, msimamizi atazame moja kwa moja vigezo vinavyofaa kwa malengo yake ya usimamizi. Wakati mwengine malengo ya uperembaji wa masuala ya kijamii na kiuchumi yanaweza yasieleweke, na wakati pamoja na vifaa vilivyoko vinaweza kutoruhusu timu kuchunguza vigezo vyote. Kwa hali hizo alama * inaonyesha vigezo muhimu zaidi vinavyotakiwa kuvikusanyia takwimu endapo vifaa vya kuperembea havitoshi na sehemu ndogo tu ya vigezo inaweza kupimwa, kwa misingi ya 1) umuhimu kwa usimamizi, 2) urahisi wa kukusanya takwimu, na 3) uwezekano wa kutoa habari mpya.

### 4.2.3 HALI HALISI KATIKA ENEO

Pengine kitu muhimu, timu inatakiwa kuchagua vigezo kwa misingi ya masuala yaliyo muhimu katika eneo la uchunguzi. Kwa mfano, kama usimamizi wa taka ni suala muhimu, basi timu inaweza kutoa kipaumbele kwa miundombinu katika jamii na kuongezea maswali mengine zaidi halisi juu ya usimamizi wa utupaji taka.

Timu pia inahitajika kufikiria mabadiliko yanayotarajiwa katika usimamizi na katika jamii. Kwa mfano, kama utalii unaongezeka, basi timu inaweza kuongeza maswali yanayohusiana na biashara ya utalii na athari zake.

*Jedwali 4.1-* **MAELEKEZO.**

Jedwali hili limeorodhesha vigezo katika aina mbalimbali na mbinu/njia za kukusanyia takwimu. Jedwali linaonyesha hasa umuhimu wa kila kigezo, ikijumuisha mbinu kuu ya kukusanyia takwimu, mara chache kabisa za kukusanya takwimu na umuhimu kwa jumla wa kukusanya takwimu. Alama * inaashiria kwamba kigezo kinachukuliwa kuwa muhimu sana kwa wasimamizi ikiwa malengo ya uperembaji hayako wazi.

Vigezo katika mwongozo huu wa *SocMon (tazama Sehemu 4 na Kiambatanisho A)* vimewekwa kulengana na aina pamoja na njia/mbinu za kukusanyia takwimu: vyanzo pili, wahojiwa wakuu, na/au makundi maalum ya kuhojiwa zimewekwa pamoja na kupewa 'K', na uchunguzi kupewa 'S'. Ziligawanywa katika hali hii ili kuwiana na aina mbili za miongozo ya mahojiano: mmoja wa vyanzo vya pili, wahojiwa wakuu na makundi ya watu maalum, na ule mwengine ni wa uchunguzi.

Ni muhimu kusisitiza tena kwamba mwongozo huu wa *SocMon* si mwongozo usioweza kubadilishwa. Mtumiaji wa mwongozo huu, timu ya uperembaji wa mambo ya kiuchumi na kijamii, inatarajiwa kuchagua vigezo (kuongezea kwa, au kupunguza kutoka kwa, vile vigezo vilivyopewa kipaumbele katika mwongozo huu), na njia muafaka kulengana na mahitaji ya eneo husika kama ilivyoonyeshwa katika *Sehemu 4.2.*

Kwa kawaida, takwimu zinatakiwa zikusanywe kutoka vyanzo vya pili kwanza, zikifuatiwa na mahojiano na wahojiwa wakuu na/au makundi maalum ya wahojiwa. Kama takwimu zilizokusanywa kupitia mahojiano na wahojiwa wakuu na vigezo vya vyanzo pili zimetosha kufikia malengo ya timu, basi hakuna haja ya kufanya uchunguzi zaidi. Hata hivyo, mara nyingi uchunguzi utafanyika ili kupata takwimu nyingi na halisi zinazohusiana na watu binafsi na kaya katika eneo la uchunguzi (tazama *Jedwali 4.1* kwa orodha ya vigezo vya vyanzo vya pili/wahojiwa wakuu/makundi maalum ya wahojiwa na vya uchunguzi, mtawalia. Uangalizi huwa wakuendelea tukiwa katika jamii.

**Jedwali 4.1 Vigezo vya SocMon vikiambatanishwa na njia za kukusanyia takwimu - (K) Chanzo pili/Wahojiwa wakuu/Kundi maalum la wahojiwa; (S) Uchunguzi.**

| Miongozo ya mahojiano kwa herufi | | Vigezo | Njia kuu za kukusanyia takwimu Uchunguzi: S Mahojiano: KI, FGI; Vyanzo pili: Sec. | Mara za kukusanya takwimu (miaka) | Umuhimu wa jumla wa kukusanya takwimu |
|---|---|---|---|---|---|
| ***Eneo*** | | | | | |
| K1 | | Eneo la uchunguzi | Sec.,KI, FGI | 5 | * |
| ***Wadau*** | | | | | |
| K2 | | Wadau | KI | 3 | * |
| K3 | | Uwajibikaji wa kijinsia na majukumu | KI, FGI | 5 | |
| ***Demografia*** | | | | | |
| K4 | | Idadi ya watu | Sec. | 5 | * |
| K5 | | Idadi ya Kaya | Sec., KI | 5 | |
| K6 | | Kiasi cha uhamiaji | Sec. | 5 | |
| K7 | S1 | Kazi | Sec., S | 5 | * |
| K8 | S2 | Umri | KI, FGI, S | | * |
| K9 | S3 | Jinsia | Wote | 5 | * |
| K10 | S4 | kabila (asili) | Sec., S | 5 | * |
| K11 | | Uwezo wa kusoma na kuandika | Sec. | | |
| K12 | S5 | Elimu | Sec., S | 5 | |
| K13 | S6 | Dini | Sec., S | 5 | |
| K14 | S7 | Lugha | Wote | 5 | |
| | S8 | Ukubwa wa kaya | Sec., S | 5 | |
| | S9 | Muundo wa kaya | S | 5 | |
| | S10 | Vyanzo vya mapato | S | 5 | * |
| | S11 | Makazi | S | 3 | |
| ***Afya*** | | | | | |
| K15 | | Vifo vya watoto wachanga, kuenea kwa magonjwa | Sec., KI | 3 | |
| ***Miundombinu na Biashara*** | | | | | |
| K16 | | Miundo mbinu ya kijamii, mendeleo ya kibiashara na umiliki | KI, FGI | 5 | * |
| K17 | | Vyanzo na upatikanaji wa mikopo | KI, FGI | 3 | |

| Miongozo ya mahojiano kwa herufi | | Vigezo | Njia kuu za kukusanyia takwimu Uchunguzi: S Mahojiano: KI, FGI; Vyanzo pili: Sec. | Mara za kukusanya takwimu (miaka) | Umuhimu wa jumla wa kukusanya takwimu |
|---|---|---|---|---|---|
| ***Shughuli za pwani na baharini*** | | | | | |
| K18 | S12 | Shughuli | Wote | 2 | * |
| K19 | S13 | Huduma na bidhaa | KI, FGI, S | 2 | * |
| K20 | S14 | Njia/mbinu | KI, FGI, S | 2 | * |
| K21 | | Thamani ya bidhaa na huduma | KI, FGI | 2 | * |
| K22 | S15 | Soko lengwa na utaratibu wa uuzaji na ununuzi | KI, S | 2 | * |
| K23 | | Utaratibu wa matumizi | KI, FGI, | 2 | |
| K24 | | Kiwango cha matumizi ya watu kutoka nje | KI, FGI | 2 | * |
| K25 | | Viwango na aina za athari | KI, FGI | 2 | * |
| K26 | | Matumizi ya bidhaa na huduma | KI, S | | |
| K27 | S16 | Muundo wa Utalii | Sec., KI, FGI | 3 | |
| ***Usimamizi*** | | | | | |
| K28 | | Bodi ya usimamizi | Sec., KI | 3 | |
| K29 | | Mpango wa usimamizi | Sec., KI | 3 | |
| K30 | | Sheria wezeshi | Sec., KI | 3 | * |
| K31 | | Vifaa vya usimamizi | Sec., KI | 3 | |
| K32 | | Kanuni rasmi za umiliki | Sec., KI | 3 | * |
| K33 | | Kanuni zisizo rasmi za umiliki, mila na utamaduni | Sec., KI, FGI | 3 | |
| K34 | | Vivutizi/vishawishi vya jamii | Sec., KI, FGI | | |
| K35 | S17 | Ushirikishwaji na kuridhika kwa wadau | Sec. KI, S | 3 | * |
| K36 | | Mashirika ya kijamii na ya wadau | Sec., KI | 3 | * |
| | S18 | Uanachama katika mashirika na vikundi | S | 3 | |
| K37 | | Nguvu na ushawishi | KI, FGI | 2 | * |
| ***Mitazamo na ufahamu*** | | | | | |
| | S19 | Ufahamu wa hali ya rasilimali. | S | 3 | |
| | S20 | Ufahamu wa matishio | S | 3 | |
| | S21 | Ufahamu wa sheria na kanuni | S | 3 | |
| | S22 | Utii wa sheria | S | 3 | * |
| | S23 | Himasheria | S | 3 | * |
| | S24 | Ufahamu wa matatizo na masuluhisho ya usimamizi wa pwani | S | 3 | |
| | S25 | Ufahamu wa matatizo ya kijamii | S | 3 | * |
| | S26 | Mafanikio ya usimamizi wa pwani | S | 3 | * |
| | S27 | Changamoto katika usimamizi wa pwani | S | 3 | * |
| | S28 | Thamani isiyouzwa na isiyotumika | S | 3 | |
| ***Hali ya kiuchumi na kijamii*** | | | | | |
| | S29 | Mtindo wa maisha kwa vifaa | S | 3 | * |

Jedwali 4.2 linadhamiria kuwasaidia wasimamizi kuvipa vipaumbele vigezo vya kuperemba kulingana na malengo na shabaha ya usimamizi wa rasilimali za pwani katika eneo husika.

| | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | ***Ya msingi*** | | | ***Demografia*** | | | | | | | | |
| **LENGO KUU** | Eneo la uchunguzi | Wadau | Majukumu na wajibu wa kijinsia | Idadi ya watu | Idadi ya kaya | Kiwango cha uhamiaji | Kazi | Umri | Jinsia | Ukabila | Uwezo wa kusoma na kuandika | Elimu |
| | **K1** | **K2** | **K3** | **K4** | **K5** | **K6** | **K7S1** | **K8S2** | **K9S3** | **K10S4** | **K11** | **K12S5** |
| **Kutambua matishio, matatizo, utatuzi na uwezekano** | | | | | | | | | | | | |
| Matishio | ● | | | ● | ● | ● | ● | | | | | |
| Matatizo | | | ● | | | | | | | | | |
| Utatuzi na uwezekano | | | | | | | | | | | | |
| **Kadiria umuhimu, thamani na umuhimu wa kitamaduni wa rasilimali na matumizi yake** | | | | | | | | | | | | |
| Umuhimu/Thamani | | | | | | | | | | | | |
| Umuhimu wa kiutamaduni | | | ● | | | | | | | | | |
| **Kukagua matukio mazuri na mabaya ya hatua za usimamizi** | | | | | | | | | | | | |
| Hali ya maisha | | | ● | ● | | | ● | | | ● | ● | ● |
| Soko na uzalishaji | | | | | | | | | | | | |
| Upatikanaji wa Chakula | | | | | | | ● | | | | | |
| Mitazamo na ufahamu | | ● | | | | | | | | | | |
| Shughuli za Pwani na Baharini | | | | | | | ● | | | | | |
| Utawala | | | | | | | | | | | | |
| **Kukadiria namna ya utendaji wa bodi ya usimamizi** | | | | | | | | | | | | |
| Ufanisi wa usimamizi | | | | | | | | | | | | |
| **Kujenga ushiriki wa wadau na mipango muafaka ya elimu na uhamasishaji** | | | | | | | | | | | | |
| Ushiriki wa wadau | | ● | ● | ● | | | ● | ● | ● | ● | ● | ● |
| Mpango wa uhamasishaji | | | | | | ● | | | ● | | | |
| **Kuhakikisha na kuweka katika maandishi yanayodhaniwa juu ya hali ya kiuchumi na kijamii katika eneo, mabadiliko ya kijamii na ufahamu wa wadau** | ● | ● | ● | ● | ● | ● | ● | ● | ● | ● | ● | ● |
| **Kuanzisha taarifa za msingi za umbo la kaya na jamii.** | ● | ● | ● | ● | ● | ● | ● | ● | ● | ● | ● | ● |

## JEDWALI 4.2 MALENGO YA UPEREMBAJI MASUALA YA KIUCHUMI NA KIJAMII NA VIGEZO MUAFAKA

| Demografia | | | | | | Afya | Miundombinu na biashara | | Shughuli za pwani na baharini | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Dini | Lugha | Ukubwa wa kaya | Muundo wa Kaya | Vyanzo vya mapato | Makazi | Vifo vya watoto, magonjwa yaliyopo | Miundombinu, maendeleo ya biashara na umiliki | Mikopo, vyanzo na upatikanaji | Shughuli za baharini | Bidhaa na Huduma | Njia/mbinu | Thamani ya bidhaa na huduma | Masoko lengwa, uendeshwaji wa masoko | Utaratibu wa matumizi | Kiwango cha matumizi kwa watu wa nje | Viwango na aina za athari | Matumizi ya bidhaa na huduma | Umbo la utalii |
| K13S6 | K14S7 | S8 | S9 | S10 | S11 | K15 | K16 | K17 | K18S12 | K19S13 | K20S14 | K21 | K22S15 | K23 | K24 | K25 | K26S16 | K27 |
| | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | ● | ● | ● | ● | ● | | | ● | ● | ● | | |
| | | | | | ● | ● | ● | ● | | | | | | ● | | | | |
| | | ● | | | | | | ● | | | | | | ● | | | | |
| | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| | | | | ● | | | | | | | | | ● | ● | ● | | ● | |
| | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| ● | | | | ● | ● | | ● | | ● | ● | ● | ● | | | | | ● | |
| | | | | | | | | ● | | ● | ● | ● | ● | | | | | |
| | | | ● | ● | ● | ● | | | | ● | ● | ● | ● | | | | ● | |
| | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | ● | ● | ● | | | | ● | ● | | |
| | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | ● | ● | ● | | | ● | ● | ● | | |
| | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| ● | ● | | | | | | | | | | ● | | | | ● | | | |
| | | | | | ● | ● | ● | | ● | ● | ● | | | | ● | ● | | |
| ● | ● | ● | ● | ● | ● | ● | ● | ● | ● | ● | ● | ● | ● | ● | ● | ● | ● | ● |
| ● | ● | ● | ● | ● | ● | ● | ● | ● | ● | ● | ● | ● | ● | ● | ● | ● | ● | ● |

| | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | ***Utawala*** | | | | | | | | | | |
| **LENGO KUU** | Bodi ya usimamizi | Mpango wa usimamizi | Sheria wezeshi | Nyenzo za usimamizi | Umilikaji na utaratibu wa kawaida | Umilikaji na utaratibu usio rasmi, mila na desturi | Vivutio kwa jamii | Ushirikishwaji na kuridhika kwa wadau | Mashirika ya kijamii na ya wadau | Uanachama katika mashir ka ya wadau | Nguvu na ushawishi |
| | **K28** | **K29** | **K30** | **K31** | **K32** | **K33** | **K34** | **K35S17** | **K36** | **S18** | **K37** |
| **Kutambua matishio, matatizo, utatuzi na uwezekano** | | | | | | | | | | | |
| Matishio | | | | | | | | | | | |
| Matatizo | | | | | | | | | | | ● |
| Utatuzi na uwezekano | | | | | | | | | | | ● |
| **Kadiria umuhimu, thamani na umuhimu wa kitamaduni wa rasilimali na matumizi yake** | | | | | | | | | | | |
| Umuhimu/Thamani | | | | | | | | ● | | ● | |
| Umuhimu wa kiutamaduni | | | | | | ● | | | | | |
| **Kukagua matukio mazuri na mabaya ya hatua za usimamizi** | | | | | | | | | | | |
| Hali ya maisha | | | | | | | | | | | |
| Soko na uzalishaji | | | | | | | | | | | |
| Upatikanaji wa Chakula | | | | | | | | | | | |
| Mitazamo na ufahamu | | | | | | | | | | | |
| Shughuli za Pwani na Baharini | | | | | | | | | | | |
| Utawala | | | | | | | | | | | |
| **Kukadiria namna ya utendaji wa bodi ya usimamizi** | | | | | | | | | | | |
| Ufanisi wa usimamizi | ● | ● | ● | ● | ● | ● | ● | ● | ● | ● | |
| **Kujenga ushiriki wa wadau na mipango muafaka ya elimu na uhamasishaji** | | | | | | | ● | | | | |
| Ushiriki wa wadau | | | | | | | ● | ● | ● | ● | ● |
| Mpango wa uhamasishaji | | | | | | | ● | | | | |
| **Kuhakikisha na kuweka katika maandishi yanayodhaniwa juu ya hali ya kiuchumi na kijamii katika eneo, mabadiliko ya kijamii na ufahamu wa wadau** | ● | ● | ● | ● | | | ● | ● | ● | ● | ● |
| **Kuanzisha taarifa za msingi za umbo la kaya na jamii.** | ● | ● | ● | ● | | ● | ● | ● | ● | ● | ● |

## TABLE 4.2 GOALS OF SOCIOECONOMIC MONITORING AND RELEVANT VARIABLES *(CONTINUED)*

| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| ***Mitazamo na ufahamu*** | | | | | | | | | | ***Hali ya kiuchumi na kijamii.*** |
| Ufahamu wa hali ya rasilimali | Ufahamu wa matishio | Ufahamu wa sheria na kanuni | Utii wa sheria | Himasheria | Ufahamu wa matatizo na masuluhisho ya usimamizi wa pwani | Ufahamu wa matatizo ya jamii | Mafanikio ya usi amizi wa pwani | Changamoto katika usimamizi wa pwani | Thamani isiyouzika na isiyotumika | Mtindo wa maisha kwa vitu |
| **S19** | **S20** | **S21** | **S22** | **S23** | **S24** | **S25** | **S26** | **S27** | **S28** | **S29** |
| | | | | | | | | | | |
| ● | ● | | | | | | | | | |
| | | | ● | ● | ● | ● | | | | |
| | | | | | ● | | ● | ● | | |
| | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | ● | |
| | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | ● |
| | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | |
| ● | ● | ● | ● | ● | ● | ● | ● | ● | ● | |
| | ● | | | | | | | | | |
| | | | | ● | | | | | | |
| | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | ● | ● | | |
| | | | | | | | | | | |
| | ● | ● | ● | | | | ● | ● | | |
| ● | ● | ● | | | | | | | ● | |
| ● | ● | ● | ● | ● | ● | ● | ● | ● | ● | ● |
| ● | ● | ● | ● | ● | ● | ● | ● | ● | ● | ● |

## 5.1 UCHAMBUZI

Uchambuzi wa takwimu ni kazi inayofanyiwa na timu nzima ya uperembaji. Wakati wa kipindi cha kukusanya takwimu timu inatakiwa ikutane mara kwa mara ili kuthibitisha, kuelezea, kusawazisha mafunzo muhimu, kutafsiri matokeo, kuthibitisha mafunzo muhimu na kupanga kuwasilisha matokeo. Kutokana na haya, uchambuzi mwingi wa takwimu, hasa ule unaohusiana na tabia/sifa/aina za vitu mbalimbali ufanyike wakati wa kukusanya takwimu ugani. Uchambuzi wa mwisho unaofanyika mwisho wa ukusanyaji wa takwimu utakuwa ni wa kupitia tu na kuhitimisha uchambuzi wa ugani.

*Mafunzo muhimu ni masuala yaliyotambuliwa au mafunzo timu ilisoma ambayo ni muhimu kwa malengo ya uperembaji au yanayo takikana kufahamu muktadha wa kiuchumi na kijamii wa wadau. hivi hutoa maelezo ya somo husika linalo fanyiwa kazi na timu hiyo. Vitu hivyo nivyamuhimu sana katika malengo ya uchunguzi, wakati mwingine pia zieleze juu ya uchumi na jamii husika. Tazama Mwongozo wa GCRMN, Sura 4: Uchambuzi wa mwisho wa takwimu kwa habari zaidi za mafunzo muhimu na kanuni za msingi za uchambuzi.*



Kuna hatua nyingi muhimu ambazo timu ya uperembaji lazima ifanye kwa pamoja kwa ajili ya kuchambua (kueleza kwa mapana) takwimu.

1. **Kukusanya takwimu zote pamoja** kwa kuweka pamoja miongozo yote kutoka kwa vyanzo pili, mahojiano na watoa habari wakuu, na miongozo ya uchunguzi (Kiambatanisho B & C).
2. **Kuandaa takwimu** kwa kuhamisha takwimu zilizokusanywa kutoka kwa chanzo pili, mahojiano na watoa habari wakuu na uchunguzi kwa karatasi ya uchambuzi wa tawimu (Kiambatanisho D & E).
3. na/au moja kwa moja takwimu zijazwe ili zihifadhiwe na zichambuliwe katika SocMon WIO database iliyotolewa. (*Tazama maelekezo ya SocMon WIO database mahali pengine*). Hii ni muhimu ili kuhakikisha uwekaji pamoja wa takwimu na usalama wake, na kurahisisha uchambuzi, utoaji wa taarifa na ushirikiano katika kanda
4. **Kutafsiri takwimu** kwa kupitia matokeo kutoka karatasi za uchambuzi ili kuzitambua na kuzipanga habari zinazohusiana na malengo ya awali ya uperembaji wa kijamii na kiuchumi *(tazama Sehemu 2).* Timu niichague takwimu zinazofaa kwa malengo ya uperembaji (*tazama Jedwali 4.2 katika sehemu ya 4* ili kuelewa ni takwimu za vigezo vipi zitatumika kwa kuchambua malengo yapi).Takwimu hizi baadaye ziangaliwe tena, zilinganishwe na zitofautishwe ili kuona mitindo na mienendo. Mitindo na mienendo vitakua vielelezo vizuri vya **mafunzo muhimu**. Matokeo yanakusanywa ili kupata takwimu zitakazo thibitisha mafunzo hayo.

   Kwa mfano, kama lengo la uperembaji ni kuonyesha athari za kijamii za kanuni isiyoruhusu watu kuvua, basi baadhi ya vigezo viwili muhimu ni *kazi (K7, S1)*, na *shughuli (K18)*. Kwa uchambuzi, kunaweza kuwa na muenendo fulani katika kazi na shughili kadri watu wanavyogeuka kutoka uvuvi hadi katika shuguli na kazi nyengine. Kama kuna mabadiliko ya kuacha shughuli ya uvuvi, funzo kuu laweza kuwa sheria na kanuni zimeathiri shughuli za uvuvi kama inavyodhihirishwa na watu kuacha shughuli ya uvuvi.. Kwa kuangalia tena, kulinganisha na kutofautisha takwimu hizi mbali mbali, inawezekana kuona mabadiliko katika kila kimojawapo ya hivyo vigezo. Kwa kila kigezo kuna maelezo ya jinsi ya kuchambua takwimu na kutumia habari hizo katika sehemu ya *Jinsi ya kuchambua takwimu* na *Umuhimu wa habari hizi kwa wasimamizi na wadau wengine* katika *Kiambatanisho A.*
5. **Kubalianeni juu ya funzo kuu** kwa kukubali funzo kuu na la muhimu zaidi ili liangaziwe, na kuchagua habari ili kuthibitisha funzo hilo
6. **Thibitisha matokeo** kwa kuzungumza na wadau funzo kuu kama sehemu ya mawasiliano yaliyoelezwa hapo chini. Tofauti zozote zitakazoonekana zisahihishwa na vyanzo asilia.

## 5.2 MAWASILIANO / MAREJESHO

Kitu **muhimu zaidi** cha mchakato wote wa uperembaji **ni kuwasilisha matokeo** yanayofungamana na malengo kwa hadhira. Hii inajumuisha kujadili matokeo na hadhira, kutafuta mapendekezo na kuyathibitisha, na kutafuta pia maamuzi na matendo muafaka ili kutumia matokeo hayo. Mchakato huu wa mawasiliano ni muhimu katika kurekebisha usimamizi wa pwani, ambao hutumia habari hizi ili kuboresha jinsi usimamizi utakavyofanyika mbeleni. Kwa mfano, kama lengo la uperembaji wa kiuchumi na kijamii ni kuelewa thamani na umuhimu wa miamba ya matumbawe, basi matokeo ya ufahamu wa watu juu ya thamani zisizouzika na zisizotumika

unaweza kutumika kuelewa thamani na umuhimu. Kama matokeo yanaonyesha kwamba watu wengi wanauelewa mzuri juu ya thamani ya kuhifadhi miamba ya matumbawe, basi hii inadhihirisha thamani kubwa ya miamba ya matumbawe. Habari hizi zinaweza baadaye kutumiwa na msimamizi kuwaonyesha watu na watunga-sera, umuhimu wa kutumia rasilimali katika kuhifadhi miamba ya matumbawe.

Kama ilivyojadiliwa katika *Sehemu 3.9*, hadhira lengwa ya matokeo haya watajumuisha wanajamii hadi watungasera na wasimamizi wa rasilimali za pwani. Kutokana na msimamo wenye maadili, inapendekezwa kwamba matokeo ya uperembaji wa kijamii na kiuchumi yawasilishwe kwa jamii hata kama jamii hiyo siyo hadhira iliyolengwa. Hii inafanyika kwa heshima ya wale wanajamii waliojitolea muda wao kusaidaia katika mahojiano. Hii itasaidia kuhakikisha kwamba kuna uhusiano mzuri na jamii kwa ajili ya kufanya kazi nao baadaye. Uchovu wa mahojiano ni shida kubwa katika juhudi zozote za kufanya uperembaji wa kiuchumi na kijamii, na jinsi watu wanavyohusika katika mchakato huo na wanavyopata matokeo ndivyo jinsi watakavyokubali kushiriki katika shughuli za uperembaji wa baadaye. Hivyo basi, ni muhimu kujadili kwa pamoja na wanajamii jinsi matokeo yatakavyo tumiwa na jinsi yatakavyoathiri usimamizi. Uperembaji pia utatumiwa moja kwa moja na jamii, hasa kwa kuwapa nafasi za kutoa maoni, kuidhinisha, au kutathmini sera au miradi, ambayo imewaathiri.

Katika kuyakinisha matokeo gani ya kuangazia na kushirikisha hadhira, timu inatakiwa ifikirie inatarajia kila hadhira itafanyia nini matokeo hayo, ikiwa ni pamoja na matendo au hatua watakazochukuwa. Inatakiwa pia kufikiria zile habari muhimu ambazo kila hadhira itakuwa inaangalia kutoka kwa hayo matokeo.

### 5.2.1 MBINU ZA KUFANYIA MAWASILIANO.

Matokeo ya uperembaji wa masuala ya kiuchumi na kijamii yanaweza kuwasilishwa kwa hadhira mbalimbali kupitia njia mbili kuu.

Njia ya kwanza ni ile ya moja kwa moja inayojumuisha mambo makuu yafuatayo;

- kutumia maandishi (karatasi, ripoti)
- takwimu za michoro (picha n.k)
- kwa kunena.
- vyombo vya habari (magazeti, majarida, redio, video n.k)
- kupitia mitandao

Njia ya pili ya mawasiliano ni ile ya majibizano na inajumuisha yafuatayo

- vikao vya kijiji (kitongoji) mfano baraza katika nchi za Kenya na Tanzania.
- mijadala kwa makundi
- mijadala ya ana-kwa-ana
- barua pepe
- mawasiliano ya mbali (simu, simu za video, kamera za mitandao n.k)

Mawasiliano kwa majibizano yana manufaa kwa sababu yanaleta umma katika mchakato wa uperembaji kwa kuwaruhusu watoe maoni yao juu ya matokeo. Kama kuna mbinu ya kuwajumuisha, basi kuna uwezekano mkubwa wa wao kuunga mkono na kuchukuwa hatua kulengana na matokeo.

Wakati wa kuamua mbinu ipi itumike, inapaswa timu izingatie maswali yafuatayo:

- Ni njia ipi ambayo wao walengwa wanaipendelea ya kupokea habari? Hii inaweza ifungamane na kiwango chao cha elimu na uwezo wa kiteknolojia. Kiwango cha kuweza kusoma na kuandika ni muhimu kuzingatiwa pamoja na ikiwa wanapenda kusoma habari, kusikiliza redio au kuangalia runinga. Je, wanaelewa matumizi ya kompyuta? Je, wanaweza kutumia mtandao wa inteneti? Je, wanakutana mara kwa mara katika mikutano au mabaraza? Ikiwa ni hivyo, ni lini?
- Je, wanapendelea mazungumzo ya kitaalam au kielimu kuliko mfumo wa mazungumzo ya kawaida? Ni wapi na jinsi gani mawasiliano kwa njia ya mazungumzo yanaweza kufanyika? Ni lugha ipi inayo tumika?
- Je, wanapendelea 'mikutano ya vijiji' au mikutano ya hadhara kama zile 'baraza' za Kenya na Tanzania panapokuwa na fursa ya mjadala wazi? Ni lugha gani inayotumika katika mikutano hii? Ni nani ahudhurie?

Kama kuna makundi ya watu wasiobahatika au waliosahaulika katika eneo hilo, ni muhimu kuchagua njia maalum za mawasiliano ili kukidhi mahitaji maalum ya watu hao, kama vile kuwa na mazungumzo maalum nao.

### 5.2.2 KUANDIKA TAARIFA.

Kama matokeo yanakwenda kuwasilishwa kwa njia ya maandishi, hivyo basi taarifa iwasilishwe kwa hadhira lengwa. Taarifa inaweza kuwa na maumbo mbalimbali kulingana na hadhira lengwa. Watumiaji wengi wa taarifa kama vile wakuu wa watengenezaji sera, au watoa-maamuzi wanaweza kuwa hawana haja sana na maelezo juu ya eneo la uchunguzi pamoja na jamii yake, lakini wanaweza kupenda kutaka kujua masuala mengine, matatizo na masuluhisho yake.Watumiaji wengine wa taarifa, kama vile watafiti na makundi mengine ya maendeleo yanayotaka kufanya kazi katika eneo hilo na wasimamizi wa pwani, wanaweza kuhitaji maelezo ya ndani ya hali zote za kiuchumi na kijamii zinazohusiana na wadau wa rasilimali za pwani.

Kwa kawaida, ripoti inajumuisha mambo yafuatayo:

***Muhtasari tekelezi*** - Ufupisho wa maelezo ya masuala, matatizo, nafasi na utatuzi uliotambuliwa wakati wa uperembaji.

***Utangulizi*** - Hujadili malengo makuu na halisi ya uperembaji wa kiuchumi na kijamii (yanayohusiana na matumizi tofauti ya taarifa za kijamii na kiuchumi kama ilivyoonyeshwa hapo juu), na pia hueleza habari za kimsingi za kibailojia, kifizikia, kijamii, kiuchumi, na kisiasa kuhusu eneo husika.

***Njia*** - Hujadili zaidi juu ya njia za kutafuta sampuli, njia za kukusanyia takwimu na njia zilizotumika kuchambua takwimu.

***Matokeo*** - Uwasilishaji wa matokeo kutokana na juhudi za uperembaji unajumuisha majedwali, michoro, kuunganisha vigezo mbalimbali pamoja na maelezo ya habari. Matokeo halisi ambayo yanaweza kuwasilishwa kwa kila kigezo yametolewa ufafanuzi katika sehemu ya uchambuzi wa kila kigezo katika *Kiambatanisho A*, na katika karatasi za uchambuzi katika *Kiambatanisho D* na *E.*

***Majadiliano*** - Mazungumzo juu ya mafunzo muhimu na maana yake halisi kutoka kwa matokeo yaliyolenga malengo ya awali ya uperembaji.

***Mapendekezo*** - Hatua zilizopendekezwa za usimamizi na hatua za utatuzi zinazoweza kuchukuliwa kwa ajili ya uperembaji.

## 5.3 KUREKEBISHA USIMAMIZI

Lengo la mwisho kabisa la kufanya uperembaji wa kiuchumi na kijamii ni kutoa habari zitakazo rekebisha na kuboresha usimamizi wa rasilimali za pwani, na kuboresha maisha ya watu binafsi na watu wa kaya ambao hutumia na kutegemea rasilimali za pwani. Matokeo ya uperembaji wa kiuchumi na kijamii yanaweza kutumika kurekebisha usimamizi, mchakato unaosisitiza kujifunza kwa kufanya na kutoa maoni, na umefungamana na mkusanyiko wa kuendelea wa habari na ujuzi wa wasimamizi. Mabadiliko ya usimamizi ni kutumia habari za kiuchumi na kijamii kukagua matokeo ya hatua za usimamizi zilizochukuliwa siku za nyuma na kutathmini kama hatua hizi zimeleta matokeo yaliyokusudiwa. Kwa misingi ya tathmini hizi, marekebisho yanayostahili yanafanywa katika mpango wa usimamizi ili kuboresha jinsi usimamizi utakavyofanywa siku za mbeleni. Kwa maelezo zaidi, tazama sehemu ya *Umuhimu wa habari hizi kwa wasimamizi na wadau wengine* ndani ya maelezo ya kila kigezo katika *Kiambatanisho A*

## 5.4 JEDWALI LA MUHTASARI WA MAWASILIANO NA MABADILIKO YA USIMAMIZI

Kama ilivyojadiliwa mwanzo, hatua mojawapo muhimu katika uperembaji ni kutambua hadhira lengwa ya matokeo ya uperembaji na njia zinazofaa za kuwasilisha habari ili kuwezesha usimamizi kubadilika kulengana na mabadiliko ya kiuchumi na kijamii. Jedwali hili ni muhtasari wa hoja ambazo zimejadiliwa pia katika sehemu zilizopita na zinaongezea hatua nyingine mbele kuhakikisha kuwa zinafaa zaidi.

Jedwali lifuatalo linaelezea kwa ufupi mambo ya kufikiriwa na timu ya uperembaji ili kuhakikisha matumizi bora ya matokeo ya uperembaji kwa kuleta mabadiliko ya usimamizi. Jedwali hili litasaidia timu ya uperembaji kupanga njia ya kuwasilisha matokeo ya uperembaji.

### JEDWALI 5.1 MUONGOZO WA UWASILISHAJI NA UREKEBISHAJI USIMAMIZI.

| Ni nani anayetakiwa kujulishwa matokeo ya uperembaji pamoja na maana yake halisi kwa kupanga, usimamizi, sera? | Kipi kinacho hitaji mabadiliko na kipi kisicho hitaji? | Ni njia ipi bora ya mawasiliano ya kutumia? | Je, inapatikana tayari? | Rasilimali au vifaa vinavyohitajika? |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |

1. Timu ya uperembaji inatakiwa kutambua wadau wanaotakiwa kujulishwa juu ya matokeo (mraba huu utajumuisha hadhira lengwa (tazama sehemu 3.9) pamoja na wadau wengine ambao niwajumuishwe kulengana na matokeo. Kwa mfano, kama katika kipindi cha uchunguzi imebainika kwamba baadhi ya bidhaa (mfano makombe) zinasafirishwa kwenda nje, itakuwa vyema kuwasilisha matokeo kwa watu hao "wanaosafirisha nje" ili kuwahusisha katika mchakato wa usimamizi wa pwani. Hii ilibainika kuwa muhimu katika Ghuba la Mnazi (Tanzania) ambapo wasafirishaji wanaushawishi mkubwa wa aina za rasilimali zinazosafirishwa nje. Wadau wanaotakiwa kujulishwa ni pamoja na watengezaji sera, wasimamizi pamoja na watumiaji.

2. Hatua ya pili ni kuandika kwa kifupi na uwazi, matokeo ya uperembaji wa kiuchumi na kijamii yanamaanisha nini kwa wadau waliotambuliwa. Swali ni kwamba ni nini kinatakiwa kubadilishwa au kipi hakihitaji mabadiliko ili kufikia malengo ya usimamizi wa rasilimali za pwani na baharini. Mabadiliko hufungamana na wadau waliotambuliwa. Kwa mfano, kama uperembaji unaonyesha kuna mahitaji makubwa ya majongoo machanga ya baharini yanayoendelea kusafirishwa nje na hakuna sheria ambayo inazuia uvunaji wa majongoo hayo, basi sheria inaweza kutungwa ili isimamie shughuli hiyo, wavuvi wa majongoo bahari, wanunuzi na wasafirishaji lazima wafahamishwe, na wahamasishwe juu ya madhara au matokeo ya shughuli za kuvua majongoo ili wabadilishe tabia na mwenendo wao. Wasimamizi pamoja na watungasera nao pia wanaweza kufahamishwa.

3. Timu ya uperembaji inatakiwa itambue njia ya mawasiliano ambayo itatumia kuwasilisha matokeo pamoja na maana halisi ya matokeo hayo kwa usimamizi kwa kila aina ya wadau lengwa, aidha kama njia hiyo ya mawasiliano tayari ipo au kama inahitaji kutengenezwa. Kwa mfano, kama njia nzuri ya kuwasilisha matokeo ya uperembaji kwa sekta ya utalii ni kwa taarifa za barua, inatakiwa ijulikane kama njia hii ipo na imefanikiwa. Kama ndivyo, matokeo ya uperembaji yanaweza kuchapishwa kwenye majarida yaliyopo. Vilevile pia vyombo vilivyopo vya habari pamoja na mitandao vinavyolenga hadhira iliyokusudiwa vinaweza kutumiwa pia. Kwa mfano, uperembaji wa kiuchumi na kijamii (SocMon-WIO), itatumia mtandoa wa WIOMSA (Western Indian Ocean Marine Science Association) kama jukwaa kwa mawasiliano na maeneo mengine yanayofanya uperembaji na kueneza habari katika ngazi ya kanda.

4. Mwisho kabisa, katika hatua za kwanza za uperembaji, itakuwa vyema kupanga bajeti kwa mahitaji ya kuwasilisha matokeo ya uperembaji kwa wadau waliotambuliwa.

*Sehemu 4* ilitoa orodha ya vigezo vya uperembaji. Kiambatanisho hiki kinafafanua kila kitu unachohitaji kujua juu ya kila kigezo, ikijumuisha;

**Ni nini** - hii inaelezea kwa undani juu ya kigezo hicho

**Jinsi ya kukusanya takwimu** - Hii hufafanua jinsi ya kukusanya takwimu (kwa mfano, aina ya watoa habari maalum, na takwimu kutoka kwa vyanzo pili) na maswali muafaka ya mahojiano ambayo yamekusanywa yote katika *Kiambatanisho B* na *Kiambatanisho C*. Mara nyengine, *ukusanyaji wa takwimu za ziada* umetolewa kupendekeza uwezekano wa ukusanyaji wa habari nyengine muhimu.

**Jinsi ya kuchambua takwimu** - maelezo ya nini la kufanya na hizo takwimu, ikiwa ni pamoja na kufanya ulinganisho na takwimu nyengine na kuyafanya majedwali au kutayarisha vifungu vya maneno, yote haya yamekusanywa katika *Kiambatanisho D* na *Kiambatanisho E*. Katika vigezo vingi, *Uchambuzi wa ziada* umetolewa kuonyesha uchambuzi unaoweza kufanywa kupita ule ulioelezewa katika karatasi za uchambuzi, *Kiambatanisho D & E* .

*Kiambatanisho hiki kinaelezea mkusanyiko wa vigezo vyote vinavyoweza kuperembwa. Kutokana na mkusanyiko huu, timu ya uperembaji inatakikana kuchagua vigezo muafaka kulengana na malengo yao na hali ya eneo kama ilivyojadiliwa katika Sehemu 4.*



**Umuhimu wa habari hizi kwa wasimamizi na wadau wengine** - inatoa maelezo ya jinsi habari hii inaweza kuwa ya manufaa tukilenganisha na malemgo yaliyoangaziwa katika sehemu iliyopita, *Sehemu 2.*

*Kiambatanisho B* na *Kiambatanisho C* vinajumuisha maswali yaliyoonyeshwa kwa kila kigezo katika sehemu zifuatazo. *Kiambatanisho D* na *Kiambatanisho E* vinajumuisha majedwali ya uchambuzi wa takwimu ya kupigia hesabu zinazoelezwa katika sehemu zifuatazo.



Vigezo vimepangwa katika vipengele 8 (yaani, eneo la uchunguzi, wadau, idadi ya watu (demografia), afya, miundombinu na biashara, shughuli za baharini, utawala, mitazamo na ufahamu, hali za kiuchumi na kijamii). Kwa vigezo vyengine (kwa mfano: umri, jinsia, elimu, uwezo wa kisoma na kuandka, dini, ukabila) njia nyengine mbadala za kukusanya takwimu zinapendekezwa. Njia mbili za msingi za ukusanyaji wa takwimu ni:

- (K) Vyanzo pili, kuwahoji watoa habari wakuu, pamoja na kuhoji makundi maalum ya wahojiwa kwa habari katika ngazi ya kaya, na
- (S) Uchunguzi, kwa habari za ngazi ya kaya au watu binafsi.

Sehemu za ukusanyaji na uchambuzi wa takwimu kwa hizo njia mbalimbali za kukusanya takwimu zimeelezewa katika maboksi zikionyesha kwa uwazi zinahusiana na ngazi gani ya habari. Rejelea *Jedwali 4.1* katika *Sehemu 4* kwa orodha ya vigezo vyote.

## KI. Eneo la uchunguzi

**Ni nini**
Eneo la uchunguzi ni ile sehemu ya rasilimali za pwani na baharini pamoja na wadau ambapo uchunguzi unafanyika. Mipaka ya eneo la uchunguzi hutegemea sehemu rasilimali zilipo pamoja na eneo wadau wanapoishi na kufanya kazi zao. Kwa hiyo eneo la uchunguzi mara nyingi linajumuisha eneo la pwani na maeneo ya maji yaliyopakana.
Wadau wanaweza wakawa wanahamahama au waliosambaa katika eneo kubwa kuliko eneo linalosimamiwa. Kunaweza kuwepo jamii moja au jamii tofauti tofauti katika eneo la uchunguzi ambao wanajumuisha wadau wote muhimu. (Angalia mwongozo wa GCRMN Sura I: Shughuli za maandalizi, kutambua eneo la uchunguzi na mahali maalum pa uchunguzi kwa maelezo zaidi.

**Jinsi ya kukusanya takwimu**
Habari juu ya eneo la uchunguzi mara nyingi hupatikana kwenye ramani ya eneo hilo na huweza pia kupatikana kwa kuwahoji watu maalum kama vile viongozi wa jamii. Kama iliyokwisha onyeshwa kwenye Chanzo pili/mwongozo wa usaili,
ni muhimu kujibu swali: Ni ipi mipaka ya eneo la uchunguzi? Eneo linalotakiwa lionyeshwe kwenye ramani.

*Ukusanyaji wa takwimu za ziada:* Ni muhimu pia kutumia alama na rangi kutambulisha mahali na pwani pamoja na rasilimali muhimu za bahari husussan katika jamii (kwa mfano:soko la samaki, kituo cha jamii).

**Angalia:** Jamii inaweza kutopenda kuweka ramani ya eneo kwa mara ya kwanza. Hii ni kwa sababu wanaweza wakahofia kuwa kutokana na ramani hiyo kunaweza kuanzishwa eneo Tengefu litakalowakataza kufika kwenye rasilimali wanazotegemeakwa maisha yao.
Ili kupata imani ya wananchi ni muhimu kueleza au kufafanua kikamilifu maana ya uperembaji wa kiuchumi na kijamii na utakavyo kuwa na faida kwao.

**Jinsi ya kuchambua takwimu**
Fanya muhtasari wa taarifa toka kwa wahojiwa maalum, na ramani mbalimbali katika ramani moja, ambayo itatumika wakati wote wa uperembaji na kuwasilishwa pamoja na matokeo. Mipaka ya eneo la uchunguzi, inayohusu eneo la pwani na rasilimali za bahari na wanakoishi wadau, ni lazima ionyeshwe kwenye ramani. Sehemu ambazo ni muhimu zinaweza pia kuzingatiwa.
Ni muhimu ikiwezekana kuwahusisha washirika wanaoweza kutoa taarifa za mifumo ya kijiografia za ki-ramani. Matokeo ya ramani yanahitaji yaunganishwe na usaili/karatasi ya uchambuzi wa chanzo pili.

**Umuhimu wa habari hizi kwa wasimamizi na wadau wengine**
Utambuzi mahususi wa eneo la uchunguzi ni muhimu kwa kutambua namna ya matumizi na shida au vitisho vinavyoweza kutokea katika rasilimali. Kwa kuonyesha maeneo ndani ya ramani, wasimamizi wanaweza kuona vitu vya ki-jiografia ambavyo vinaonyeshwa katika eneo, kama vile maeneo yenye maji, maeneo ya kilimo au msongamano mkubwa wa maendeleo ya makazi.

Kutokana na mtazamo wa mpango wa uperembaji wa kiuchumin a kijamii, ni muhimu zaidi kuainisha eneo la mafunzo kwa vile hili ndilo eneo mahususi uperembaji utakapofanyika mara kwa mara.
Ili kuwezesha ulinganifu kufanyika, timu ya uperembaji lazima ielewe jamii iliyomo ndani ya eneo la uchunguzi.

Kuweka ramani ya eneo ni hatua ya maana katika kujenga uhusiano baina ya wasimamizi na jamii. Ramani itakuwa muhimu kwa watumiaji wa rasilimali.

WADAU

## K2. Wadau

**Ni nini**
Wadau ni mtu mmoja, kundi la watu, mashirika ya watu wanaofaidika, wanaohusika au wanaoathiriwa (hasi au chanya) na usimamizi wa rasilimali za pwani. Wadau hawa wanaweza au wasiweze kuwa ni wakazi wa karibu na mahali hapo lakini ni watu wanaofaidika au wenye ushawishi katika usimamizi wa rasilimali za pwani. (Angalia Mwongozo wa GCRMN Sura ya 1: Shughuli za maandalizi, kutambua wadau wa mwambani kwa maelezo zaidi. Hawa ndio kiini cha shughuli zote za usimamizi kwani tabia zao lazima zijionyeshe ili kuboresha usimamizi wa rasilimali za pwani.

**Jinsi ya kukusanya takwimu**
Watoa habari maalum (kwa mfano, viongozi wa serikali, viongozi wa kuchaguliwa, wavuvi, viongozi wa wafanya biashara, wachuuzi wa samaki) katika eneo wanahojiwa ili kutambua makundi matatu makuu ya wadau kwa kila shughuli ya pwani (kwa mfano: uvuvi, ufugaji viumbe baharini, utalii). Shughuli za pwani zinatambuliwa kama sehemu ya shughuli mbalimbali (K18) na kuonyeshwa katika chanzo cha pili/ jedwali la mwongozo wa uhojaji kama iliovyofafanuliwa.

*Ukusanyaji wa takwimu za ziada:* Ili kufahamu miundo ya ki-uwezo, (kisiasa, kiuchumi na kijamii) katika jumuia, watoa habari wakuu wanaweza kuulizwa ni kiasi gani makundi ya wadau mbalimbali yanavyoathiriana.

**Jinsi ya kuchambua takwimu**
Fanya muhtasari wa takwimu zote kutoka kwa watoa habari wakuu katika jedwali ndani ya karatasi ya mahojiano/chanzo pili kama inavyoonyeshwa:-

| Shughuli ya pwani* | Kundi la wadau 1 | Kundi la wadau 2 | Kundi la wadau 3 |
|---|---|---|---|
| Uvuvi | Wavuvi katika bandari ya Mashariki. | Wavuvi katika bandari ya Magharibi. | Wavuvi katika bandari ya Kaskazini |
| Ufugaji wa viumbe baharini | Wamiliki wa ufugaji viumbe, wasimamizi na watumishi | | |
| Utalii | Wamiliki wa hoteli wasimamizi na watumishi | Waendeshaji michezo ya majini | Watalii |
| *Tengeneza orodha kulingana na shughuli kama zilivyotambuliwa katika Shughuli (KI8) | | | |

*Uchambuzi wa ziadi:* Aya fupi inaweza kuandikwa ili kutambua makundi ya wadau wanaohusika katika kila mojawapo ya shughuli za pwani.

**Umuhimu wa habari hizi kwa wasimamizi na wadau wengine**
Wasimamizi wa rasilimali za pwani wamekuja kutambua kuwa ushirikishaji kikamilifu wa wadau wa rasilimali za pwani katika kupanga na kutekeleza kunaweza kuboresha mafanikio ya ulinzi wa rasilimali hizo.
Endapo wenyeji wanahusishwa katika usimamizi wa rasilimali za pwani na kuziona kama ni zao, kuna uwezekano mkubwa wao kuunga mkono usimamizi wa rasilimali hizi. Kuwaelewa wadau kutafanya msimamizi kuwatambua vizuri zaidi mtu mmoja mmoja ambaye atakuwa ameguswa na hatua za ulinzi na kuoanisha mguso huo wa wadau.Wadau pia hutambuliwa ili kufahamu ni akina nani wawe muhimu zaidi katika kuwasaidia viongozi. Kuwasaidia viongozi kuwatambua wadau wote itatoa nafasi kwa wadau kuhakikisha kwamba makundi yote ya watumiaji wa rasilimali wanajumuishwa katika shughuli za usimamizi na wananufaika na mipango mahususi kwa mahitaji yao.

## *K3. Majukumu na wajibu wa kijinsia*

**Ni nini**
Majukumu na wajibu wa jinsia ni kiashiria cha mgawanyo wa shughuli na wajibu kulingana na jinsia katika eneo la uchunguzi.

**Jinsi ya kukusanya takwimu**
Habari halisi hukusanywa kutoka kwa makundi maalumu ya wahojiwa (kwa kuzingatia jinsia). Makundi ya wahojiwa huulizwa kujadili kalenda za kila siku (moja kwa wanaume na moja kwa wanawake).

Katika ukanda huu wetu, misimu ni muhimu, hivyo kalenda zitajumuisha misimu ya asili. Shughuli zisizofanywa na jinsia moja, na sababu zake lazima zijadiliwe.

Watoa habari wanaombwa waorodheshe shughuli zinazofanywa katika ngazi ya kaya,na shughuli zinazowaingizia pato la chakula na pesa.

Kwa kila shughuli, watoa habari wanaulizwa ni akina nani (jinsia gani, umri) wanaofanya hiyo shughuli, ni nani (umri, jinsia) wanafanya maamuzi gani katika ngazi ya kaya (kwa mfano: matumizi ya wakati, matumizi ya pato la pesa, wapi lini na jinsi gani shughuli ifanywe) na ni nani anafanya maamuzi juu ya shughuli za pwani na baharini.

Watoa habari pia wanaulizwa:
Ni shughuli zipi katika ngazi ya kaya Wanaume/Wanawake hawaruhusiwi kufanya.
Kwa nini?............................

Ni shughuli zipi za pwani na baharini Wanaume/Wanawake hawaruhusiwi kufanya?
Kwa nini?............................

**Jinsi ya kuchambua takwimu**
Fanya muhtasari wa habari kutoka kwa watoa habari wakuu na makundi tofauti ya wahojiwa maalumu katika jedwali la mahojiano/karatasi ya uchambuzi chanzo pili.

Shughuli zinaorodheshwa pamoja na jinsia na umri wa wanaozifanya. Orodha ya sababu za kwa nini wanaume na wanawake hawaruhusiwi kufanya baadhi ya shughuli ni lazima itengenezwe na kuandikwa ndani ya karatasi ya uchambuzi katika jedwali la mahojiano/chanzo cha pili kama inavyoonyeshwa katika mfano huo hapo chini. Maelezo mafupi yanaweza kutolewa kwa kila sababu inayotambuliwa.

| Shughuli | Jinsia na umri* | | Kwa nini baadhi ya shughuli hufanywa na jinsia moja? | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Kaya** | **Wanawake** | **Wanaume** | **Sheria** | **Utamaduni** | **Hali** | **Elimu** | **Dini** | **Uchumi** | **Nyenginezo** |
| Uchotaji maji | Wote | | | | | | | | |
| Kutafuta kuni | Wote | | | | | | | | |
| Ulezi wa watoto | Mtoto | | | | | | | | |
| Upishi | | Watu wazima | | | | | | | |
| ***Kipato cha kula/pesa*** | | | | | | | | | |
| Walioajiriwa hotelini | | Watu wazima | | | | | X | | |
| Wanaoongoza uvuvi | | Watu wazima | | | | | | | |
| Biashara ya samaki | Wakubwa | Watu wazima | | | X | | | | |
| Uokotaji makome | Wote | | | | | | | | |

**Mpangilio wa umri: watoto, watu wazima na wakubwa.*

Ushiriki katika kutoa maamuzi: kaya na shughuli za pwani na baharini.

| Kaya | Wanawake pekee | Wanaume pekee | Mara nyingi wanawake | Mara nyingi wanaume | Wote |
|---|---|---|---|---|---|
| Muda wa kutumia | | | | X | |
| Matumizi ya wakati | | | | | X |
| Akiba/uwekezaji | X | X | | | |
| Elimu | | | X | | |
| Afya | | | | X | |
| **Shughuli za pwani na baharini - shughuli za kutoa** | | | | | |
| Mahali | | Wakubwa | | | |
| Njia/Mbinu | | | | | |
| Muda | | | | | |
| Vikwazo | | Wakubwa | | | |
| **Shughuli za pwani na baharini - shughuli zisizokuwa za kotoa** | | | | | |
| Mahali | | | | | |
| Njia/Mbinu | | | | X | |
| Muda | | | X | | |
| Vikwazo | | Wakubwa | | | |

*Uchambuzi wa ziada:* Linganisha majukumu na wajibu kwa miaka. Pia uilinganishe na njia (K 20 na K14) viwango na aina za athari (K25) angalia kwa makini habari za wadau (K2) na kazi zao (K7 na S1) ambapo majukumu ya jinsia katika shughuli za pwani na baharini ni muhimu ziingizwe.

**Umuhimu wa habari hizi kwa wasimamizi na wadau wengine**

Kuelewa mgawanyo wa shughuli na wajibu kulingana na jinsia na/umri itasaidia wasimamizi kulenga makundi ya kuendeleza mipango ya uhamasishaji katika matumizi ya rasilimali.Vivyo hivyo itawasaidia kulenga shughuli zao kwa makundi ambayo yanaweza kuathiriwa zaidi na sheria na kanuni zinazotumika.
Kwa mfano kuzuia wavuvi wa juya nchini Kenya kunaathiri siyo wavuvi pekee bali hata wanawake waliojikita katika biashara ya samaki wachanga.

Itawezesha viongozi kuchukua hatua sahihi kuhakikisha kuwa ushirikishaji katika usimamizi na maamuzi unahusisha sehemu kubwa ya watu wenye wajibu kwa shughuli mbalimbali zitakazosimamiwa.

Hatimaye itasaidia viongozi kuelewa jinsi ya kuwafikia wadau (wale wanaofanya shughuli na wanaotoa maamuzi endapo ni tofauti) ili kusaidia kubadilisha mitazamo na tabia zao. Kwa mfano, kama wanaume wakubwa ndio wenye majukumu ya kutoa maamuzi ya wapi wanawake wakaokote makome, basi wasimamizi wanawajibika kuwaendea wanaume na wanawake wakubwa ili kurekabisha uokotaji wa makome.

Kufanya uperembaji wa wajibu na majukumu ya jinsia itasaidia wananchi kuelewa vizuri zaidi muundo wa jamii yao. Inaweza pia kusaidia makundi mbalimbali kutambua jinsi mgawanyo wa kazi unavyokuwa.

## IDADI YA WATU

## NGAZI YA KIJAMII: K4-K14

### *K4 & K5. Idadi ya Watu na Kaya*

**Ni nini**

Idadi ya watu ni jumla ya watu waishio katika eneo la uchunguzi. Idadi ya kaya ni idadi ya vitu vilivyoelezewa kama kaya katika mwanzo wa mchakato wa uperembaji (kwa mfano: watu wanaochangia chakula na kipato cha pesa) katika eneo la uchunguzi, bila kuangalia idadi ya jamaa wanaoishi katika nyumba.

**Jinsi ya kukusanya takwimu**

Takwimu za idadi ya watu na idadi ya kaya kwa kawaida hupatikana kutoka katika vituo vya hesabu za watu za taifa, mkoa, na au vituo vya takwimu vya mitaa, ambayo huweza kupatikana kutoka ofisi za serikali za mitaa au Halmashauri za miji. Ni muhimu kuzitazama takwimu hizi na watoa habari muhimu kama vile kiongozi wa jamii. Kama ilivyochukuliwa kutoka chanzo cha pili /mwongozo wa mahojiano, maswali ya msingi ya kuulizwa ni:

Watu wangapi wanaishi katika eneo la uchunguzi? ------------

Kaya ngapi zinapatikana katika eneo la uchunguzi? -----------

*Ukusanyaji wa takwimu za ziada:* Itakuwa ni vizuri pia kuuliza kuhusu mabadiliko katika idadi ya watu kwa kipindi chote cha mwaka na sababu ya mabadiliko hayo.

**Jinsi ya kuchambua takwimu**

Tumia takwimu kutoka katika vyanzo vya pili na watoa habari maalum kukadiria idadi ya watu na idadi ya kaya na zinukuliwe katika karatasi ya mahojiano/uchambuzi wa vyanzo pili.

*Uchambuzi wa ziada:* Toa matokeo kutoka miaka ya nyuma ili kutafuta mabadiliko kwa muda. Linganisha mabadiliko ya idadi ya watu na idadi ya kaya kwa muda na mabadiliko katika hali ya rasilimali na takwimu kutoka kiwango na aina ya athari (K25) kuangalia kama mabadiliko ya idadi ya watu yanalingana na hali ya athari.

**Umuhimu wa habari hizi kwa viongozi na wadau wengine**

Kufahamu viwango vya idadi ya watu katika eneo la uchunguzi na idadi ya kaya ni muhimu ili kujua tisho linalokabili raslimali. Viwango vya idadi ya watu vinaonyesha kwa jumla kiwango cha shinikizo juu ya rasilimali. Watu wengi katika eneo kwa ujumla wanapelekea

mshinikizo mkubwa katika rasilimali. Taarifa juu ya mabadiliko kulingana na muda zinaweza kutumika katika kuona kama mshinikizo huu unaongezeka, unapungua, au umebaki vile vile. Ulinganifu wa hali ya rasilimali na kiwango cha matumizi unasaidia kuona ni kwa kiasi gani ongezeko la watu linaathiri hali ya rasilimali.

Kutokana na mtazamo wa programu ya uperembaji wa masuala ya kiuchumi na kijamii, watu na idadi ya kaya ni muhimu katika kutambua sampuli za kaya kwa mahojiano. Hivyo ni muhimu kukusanya taarifa hizi kutoka kwa watoa habari wakuu kabla ya kuanza kwa uchunguzi.

## *K6. Kiwango cha Uhamiaji*

**Ni nini**

Kiwango cha uhamiaji kinahusu badiliko la asilimia katika idadi ya watu kwa sababu ya watu kuingia au kutoka katika eneo la uchunguzi katika mwaka uliopita.

**Jinsi ya kukusanya takwimu**

Takwimu za uhamiaji mara nyingi zinapatikana kutoka katika ngazi ya taifa, mkoa, na/au vituo vya takwimu za watu vya mitaa ambazo zinaweza kupatikana kutoka ofisi za serikali za mitaa na halmashauri za miji. Ni muhimu kuziangalia upya hizi takwimu pamoja na watoaji habari wakuu, kama vile viongozi wa jamii. Kama ilivyoandikwa katika chanzo pili/mwongozo wa mahojiano, maswali ya msingi ya kuyashughulikia hapa ni:

Ni idadi gani ya ongezeko au upungufu wa watu walioingia au kutoka katika eneo la uchunguzi katika mwaka uliopita?….. (andika alama + au - kuonyesha kuingia au kutoka)

**Jinsi ya kuchambua takwimu**

Tumia takwimu kutoka chanzo pili na watoaji habari maalum kuyakinisha kiwango cha uhamiaji na andika katika karatasi ya mahojiano/uchambuzi wa vyanzo pili. Kwa mfano: endapo kulikuwa na watu 1000 katika jamii mwaka 1999 na watu 500 waliingia katika eneo la uchunguzi mwaka 2000, kwa hivyo kiwango cha uhamiaji kitakuwa 500/1000 = 50%.

*Uchambuzi wa ziada:* Toa jawabu kutoka miaka iliyopita kupiga hesabu mabadiliko kwa muda fulani. Linganisha mabadiliko katika kiwango cha uhamiaji kwa kipindi fulani na mabadiliko katika hali ya rasilimali na kiwango na aina ya athari (K25) kuona endapo kiwango cha uhamiaji kina uhusiano na hali na athari zilizotokea.

**Umuhimu wa habari hizi kwa viongozi na wadau wengine**

Viwango vya uhamiaji pia ni muhimu kwa kufahamu athari. Jinsi watu wanavyoingia katika eneo ndivyo msongo katika rasilimali unavyoongezeka. Ulinganisho na hali ya rasilimali pamoja na kiwango cha athari ni muhimu mahsusi kwa kuona endapo wageni wanahusiana na mabadiliko katika hali ya rasilimali na athari zake.

Viwango vya uhamiaji pia ni muhimu kwa maingiliano na wadau, hususan kwa kuendeleza mipango ya ufahamu katika ongezeko la rasilimali. Wahamiaji wanaweza wakatazamiwa kuwa na uelewa mdogo wa rasilimali za pwani na mipango ya usimamizi kuliko wakazi wa muda mrefu. Mpango wa usimamizi wa rasilimali za pwani pamoja na kiwango kikubwa cha wahamiaji katika jamii unaweza kuhitaji kuanzisha mipango ambayo inaendana na hali hiyo ya idadi ya watu inayoongezeka yenye kiwango kidogo cha ufahamu na ukubalifu wa mazingira. Kwa mfano, msimamizi anaweza akahitaji mikutano ya jamii ya watumiaji rasilimali ambao ni wenyeji na wahamiaji ili kuwatambulisha wageni katika utaratibu uliopo. Zaidi ya hayo, endapo msimamizi anafahamu shughuli gani wahamiaji wanafanya, anaweza akapanga mipango inayolenga shughuli hizo. Kwa mfano, kama kuna idadi kubwa ya wenye hoteli wageni wanaoingia na kukata mikoko na wenye ufahamu haba wa ikolojia ya mwambao, basi meneja atahitaji kuanzisha elimu ya video juu ya umuhimu wa rasilimali za pwani kama vivutio vya utalii na athari ya shughuli za hoteli katika rasilimali hizi muhimu.

## *K7. Ajira*

**Ni nini**

Ajira ni shughuli ambayo ineleta uchumi au riziki kama vile kipato cha pesa, chakula au njia nyinginezo za kujikimu. Ajira ya msingi ni ile shughuli kuu ya uchumi, ambapo ajira ya pili au nyengineyo itakuwa shughuli ya pili na ya tatu muhimu za kuleta uchumi au riziki.

**Jinsi ya kukusanya takwimu**

Takwimu juu ya ajira zinaweza kupatikana kupitia vyanzo vya pili, kama vile takwimu za idadi za watu (sensa), habari za uvuvi na mipango ya maendeleo ya jamii. Hata hivyo, takwimu hizi huenda zisitolewe kwa kiwango cha ajira ambacho kitamsaidia msimamizi.

Kwa mfano, "utalii" unaweza kuandikwa kama ni ajira, lakini bado msimamizi atahitaji kujua asilimia ya wahudumu au wanaoshughulika na michezo ya majini mbali na wale wa hotelini. Ni muhimu kwahivyo kuwahoji watoa habari wakuu, kama vile viongozi wa jamii. Habari hii inatakiwa iingizwe katika jedwali la chanzo pili /mwongozo wa mahojiano kama ilivyofafanuliwa hapa chini.

*Ukusanyaji wa takwimu za ziada:*
Timu inaweza kuuliza kuwepo kwa shughuli haramu kama vile uvuvi haramu na madawa ya kulevya. Kwa vile ni vigumu kupata taarifa hii kutoka kwa wanaochunguzwa, ni muhimu sana kupata taarifa hizi toka kwa watoa habari wakuu. Kuangalia pia kunaweza kutoa taarifa za shughuli haramu zinazofanyika katika eneo la uchunguzi.

Timu inaweza pia kuhitaji kujua kiwango cha ukosefu wa ajira au kutoajiriwa kikamilifu. Kiwango kikubwa cha ukosefu wa ajira kinaweza kuashiria msongo mkubwa wa rasilimali.

**Jinsi ya kuchambua takwimu**
Kwa kutumia takwimu toka chanzo pili na watoa habari wakuu, yakinisha asilimia ya wafanyao kazi katika kila aina ya kazi, na nambari ya watu ambao hujihusisha na kazi hiyo kama kazi zao za msingi. Andika taarifa hii katika karatasi ya mahojiano/uchambuzi wa vyanzo pili kama mfano ufuatao.

| Kazi kuu katika jamii | Asilimia ya watu wanaofanya kazi hiyo kama kazi yao ya msingi | Idadi ya watu wanaofanya kazi hiyo kama kazi yao ya msingi | Asilimia ya watu katika jamii wanaofanya kazi hiyo kama kazi yao ya pili. | Asilimia ya watu wanaofanya kazi hiyo kama kazi yao ya tatu |
|---|---|---|---|---|
| 1. Wavuvi | 60% | 600 | 20% | 10% |
| 2. Wanaoendesha michezo ya majini | 10% | 100 | 0% | 0% |
| 3. Wakuza viumbe baharini | 20% | 200 | 5% | 1% |
| 4. Wafanyakazi mahotelini | 5% | 50 | 0% | 0% |
| 5. Wakulima | 5% | 50 | 10% | 4% |

*Uchambuzi wa ziada:* Toa matokea kutoka miaka ya nyuma ili kutafuta mabadiliko kwa kipindi fulani. Linganisha matokeo haya na mabadiliko ya hali ya rasilimali. Mbinu (K16), viwango na aina ya athari (mguso) (K25) na tisho linalofikiriwa (S20) kuona kama kuna uhusiano. Inaweza ikawa vizuri pia kutoa maelezo mafupi ya kazi kuu, umuhimu wake kwa kuangalia asilimia na idadi ya watu wanaofanya kila moja ya kazi hizo na mabadiliko kwa kipindi fulani.

Asilimia ya kazi za msingi na kazi za pili zinaweza kuunganishwa zikawa kiashiria cha utegemezi kwa kila shughuli. Katika mfano huu asilimia 80 ya watu wanaofanya kazi wanategemea uvuvi wakati ambapo asilimia 10 huchukuwa uvuvi kama kazi yao ya tatu.

Takwimu kama hizo hukusanywa kama sehemu ya uchunguzi. Ulinganifu baina ya matokeo huleta usahihi wa takwimu.
Kama kuna tofauti kubwa kati ya matokeo kuna haja ya kufanya sensa ya uchunguzi. Ona ya kwamba uchunguzi wa takwimu hufanywa kwa idadi nzima ya watu (siyo tu idadi ya wafanyao kazi), ambayo inajumuisha hata wale ambao hawajaajiriwa. Ili kulinganisha kwa usahihi, asilimia za uchunguzi lazima zifanyiwe hesabu tena kwa kuzingatia watu walioorodheshwa kama wafanyakazi pekee (yaani siyo watu ambao walioandika "mwanafunzi" ,"sina ajira", n.k. kama kazi zao.

**Umuhimu wa habari hizi kwa wasimamizi na wadau wengine**
Shughuli nyingi zinatishia rasilimali. Mabadiliko ya muda na mlingano wa viwango na aina za athari (K25) na hali ya rasilimali inaweza kutupa ufahamu mwingi juu ya athari. Kwa mfano, iwapo idadi kubwa ya watu wanajiingiza kwenye shughuli ya uvuvi kama kazi yao ya msingi katika kipindi fulani, basi uvuvi wa kupindukia ndilo jambo la kutia shaka. Ulinganifu na hali ya rasilimali lazima uonyeshe kupungua kwa idadi ya samaki kila idadi ya watu wanaovua inavyoongezeka. Ulinganifu na njia/mbinu (K20) na kiwango na aina za athari (K25) inaweza pia ikawa muhimu katika kuona jinsi shughuli hizo zinavyokuwa na kuongezeka. Ulinganifu na athari zinazofikiriwa (S20) ni muhimu kwa kuona jinsi jamii inavyofikiria juu ya haya maongezeko endapo yanaonekana kuathiri rasilimali. Kama idadi ya wavuvi inaongezeka, lakini hali ya rasilimali ni nzuri, aina za matumizi kwa kiasi fulani ni mema, na jamii haichukulii uvuvi kama wenye kiwango cha kati cha athari au athari kubwa, uvuvi kwahiyo hautakuwa wenye athari.

Kazi zinazofanywa na jamii pia ni muhimu kuweza kukadiria umuhimu wa rasilimali. Jinsi asilimia ya watu wanaotumia rasilimali inavyoongezeka ndivyo hivyo hivyo utegemezi katika matumizi ya rasilimali unavyoongezeka, na kwahivyo umuhimu zaidi wa rasilimali. Ongezeko katika idadi na/au asilimia ya watu wanaofanya shughuli zenye uhusiano na pwani inaashiria ongezeko la umuhimu. Mgawanyiko wa watu katika kazi tofauti tofauti pia unaashiria kiwango cha uimara wa uchumi wa jamii, ambao pia ni muhimu kwa kufahamu umuhimu wa rasilimali. Kama idadi kubwa ya watu wanategemea uvuvi, basi jamii hiyo itaathiriwa kwa kiwango kikubwa na kusambaratika kwa biashara ya samaki. Kaya nyingi katika Magharibi mwa Bahari ya Hindi wana kazi zaidi ya moja ambao ni mkakati muhimu kwa kuhakikisha upatikanaji wa kipato cha kutosha na cha mara kwa mara cha kaya.

Hatimaye, kazi zinazofanywa na jamii ni muhimu kwa kuelezea athari za mikakati ya usimamizi katika maisha ya jamii. Kwa mfano, wasimamizi wanaweza wakaona endapo kazi zitabadilika baada ya kuendesha mafunzo ya njia mbadala za kujiingizia kipato,au wanaweza kuona kama kuanzishwa kwa eneo lisiloruhusiwa kuvua kunasababisha watu kuacha uvuvi na kuingia kwenye kazi zengine.

Habari hii itakuwa muhimu kwa wadau kuelewa vizuri kiwango chao cha utegemezi katika rasilimali za pwani na baharini. Kuelewa umuhimu wa shughuli mbalimbali kutaisaidia jamii kuchangia zaidi na kwa uwakilishi mkubwa katika usimamizi na kuhakikisha kuwa maamuzi yanazingatia athari kwa watumiaji wa rasilimali na yanahusishwa na hali ya wadau.

## *K8-14. Umri, Jinsia, Ukabila, Uwezo wa kusoma na kuandika, Elimu, Dini, Lugha*

**Ni nini**

Umri, jinsia, kabila, elimu, uwezo wa kusoma na kuandika, na dini ni vigezo vya msingi vya demografia (uwiano wa watu). Elimu inapimwa kwa miaka wastani ambayo watu wenye umri zaidi ya miaka 16 katika eneo la uchunguzi walitumia katika mafunzo ya kawaida.Uwezo wa kusoma na kuandika unapimwa kwa asilimia ya watu wanaojua kusoma na kuandika katika eneo la uchunguzi. Umri unapimwa kwa asilimia ya watu katika eneo la uchunguzi wenye umri tofauti tofauti. Jinsia inapimwa kwa asilimia ya watu ambao ni wanaume na walio wanawake. Kabila na dini hupimwa kwa asilimia ya watu katika eneo la uchunguzi wenye asili za kabila tofauti na wenye kufuata dini mbalimbali.

**Jinsi ya kukusanya takwimu**

Habari ya msingi ya idadi ya watu inapatikana katika chanzo pili kama vile idara za serikali zinazoweka hesabu za watu, ofisi za mijini, na vituo vya jamii. Ni vyema kuhakikisha takwimu hizi na watoaji habari wakuu.

Ukusanyaji wa takwimu lazima ulenge kuelezea asilimia ya watu katika eneo la uchunguzi ambao wamo katika makundi tofauti-tofauti ya umri, jinsia, elimu, na dini na kabila. Kama inavyoonyeshwa ndani ya mwongozo wa chanzo kati/ mahojiano, maswali ya msingi ya kuuliza ni:

Ni asilimia ngapi ya watu katika eneo la mafunzo wamo kwa sasa katika makundi ya umri yafuatayo?

0 18-----; 19 30-------;30 31---------; 50------; zaidi ya 50 -----------

Ni asilimia ngapi ya watu ni wanaume au wanawake? Wanaume ------; Wanawake ---------

Nini wastani wa miaka ya elimu kwa watu wenye umri zaidi ya miaka 16 katika eneo la uchunguzi

Ni asilimia ngapi ya watu wanajua kusoma na kuandika?---------

Ni makabila ya watu yapi yanayopatikana katika eneo la uchunguzi (Asilimia ya kila kabila kuu katika eneo la uchunguzi?

(andikandani)------- (andikandani) -----------; (andikandani) ------

Kuna makundi yapi ya kidini katika eneo la uchunguzi? (Asilimia ya kila kundi kuu la dini katika eneo la uchunguzi?

(andikandani)------- (andikandani) -----------; (andikandani) ------

Ni lugha zipi kuu zinayozungumzwa katika eneo la uchunguzi (Asilimia ya kila lugha kuu katika eneo la uchunguzi?

(andikandani)------- (andikandani) -----------; (andikandani) ------

*Ukusanyaji wa takwimu za ziada:* Timu ya uperembaji inaweza kuhitaji kupata habari za upokeo wa wadau kuwa washirika katika siasa, katika ngazi ya jamii. Hii ni habari nyeti kabisa na inaweza kupatikana vizuri kupitia kwa watoaji habari wakuu au vyanzo pili. Upokeo wa wadau kuwa washirika katika siasa unaweza kuwazuia watu kufanyakazi pamoja. Upokeo wa wadau kuwa washirika katika siasa pia kunaweza kutoa ufahamu juu ya fikra na thamani za watu kuhusu rasilimali.

Inaweza pia kuwa sahihi katika baadhi ya maeneo kukusanya habari kuhusu ukoo. Hii inaweza kuwa na umuhimu mahali ambapo wajibu na majukumu yanaamuliwa na koo. Habari hii inaweza pia kuthibitishwa na matokeo ya wamiliki wa ardhi wasio rasmi na tamaduni (K34) na nguvu na ushawishi (K37).

**Jinsi ya kuchambua takwimu**

Tumia habari kutoka kwa vyanzo pili na watoaji habari wakuu kuonyesha asilimia ya watu katika kila kundi na kuandikwa katika karatasi ya mahojiano/uchambuzi wa vyanzo pili. Mfano wa umri ni kama ufuataao:

Asilimia ya umri katika jamii: 0-18 23%; 19-30; 41%; 31- 50; 16%; Zaidi ya 50 20%.

*Uchambuzi wa ziada*: Michoro (chati) mitatu inaweza kutayarishwa kuelezea umri na dini na maenezi ya makabila katika eneo la uchunguzi. Ondoa matokeo kutoka ya miaka iliyopita kupata hesabu ya mabadiliko katika kipindi hicho.Zaidi ya hivyo, inaweza ikawa muhimu kuelezea mchanganyiko wa watu katika eneo la uchunguzi na madiliko yaliyotokea kwa kipindi hicho.

Takwimu za namna hiyo hukusanywa kama sehemu ya uchunguzi. Ulinganisho baina ya matokeo huwezesha kuhakiki usahihi wa takwimu. Endapo zipo tofauti kati ya matokeo, itakuwa vizuri kuwasiliana na wahojiwa wakuu kuona ni wapi paliposabisha upungufu. Hatahivyo ni lazima ifanyike sensa ya uchunguzi (uchunguzi wa kaya zote, na siyo tu kuchukuwa sampuli) ili kuelewa kwa usahihi eneo la uchunguzi.

**Umuhimu wa habari hizi kwa wasimamizi na wadau wengine**

Mambo haya yote ni muhimu kwa kuendeleza ushiriki wa wadau katika usimamizi. Elimu, uwezo wa kusoma na kuandika, na umri vinaweza vikawa ni vibashiria vya ukubali wa mawazo mapya. Kwa jumla, kadri umri unavyoongezeka, uwazi wa mawazo mapya (kwa mfano, uanzishwaji wa eneo lisiloruhusiwa kuondoa/kuchukua kitu chochote) hupungua. Na kadiri kiwango cha elimu kinavyoongezeka, uwazi wa mawazo huongezeka. Kwa mfano mvuvi kijana aliye na elimu anaweza kukubali kupata mafunzo zaidi ya ujuzi mpya kuliko mvuvi asiye na elimu. Kwa kufahamu vipengele hivi, wasimamizi hupata ufahamu wa uwezekano wa uhamasishaji, uungaji mkono na kukubali hatua za usimamizi.

Ukabila na dini pia ni muhimu kwa kupata ushiriki wa wadau. Mambo yote haya ni vipengele muhimu vya muundo wa jamii na mara nyingi yanahusiana na uwanachama wa kikundi, uaminifu na vipengele vingine vya tabia za kijamii. Hali ya kuwa sawa ya jamii mara nyingi huleta ukubalifu mkubwa katika kufanyakazi pamoja. Kwa kufahamu watu wa kabila na dini fulani, wasimamizi watakuwa kwenye nafasi njema ya kuelewa tabia za wadau na jinsi ya kuingiliana nao. Jamii moja au inayofanana ina uwezekano kufanyakazi pamoja kuliko eneo lenye watu wa kabila na dini mbalimbali.
Habari hii inaweza pia kutumika kuamua jinsi ya kuingia kwenye makundi. Kwa mfano, endapo ushirikishi wa kidini ni mizito, basi huduma za kidini au mikutano ya kidini inaweza kuwa njia sahihi za kuwafikia watu na viongozi wa dini wanaweza kuwa wawakilishi sahihi wa jamii. Ukabila na dini zinaweza pia kutoa ufahamu wa watu na thamani ya rasilimali, ingawa hii inahitaji kuelewa itikadi zao za kidini na kikabila.

Kutegemea na utamaduni, jinsia inaweza pia kuwa kiashiria muhimu cha kushiriki kwa vile katika baadhi ya tamaduni wanawake hawashiriki kikamilifu katika siasa na usimamizi. Inaweza ikawa vigumu zaidi katika hali hizi kuwashirikisha katika usimamizi.

Elimu, kujua kusoma na kuandika na ushirikishi wa kabila na dini ni muhimu kwa kufahamu athari za usimamizi kwa maishilio na ustawi kwa kipindi fulani. Kuongezeka kwa viwango vya elimu vikiandamana na mikakati halisi ya usimamizi inaonyesha athari bayana. Upungufu mkubwa wa asilimia ya watu katika vikundi vya kabila fulani unaweza kuonyesha kwamba athari za mikakati ya usimamizi si sawa katika makundi hayo. Shida katika fasiri hizi ni kuoanisha mikakati ya usimamizi wakati ambapo sheria zingine na mipango mingine inasababisha haya mabadiliko.

Umri ni muhimu kwa kukisia misongo ya baadaye juu ya raslimali. Idadi ya watu ambao ni vijana, ambao ni kawaida kwa mataifa yaliyoko eneo la Magharibi mwa Bahari ya Hindi inaonyesha kutakuwa na msongo mkubwa juu ya rasilimali katika miaka ijayo.

Vilevile, kutokana na mitazamo ya shughuli ya uperembaji wa kiuchumi na kijamii, habari ya mgawanyo wa umri, jinsia, elimu, kabila, dini na kazi zinazofanywa na jamii itasaidia kuhakikisha kuwa kiasi kikubwa cha watu katika eneo la uchunguzi wanahojiwa. Kwa mfano, iwapo kuna asilimia 30 Wabaptisti, aslimia 40 Wakatoliki, na asilimia 40 Waevanjilisti, basi timu inatakiwa ihakikishe kuwa mahojiano yanafanywa kukaribia na asilimia ya kila kundi. Ni muhimu kukusanya habari hii kutoka kwa watoaji habari wakuu kabla ya kuanza uchunguzi. Angalia Sehemu 3.4 kwa maelezo juu ya kuchagua watoa habari.

## *S19. Ajira, Umri, Jinsia, Kabila, Elimu, Dini, Lugha, Ukubwa wa kaya, Muundo wa kaya*

**Ni nini**

Kuongezea kwa kazi, umri, jinsia, kabila, elimu, dini, lugha na kazi (angalia "Ni nini" K7-14) timu ya uperembaji itaweza kuchunguza ukubwa na muundo wa kaya katika kiwango cha kaya. Ukubwa wa kaya unaashiria wastani wa ukubwa wa kaya katika eneo la uchunguzi. Muundo wa kaya unahusu endapo kaya inaongozwa na mwanaume au mwanamke (Mjane au la) Muundo wa kaya pia unahusu wastani wa idadi ya wanaume, wanawake na watoto wanaotengeza kaya

*Ukusanyaji wa takwimu za ziada:* Katika ngazi ya kaya, timu ya uperembaji ingetaka kuuliza kwa undani zaidi juu ya lugha ya kigeni inayozungumzwa na wakazi wa kaya. Hii inaweza kutoa habari za endapo wenyeji wa jamii hiyo wako katika hali nzuri ya kupata nafasi zinazotolewa na sekta ya utalii inayojitokeza au iliyopo.

Timu pia ingetaka kuuliza kuhusu kuwepo kwa kazi haramu/zisizo halali, kama vile uwindaji wa samaki na madawa ya kulevya. Ni lazima ifahamike kwamba hili linaweza kuwa jambo nyeti kabisa na, kwahivyo ni rahisi zaidi kupata habari zaidi kutoka kwa wahojiwa wakuu. (Angalia K7)

**Jinsi ya kukusanya takwimu**

Habari juu ya vigezo hivi vyote vinavyohusiana na watu (S1-9) inakusanywa kwa kuuliza juu ya watu wote katika kaya ya mhojiwa. Kwa njia hii, timu hukusanya habari juu ya tabia mbalimbali za watu katika kaya,na wala siyo tu juu ya mambo ya kibinafsi ya mhojiwa.

Timu ya uchunguzi inamuuliza mhojiwa kukamilisha jedwali lifuatalo kama lilivyo andikwa katika Mwangozo wa uchunguzi. Kila mmoja wa wanakaya anaandikwa katika safu ya kwanza na habari kumhusu zinaandikwa upande wa kulia.

| Wanakaya* | Umri | Jinsia | Kiwango cha elimu kilichofikiwa (uliza tu kama > miaka 16) | Dini** | Kabila | Lugha (lugha ya mama na nyenginezo) | Kazi ya msingi | Kazi ya pili |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| KK | | | | | | | | |
| | | | | | | | | |
| | | | | | | | | |
| | | | | | | | | |

**Watambue wote wanaoishi katika kaya ya mhojiwa kwa majina au jukumu (kwa mfano bibi)*
*** Habari juu ya ushirikishi wa kidini inaweza kuwa nyeti kuuliza katika ngazi ya kaya. Inaweza kufaa zaidi kuipata kutoka ngazi ya jamii kwa kutumia watoaji habari wakuu au chanzo pili.*
*KK: inaonyesha ni nani mkuu wa kaya (kwa mfano mama) na kama ni mwanamke mjane (m)*

**Jinsi ya kuchambua takwimu**

*Uchambuzi wa kazi*

Kwa uchambuzi wa kazi zinazofanywa na jamii, kwanza zitambue kazi zote zilizotajwa wakati wa mahojiano na ziorodheshe katika jedwali ndani ya karatasi ya uchambuzi wa uchunguzi(angalia mfano). Baada ya hapo, piga hesabu ya jumla ya watu katika jedwali la kaya ambao wameorodhesha kazi hii kama kazi yao ya msingi. Halafu piga hesabu ya asilimia ya watu wote ambao wameajiriwa katika kila kazi kama shughuli yao ya msingi kwa kugawanya idadi ya watu walioandikwa kwa kila shughuli kwa jumla ya watu katika kaya kama ilivyoandikwa ndani ya karatasi ya uchambuzi wa uchunguzi na kuelezwa katika jedwali.

Fanya hesabu za aina hiyo kwa kazi ya pili kwa, kwanza kupiga hesabu ya jumla ya watu kutoka kwenye kaya zote ambao wameandika kila shughuli kama kazi yao ya pili. Halafu piga hesabu ya asilimia ya watu kutoka kwenye kaya ambao wameandika kila shughuli kama kazi yao ya pili kwa kugawanya idadi ya watu wa pili kwa kila kazi kwa jumla ya watu katika kaya zote zilizohojiwa

kama ilivyo elezwa ndani ya jedwali. Pia angalia kwamba jumla ya asilimia ya wakazi wa kaya wenye kazi ya pili ni chini ya asilimia 100. Hii ni kwa sababu si kila mkazi kwenye kaya anayo kazi ya pili. Katika mfano ufuatao hapa chini, asilimia 80 wana kazi ya pili na asilimia 20 hawana.

Mwisho, jumlisha asilimia kutoka kwenye kazi ya msingi na kazi ya pili kwa kila kazi ili kujua jumla ya asilimia ya wanajamii wanaotegemea kila kazi kama ilivyoonyeshwa katika jedwali. Angalia kwamba jumla inakuwa zaidi ya asilimia 100. Hii ni kwa sababu jumla ya asilimia yote iinajumuisha kazi ya msingi na ya pili ya wanakaya. Kwahivyo, wanahesabiwa mara mbili endapo wana kazi ya pili.

| Kazi | MSINGI | | YA PILI | | Jumla ya asilimia ya wanajamii wanaotegemea kazi hii (kazi yao ya msingi na ya pili) |
|---|---|---|---|---|---|
| | Idadi ya wanakaya walioorodheshwa kama kazi ya msingi | Asilimia ya wanakaya ambao wameorodheshwa kama kazi ya msingi | Idadi ya wanakaya walioorodheshwa kama kazi ya pili | Asilimia ya wanakaya ambao wameorodheshwa kama kazi ya pili | |
| *Uvuvi* | 65 | 32.5% | 50 | 25% | 57.5% |
| *Maendeleo ya hoteli* | 50 | 25% | 20 | 10% | 35% |
| *Kilimo* | 30 | 15% | 60 | 30% | 45% |
| *Nyinginezo* (Uchimbaji wa matumbawe, kilimo)* | 5 | 2.5% | 30 | 15% | 17.5% |
| *Hawana kazi*** | 50 | 25% | 0 | 0% | 25% |
| *JUMLA* | 200 | 100% | 160 | 80% | 180% |

**Andika pamoja kazi zote ambazo zimetajwa <5% ya wanakaya wote*
***Kwa mfano, wasio na ajira, wanafunzi, waliostaafu.*

*Uchambuzi wa ziada:* Linganisha majawabu haya na takwimu kutoka kwa watoaji habari wakuu/ chanzo pili *kazi (K7),* ambacho kinauliza asilimia ya idadi ya watu wanaendesha kazi hii kama kazi yao ya msingi na kazi yao ya pili. Ikiwa kuna tofauti zinazoonekana basi waone watoaji habari wakuu kuelezea sababu. Endapo tofauti haiwezi kuelezeka inaweza kuwa muhimu kufanya uhojaji upya kwa kaya zote kwa usahihi zaidi ili kupata muundo wa kazi. Kulinganisha asilimia ya kaya kwa usahihi, kutahitaji kupigwa hesabu kwa kuzingatia watu walioorodheshwa kuwa wanafanya kazi (yaani siyo kuwahusisha wale ambao wameorodheshwa kuwa "hawana ajira" au ni "wanafunzi" kama kazi yao).

Linganisha mabadiliko katika idadi ya watu kwa kila kazi kwa muda fulani na takwimu katika mabadiliko ya *njia/mbinu (K20), viwango na aina ya athari (K25)*, na hali ya rasilimali kwa muda fulani ili kutambua uhusiano wowote.

Pia piga hesabu ya mabadiliko katika muundo wa kazi kwa muda fulani. Chukuwa asilimia ya mwaka wa sasa na idadi na utoe asilimia ya miaka iliyopita kuona kama kuna ongezeko, upungufu au hakuna mabadiliko.

**Uchambuzi wa idadi ya watu**

Kwa kila kazi ya msingi, piga hesabu ya asilimia ya watu katika kila kundi la umri mmoja, kundi la elimu, kundi la kabila, kundi la dini na kundi la jinsia na andika asilimia hizi ndani ya karatasi ya kupimia uchambuzi (angalia mfano huu hapa chini wa jedwali la umri na elimu)

| | ASILIMIA YA MAITIKIO | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kazi ya Msingi | Umri 0-15 | Umri 16-25 | Umri 26-45 | Umri Zaidi Ya 50 | < miaka 6 ya kusoma | Miaka 6-9 ya kusoma | > miaka 9 ya kusoma |
| *Uvuvi* | 6% | 20% | 39% | 35% | 10% | 60% | 30% |
| *Maendeleo ya hoteli* | 0% | 45% | 30% | 25% | 5% | 30% | 65% |

*Uchambuzi wa ziada:* Linganisha hizi takwimu zinazohusiana na idadi ya watu kwa kazi zote pamoja na takwimu *za mahojiano/chanzo pili, umri, jinsia, elimu, kujua kusoma na kuandika, kabila, dini na lugha (K8-14)*. Kama kuna tofauti kubwa zinazoonekana, basi wasiliana na watoaji habari wakuu kuelezea sababu. Kama tofauti haielezeki, inaweza kulazimu kufanya mahojiano kwa kaya zote ili kuweza kuelezea kwa usahihi zaidi idadi ya watu katika jamii. Kwa kuongezea, masimulizi mafupi yanaweza kuandaliwa kuelezea sifa za kila kundi la kazi.

**Uchambuzi wa ukubwa wa kaya na muundo wa kaya**

Piga hesabu ya wastani wa ukubwa wa kaya kwa kujumlisha idadi ya watu katika kila kaya halafu gawanya kwa idadi ya kaya.

Piga hesabu ya wastani wa idadi ya wanaume kwa kaya kwa kujumlisha idadi ya wanaume katika kaya halafu gawanya kwa jumla ya kaya zote. Kupata idadi ya wanawake, piga hesabu ya wastani wa wanawake katika kila kaya kwa kujumlisha idadi ya wanawake katika kaya halafu gawanya kwa idadi ya kaya zote. Fanya hivyo hivyo kwa idadi ya watoto.

Piga hesabu ya asilimia za kaya zinazoongozwa na wanawake na asilimia za kaya zinazoongozwa na wanawake wajane kwa kujumlisha idadi ya kaya zinazoongozwa na wanawake na zile zinazoongozwa na wanawake wajane. Gawanya namba hizi kwa jumla ya idadi ya kaya zilizohojiwa, halafu zidisha kwa 100 *(Angalia karatasi ya kupima uchambuzi.)*

**Umuhimu wa habari hizi kwa wasimamizi na wadau wengine**

Pamoja na takwimu za idadi ya watu zilizotolewa kutoka kwa watoaji habari wakuu/chanzo pili, takwimu kutoka kwa wapimaji zinachambuliwa mahsusi kwa kila kazi. Hii humpatia msimamizi kuelewa aina ya watu walioajiriwa katika kazi tofauti ambazo zinaweza kumsaidia kupanga mipango ya usimamizi. Kwa mfano, iwapo kiongozi anafahamu kwamba idadi kubwa ya wakulima wa viumbe baharini hawajui kusoma wala kuandika na idadi kubwa ya wenye hoteli wameelimika vya kutosha kwahivyo anaweze kuandaa mpango mzuri wa elimu.

Kaya zinazoongozwa na wanawake na hasa kaya zinazoongozwa na wanawake wajane zinatabia ya kuwa masikini zaidi katika jamii. Msimamizi kwa kuzingtia hali hiyo anaweza kuandaa mpango kwa ajili ya kaya hizi ambao unaweza kutambulika mahsusi kama makundi dhaifu kwa mabadiliko katika usimamizi wa rasilimali.

Kwa kuchangia katika ukusanyaji wa habari katika muundo wa jamii, wadau wataweza kusaidia kuhakikisha kuwa wasimamizi wanapata uelewa mzuri wa kiwango kikubwa cha wadau na wanakuwa na uwezo wa kuunda shughuli za usimamizi ambazo ni nzuri kwa ajili yao.

## *S10. Vyanzo vya Mapato ya Kaya*

**Ni nini**

Kipato cha kaya kinahusu vyanzo vikuu vya kuingiza kipato (chumo)cha kaya. Habari hii inakusanywa pamoja na kazi zinazofanywa na wanajamii ili kutambua chanzo chochote cha chumo (mapato) ambacho hakihusiani na kazi kama vile misaada toka nje.

**Jinsi ya kukusanya takwimu**

Kama ilivyoandikwa katika mwongozo wa uchunguzi, takwimu juu ya kipato zinapatikana kwa kuuliza kila mhojiwa:

Nini chanzo muhimu zaidi cha kipato cha kaya yako? -------------------
Nini chanzo cha pili muhimu cha kipato cha kaya yako?------------

Angalia kwamba ukusanyaji wa takwimu hii unaweza ukawa nyeti kwa baadhi ya watu kwa vile ni ya kibinafsi. Timu ya uperembaji inahitaji kwa uangalifu kufikiria eneo lao la utafiti pamoja na wanajamii ili kujua kama ni sahihi kuuliza swali hili.

**Jinsi ya Kuchambua takwimu**

Kwa kila kazi, piga hesabu ya asilimia ya wahojiwa ambao walisema kuwa ni chanzo cha msingi wa kipato cha kaya yao na asilimia ya wale waliosema kuwa ni chanzo cha pili cha kipato cha kaya yao na andika hizi asilimia katika *karatasi ya uchambuzi wa uchunguzi.*

*Uchambuzi wa ziada:* Linganisha matokeo haya na takwimu juu ya *kazi (K7 na S1)* kuhakikisha kazi hizo ni muhimu zaidi. Angalia kuwa kuna uwezekano wa kuwepo na tofauti kutokana na vyanzo vya kipato ambavyo siyo kazi (kwa mfano, kupatiwa fedha). Fuatilia matokeo haya kwa muda fulani kutambua mabadiliko katika umuhimu wa kazi tofauti tofauti.

**Umuhimu wa habari hizi kwa wasimamizi na wadau wengine**

Habari juu ya vyanzo vya msingi na vyanzo vya pili vya kipato ni muhimu kwa kudhihirisha umuhimu wa rasilimali kwa jamii. Kwa mfano, iwapo zaidi ya asilimia 80 ya jamii wanachukulia uvuvi kuwa ndiyo chanzo cha msingi au cha pili cha kipato, basi hii inaonyesha kuwa kiwango kikubwa cha jamii hutegemea uvuvi na kwahivyo kwa rasilimali za bahari.

Kwa kufahamu vizuri umuhimu wa shughuli mbalimbali kwa kipato, jamii inaweza kutoa mchango wa mawazo kusaidia wasimamizi kuboresha shughuli za usimamizi na kutia maanani athari za sheria na kanuni kwa mustakabali wa maishilio ya wadau.

## *S11. Hali ya makazi*

**Ni nini**

Makazi yanaonyesha endapo wanakaya ni wakazi wa muda mrefu au hapana, na kama la, kipindi chao cha kukaa. Makazi yatatoa habari kwa undani zaidi juu ya utaratibu wa uhamaji na kukamilisha habari za *kiwango cha uhamiaji (K6).*

**Jinsi ya kukusanya takwimu**

Habari juu ya makazi inakusanywa kwa kupitia uchunguzi. Wahojiwa wanaulizwa endapo wana makazi ya kudumu katika eneo la uchunguzi au wanaishi kwa muda. Halafu wanaulizwa juu ya muda walioishi na asili yao kama wamekaa kwa musimu (kwa muda).

| Mwana kaya* | Kudumu / kwa muda | Idadi ya miaka ya kudumu | Idadi ya miaka ya muda | Kwa muda asili | Kwa muda miezi gani | Kazi ya msingi | Kazi ya pili |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | |
| | | | | | | | |
| | | | | | | | |
| **Watambue wahojiwa kwa majina na majukumu yao (kwa mfano: baba)* | | | | | | | |

***Angalia**:* Itakuwa muhimu kufanya uhojaji na watoa habari wakuu juu ya mtindo wa uhamaji wa makundi tofauti tofauti ya wadau kwa vile hii itasaidia kubuni njia ya uchunguzi (yaani kwa ajili ya timu ya uperembaji kufahamu ni wapi wanapoishi wahamaji wa muda na huwa wanakuja lini hasa). Maswali juu ya makazi yanaweza kujumuishwa na yale ya uchunguzi wa idadi ya watu. Inaweza ikawa sahihi zaidi wakati mwengine kuchunguza mtindo wa uhamiaji kulengana na misimu kwa kutumia watoaji habari wakuu au kwa kuhoji vikundi maalum kwa kuchukuwa sampuli za wahamaji wa misimu. Baadaye watoaji habari wakuu wanaulizwa kuhusu wahamaji wa majira (kulingana na shughuli wanazopenda), asili yao na wakati wanapokuja.

Idadi kubwa ya wavuvi wa majira kutoka Pwani ya Kusini wanakwenda kuvua Kilifi, Pwani ya Kaskazini ya Kenya, wakati wa kaskazi na wanaishi bandarini. Itakuwa muhimu kuwahoji watoa habari wakuu kuona mtindo wa uhamaji ili kuweza kupata habari hii katika uchunguzi (hakikisha kwamba sampuli zinakuwa na uwakilishi wa kutosha).

**Jinsi ya kuchambua takwimu**

Onyesha asilimia ya wadau wa kudumu, na upige hesabu ya asilimia ya watu katika makundi ya wale wa muda na wale wa kudumu. Kwa kila kundi wa kudumu/muda, piga hesabu ya asilimia ya idadi ya watu ambao wamekaa/wamezuru kwa zaidi au chini ya miaka 5.

Kwa idadi ya watu ambao wanahama piga hesabu ya asilimia ya wahamaji wa muda/majira wanaokuja kwa majira tofauti tofauti, asilimia ya wahamaji wa muda kwa kila aina ya muda, na asilimia wahamaji wa muda kulengana na kabila (asili) zao. Pia piga hesabu ya wastani wa kipindi cha kukaa kwa idadi ya watu wa muda na asilimia ya wahamaji wa muda kwa kila musimu. Andika hizi asilimia na wastani ndani ya *karatasi ya uchambuzi wa uchunguzi* (angalia mifano hiyo hapo chini kwa miaka na asili).

| ASILIMIA YA MAITIKIO | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Kazi ya Msingi | ASILIMIA YA MAITIKIO | | | KUDUMU | | |
| | Ya Kudumu | Ya Muda | Jumla | Miaka 1-5 | Miaka >5 | Jumla |
| Uvuvi | 70% | 30% | **100%** | 20% | 80% | **100%** |
| Maendeleo ya Hoteli | 50% | 50% | **100%** | 55% | 45% | **100%** |

Kwa uchambuzi wa asili ya wahamaji wa muda, orodhesha asili zote zilizotajwa wakati wa mahojiano katika jedwali kama inavyoonyeshwa ndani ya *karatasi ya uchambuzi wa uchunguzi* halafu ziweke kwenye makundi ya uwakilishi kwa utaratibu wa kijiografia (kwa mfano Kanda ya 1, Kanda ya 2, Kanda ya 3, au Pwani ya Kaskazini, Pwani ya Kusini n.k.) na kisha piga hesabu ya asilimia ya wahamaji wa muda wanaokuja kutoka maeneo mbalimbali. Aina lazima zielezwe kikamilifu.

| ASILIMIA YA MAITIKIO | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | WAHAMAJI WA MUDA (MAJIRA) | | | | | | | |
| **Kazi ya Msingi** | **Miaka 1-5** | **Miaka >5** | **Jumla** | **Asili Kitaifa Pwani Kaskazini** | **Asili Kitaifa Pwani Kusini** | **Asili Kitaifa Bara** | **Asili Kigeni** | **Jumla** |
| *Uvuvi* | *50%* | *50%* | **100%** | *30%* | *40%* | *0%* | *30%* | **100%** |
| *Maendeleo ya Hoteli* | *55%* | *45%* | **100%** | *33%* | *17%* | *40%* | *10%* | **100%** |

*Uchambuzi wa ziada:* Matokeo yanaweza kwa urahisi zaidi kuwasilishwa katika chati za mfano wa mnara wa sabuni (bar charts) au chati za mfano wa sambusa au andazi (pie charts).

Linganisha mabadiliko kwa kipindi cha miaka kadhaa katika asilimia ya wahamaji wa muda/kudumu kwa kila kazi. Linganisha mabadiliko kwa kipindi cha miaka kadhaa katika asili na urefu wa kukaa wa wahamaji wa muda (majira). Chukuwa asilimia ya mwaka uliopo toa idadi ya asilimia ya mwaka uliopita kuona kama kuna ongezeko, upungufu au kama hakuna badiliko.

Linganisha mabadiliko kwa kipindi ya idadi ya asilimia ya wadau wa kudumu na wale wa muda, na asili ya wahamaji wa muda pamoja na takwimu katika mabadiliko *ya kazi zinazofanywa na jamii (S1)* na *viwango na aina ya athari (K25)*. Linganisha mabadiliko ya idadi ya watu katika majira fulani na ile idadi ya watu ambao wamekuja kuishi hivi juzijuzi na *njia/mbinu (K20)* kuona kama kuna uhusiano. Linganisha pia matokeo na mabadiliko katika *kiwango cha uhamiaji (K6)* na *kiwango cha utumiaji kwa watu wa nje (24).*

**Umuhimu wa habari hizi kwa wasimamizi na wadau wengine**
Ukazi unatoa maelezo kwa undani zaidi juu ya kiwango cha uhamaji na itasaidia sana kuelewa athari. Jinsi watu wanavyoingia katika sehemu moja iwe ni kwa kudumu au kwa muda, msongo juu ya rasilimali unaongezeka. Ulinganisho wa hali ya rasilimali na viwango vya athari ni vizuri zaidi ili kuona endapo wageni wanahusika na hali ya mabadiliko na athari.

Kuelewa ukazi kutakuwa pia muhimu kwa kuchanganyika na wadau, hususan kwa kuandaa mipango ya uhamasishaji. Wahamiaji wa muda na wale ambao wamekaa hivi majuzi wanaweza wasifahamu mipango ya usimamizi wa rasilimali za pwani na za baharini kuliko wale wenyeji wa muda mrefu. Wahamiaji wanaweza wasiwe na ufahamu wa kutosha na ushawishi wa kutosha kukubaliana na sheria na kanuni za usimamizi wa pwani zilizoanzishwa. Zaidi ya hivyo, endapo msimamizi anaelewa ni shughuli zipi wahamiaji wa muda wanafanya, anaweza akaziwekea malengo. Kwa mfano, kama kuna wahamiaji wanaokata mikoko bila kujua ikolojia ya pwani, msimamizi anaweza kuanzisha uhamasishaji kwa kutumia video juu ya umuhimu wa mikoko kwa uendelevu wa rasilimali zenginezo za pwani na bahari.

Habari juu ya ukazi zitakuwa na matumizi ya moja kwa moja kwa jamii. Hii inaweza ikawa njia mojawapo kwa jamii kuthamini endapo kumekuwa na ongezeko la kuwepo kwa nafasi za ajira zitakazoundwa chini ya mpango wa usimamizi. (kwa mfano, endapo mojawapo ya mawazo ya watu katika habari ya makazi itakuwa kuhakikisha kuwa wasimamizi watawahusisha kwenye maamuzi ya usimamizi ambayo yatakuwa na athari kubwa kwao.

## AFYA

## *K15. Kiasi cha vifo vya watoto, vifo kutokana na magonjwa*

**Ni nini**
Vifo vinavyosababishwa na magonjwa (pamoja na majonjwa yanayochukuzwa na maji) na kiasi cha vifo vya watoto ni kipimo cha ubora wa afya ya jamii katika eneo la uchunguzi. Ni idadi ya vifo vya watoto wachanga (miezi 18-24) ikilinganishwa na idadi ya watoto wa umri huu, na asilimia ya vifo vinavyotokana na magonjwa katika eneo la uchunguzi.

**Jinsi ya kukusanya takwimu**

Habari hii inakusanywa katika vyanzo vya pili, kama vile taarifa za vifo kwenye eneo (NGO au mashirika ya serikali), au idara ya afya. Inaweza pia kukusanywa kutoka kwa watoa habari wakuu, kama vile wakurugenzi wa hospitali, wakurugenzi wa afya vikundi, vyama vya uhamasishaji, n.k. Wakati mwengine vifo na uzazi huandikwa katika ngazi ya kijiji na viongozi wa jamii.

*Ukusanyaji wa takwimu za ziada:* Timu ya uperembaji inaweza kutaka kukusanya habari kuhusu kuwepo kwa UKIMWI katika eneo la uchunguzi. Hii mara nyingi ni habari nyeti. Pia ni habari ngumu kuipata kwa vile mara nyingi kifo husababishwa na magonjwa mengine mbali na UKIMWI. Kupata habari ya UKIMWI inaweza kuwa bora zaidi kuyaendea mashirika yasiyokuwa ya serikali (yaani NGO) au mashirika mengine ambayo yanashughulika na uhamasishaji na kutibu magonjwa yatokanayo na UKIMWI (kwa mfano MFS). Mashirika haya yaweza kuipatia timu ya uchunguzi makadirio ya asilimia ya watu wenye UKIMWI katika eneo la uchunguzi.

Kama iilivyoonyeshwa katika *vyanzo vya pili/mwongozo wa mahojiano*, maswali ya msingi ya kuulizwa ni:

Ni kiasi gani cha vifo vya watoto wachanga wenye umri kati ya miezi 18-24 kwa mwaka? _________(kwa kila watoto elfu moja)

Ni asilimia ngapi ya vifo kwa mwaka katika eneo la uchunguzi husababishwa na (orodhesha magonjwa ya kawaida ukijumuisha pia magonjwa yanayosababishwa na maji):

Malaria ________; Kipindupindu/ Kuhara damu: ________; Homa ya matumbo: ________

**Jinsi ya kuchambua takwimu**

Yakinisha asilimia ya vifo kwa kila kundi na andika katika karatasi ya mahojiano/vyanzo vya pili. Mfano wa magonjwa ni kama huu unaofuata.

Asilimia ya vifo vinavyosababishwa na: Malaria 10%; Kipindupindu 15%; Homa ya matumbo 3%.

*Uchambuzi wa ziada:* Linganisha asilimia hizi na miaka ya nyuma (toa asilimia ya mwaka huu na miaka iliyopita ili kuangalia endapo asilimia imeongezeka, imepungua au imebaki kama ilivyokua awali. Linganisha mabadiliko katika afya na mabadiliko katika *miundo mbinu katika jamii na biashara (K16)* na *matatizo ya jamii (S25).*

**Umuhimu wa habari hizi kwa wasimamizi na wadau wengine**

Kwa kufanya uperembaji wa hivi vipengele vya afya, msimamizi anaweza akaona kama afya ya jamii na ubora wa hali zao unaongezeka, unapungua, au umebaki kama ulivyokuwa. Kama asilimia kubwa ya jamii hawana njia nzuri za kupata maji safi, ufahamu mdogo wa afya au/na kwamba huduma za afya hazitoshelezi.

Kama usimamizi wa pwani unaboresha maishilio na kipato, na kuongezeka kwa utajiri kwa ujumla katika jamii, basi inaweza ikatazamiwa kwamba ubora wa afya ya jamii unaweza kuongezeka. Ugumu ni kuingiza mabadiliko haya kwenye usimamizi wa pwani. Katika hali nyengine hizi zinaunganishwa; kwa mfano, kama mpango wa usimamizi umewezesha kupatikana kwa maji au kusafisha maji machafu kwa jamii, inaweza ikakisiwa kwamba magonjwa yaletwayo na maji yatapungua. Lakini katika hali zingine, kama usimamizi hauhusishwi na miradi ya miundo mbinu, basi uhusiano unaweza ukawa mgumu kugundua.

Kuelewa ubora wa afya katika eneo la uchunguzi kutasaidia pia wasimamizi kuyakinisha malengo halisi ya usimamizi ambayo ni nyeti kwa matatizo yanayoyoweza kuwapata wadau. Kwa mfano, kama ubora wa afya ni wa kiwango cha chini sana wasimamizi wanaweza wakatarajia ugumu katika kuishirikisha jamii kwenye shughuli za uhifadhi.

Mabadiliko katika ubora wa afya yanaweza yakaongeza ufahamu wa wadau wa jinsi ubora wa maisha unavyoongezeka, unavyopungua au unavyobaki katika hali hiyohiyo kulengana na miaka.

## MIUNDOMBINU YA JAMII NA MAENDELEO YA BIASHARA

### *K16. Miundombinu ya jamii, maendeleo ya biashara na umilikaji*

**Ni nini**

Miundombinu ya jamii ni kipimo cha kijumla cha maendeleo ya jamii na utajiri. Ni maelezo ya kiwango cha huduma za jamii (kwa mfano hospitali, shule) na miundombinu (kwa mfano barabara,na huduma nyingine , ambazo zinaweza zikahusisha habari ambazo ni muhimu kuweza kuelezea vyanzo vya athari zinazotokana na wanadamu kwenye rasilimali za pwani (kwa mfano huduma za maji

taka). Maendeleo ya biashara ni kipimo cha jumla cha maendeleo ya kiuchumi ya jamii. Kimejikita katika idadi na aina za shughuli za biashara katika eneo na ni akina nani wanaozimiliki (kama wamiliki ni wa kutoka nje ya nchi, raia lakini sio wenyeji au wenyeji na kama ni wageni, raia lakini sio wenyeji au ni wenyeji). Umiliki wa biashara utatoa ufahamu endapo kipato kutokana na hizi biashara kina uwezekano wa kutumika katika eneo, na hivyo basi kuwa na kiwango kikubwa au cha kati cha athari kwa maendeleo ya eneo.

**Jinsi ya kukusanya takwimu**

Habari hii inakusanywa kwa kuwahoji watoa habari wakuu, viongozi wa jamii au wahandisi wa mji; kuzipitia takwimu za pili kutoka taarifa za mji, hususan ofisi ya maendeleo ya jamii, na kwa kutembea katika jamii, kuangalia na kuhesabu miundombinu ya jamii.

Kwa miundombinu ya jamii ni muhimu kueleza endapo vitu vifuatavyo vinapatikana katika eneo la uchunguzi:

shule, madaktari wakazi, wauguzi wakazi, hospitali, zahanati zinazofanya kazi, umeme, simu, upatikanaji wa mtandao wa internet, redio, runinga, magazeti, mitambo ya kusafishia maji taka, mitambo ya barafu, barabara za lami, usambazaji wa maji katika majumba, huduma za benki, majengo ya ibada (misikiti, makanisa, mahekalu).

Kwa maendeleo ya biashara ni muhimu kuelezea endapo vitu vifuatavyo vinapatikana katika eneo la uchunguzi:

masoko ya vyakula, migahawa, mabanda ya vyakula, vituo vya mafuta, benki, maduka maalum, maduka ya zawadi, maduka ya vifaa vya kuzamia, shughuli za kitalii, uongozaji uvuvi, nyumba za wageni/hoteli/nyumba za wageni zenye kutoa huduma za vyakula/sehemu za pwani ambazo watu wengi hupenda kutembelea/sehemu za kukodisha mashua.

Kwa kila kitu kilichoorodheshwa itakuwa ni muhimu kufahamu ni nani mmiliki wa hiyo biashara (yaani sehemu ya kuishi hao wamiliki na asili zao). Matabaka tofauti ya wamiliki watawekwa kwenye madaraja kulingana wingi wa idadi kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali hapa chini. Aina za uraia na asili zielezwe kwa uwazi.

| Biashara | Asili na sehemu ya makazi | Daraja* |
|---|---|---|
| | | |
| | | |
| | | |
| *Panga madaraja kulengana na wingi: aina ya wamiliki wachache kabisa watakuwa daraja 1* | | |

Sehemu ya makazi inahusu ni wapi mmiliki hasa anapoishi (nje ya nchi, nchini, katika eneo) na asili ni kule mmiliki anakotoka.

Katika hali zingine orodha hizi zinahitaji kugeuzwa kidogo ili zimulike kwa usahihi zaidi vigezo vya miundombinu ya jamii na maendeleo ya biashara katika eneo. Ni muhimu kujumuisha safu za miundombinu katika sehemu hiyo. Kwa mfano, kama runinga tayari zinapatikana kwa wingi katika sehemu hiyo, lakini vipokezi vya satilaiti ndiyo sasa vinaanza kutokea, kwahivyo itakuwa ni vizuri kuingiza vipokezi hivyo katika orodha. Utengenezaji wa mizani sahihi unahitajika ili kufanya ulinganifu wenye maana kati ya jamii na kwa muda, kama vile kabla na baada ya kuanzishwa kwa eneo la bahari lisiloruhusiwa kuvuliwa.

*Ukusanyaji wa takwimu za ziada:* Timu ya uperembaji inaweza pia kukusanya habari maalumu kuhusu idadi na sifa za vitu hivi.

**Jinsi ya kuchambua takwimu**

Orodhesha vifaa vya miundombinu vilivyopatikana kupitia kwa uangalizi, , watoa habari wakuu, mahojiano na vyanzo vya pili katika *karatasi ya uchambuzi mahojiano/chanzo pili.*

Mfano wa matokeo katika umilikaji wa biashara umetolewa hapa chini.

| Biashara | Asili na sehemu ya makazi ya wamiliki | Daraja* |
|---|---|---|
| Waongozaji uvuvi | Wenyeji, wakazi,<br>Wageni, wakazi | 1<br>2 |
| Wafanyi Biashara ya samaki | Wenyeji, wakazi<br>Mwananchi ambaye si mwenyeji | 1<br>2 |
| Waendeshaji Biashara ya utalii | Watu toka nje ya nchi, wageni<br>Mwananchi ambaye si mkazi, asiye mwenyeji<br>Wageni, wakazi | 1<br>2<br>3 |

*Uchambuzi wa ziada:* Linganisha orodha hizi kwa muda fulani. Maelezo mafupi kuhusiana na orodha hii yanaweza kutayarishwa kuelezea miundombinu katika eneo la uchunguzi na jinsi zilivyobadilika kwa wakati. Linganisha aina ya wamilikaji na uone jinsi madaraja yanavyojitokeza kwa wakati na aina ya wamiliki wengine wanavyojitokeza.

**Umuhimu wa habari hizi kwa wasimamizi na wadau wengine**

Miundombinu ya jamii na maendeleo ya biashara ni muhimu kwa kuelezea jinsi msimamizi anaweza kuona kama utajiri na ubora wa maisha ya jamii vinaongezeka, vinapungua au vimebaki kama vilivyokuwa tangu awali. Kwa mfano, ongezeko katika shughuli za biashara, kama vile maduka ya vifaa vya kuzamia, hoteli na migahawa kwa ajili ya watalii, inaashiria ongezeko kwa jumla katika maendeleo ya uchumi wa jamii. Ugumu upo katika kuyaingiza mabadiliko haya katika harakati za usimamizi wa pwani. Katika hali zingine haya yanafungamana kwa karibu; kwa mfano, kama mpango wa usimamizi umewezesha kupatikana kwa maji au usafishaji wa maji machafu katika jamii. Katika maeneo mengine, wasimamizi wa pwani hawana jukumu la miundombinu katika jamii.

Habari za kuwepo huduma za benki, barafu kwa ajili ya wavuvi na barabara nzuri zinazoweza kupitika kwa majira yote zinaweza kuwa za manufaa kwa kutambua uwezo wa wavuvi kuimarisha biashara yao. Wakati huo huo, habari juu ya usafishaji wa maji machafu zinatoa ufahamu endapo maji taka yasiyosafishwa yanaweza yakaathiri ubora wa maji ya pwani. Habari juu ya nyumba za wageni, hoteli/ nyumba za wageni zinazotoa huduma za vyakula, migahawa ni za manufaa kwa kuelezea hali jumla ya kiwango cha utalii katika eneo.

Kuelewa aina mbalimbali za wamiliki biashara itawawezesha wasimamizi kuandaa uhamasishaji na mipango ya kazi kwa wamiliki tofauti tofauti na kuwahusisha kikamilifu zaidi katika shughuli za usimamizi wa pwani na bahari. Asili ya wamiliki itaashiria endapo faida za kiuchumi zitokanazo na biashara kwa uhakika zinabakia kwa jamii, au faida hupelekwa kwingineko.

Mwisho, habari juu ya kuwepo kwa simu, mtandao wa internet, radio, runinga na magazeti ni muhimu kwa maendelezi ya elimu na mipango ya kuifikia jamii. Kampeni za uhamasishaji zinaweza kuandaliwa kwa kutumia chombo cha habari kinachopatikana kwa wingi zaidi.

## *K17. Vyanzo na upatikanaji wa mikopo*

**Ni nini**

Vyanzo na upatikanaji wa mikopo ni kipimo cha jumla cha upatikanaji wa mikopo kwa wadau, na nafasi ya wadau kujiendeleza na kupanua biashara zao. Ni orodha ya vyanzo vya mikopo aidha vya kawaida au visivyo vya kawaida (kwa mfano, mabenki, fedha za mzunguko (Upatu), vyama vya ushirika), masharti ya kupata mikopo na kiasi cha mkopo kinachotolewa na vyanzo hivi vya mikopo kwa mwaka.

**Jinsi ya kukusanya takwimu**

Habari hii inakusanywa kupitia watoaji habari wakuu kama vile viongozi wa jamii, makatibu wa vyama vya ushirika, wanachama wa upatu, wakurugunzi wa benki, kwa kupitia taratibu za mikopo midogo midogo na kwa kuiangalia jamii.

Ni muhimu kuanzisha orodha ya vyanzo vya mikopo vya kawaida na visivyo vya kawaida katika eneo la uchunguzi: mabenki, taratibu za mikopo midogo midogo, vyama vya ushirika, upatu, wakopeshao fedha. Kwa kila kimoja ya vitu hivi wahojiwa wanaulizwa juu ya kiwango cha riba, masharti yanayowazuia kupata mkopo (kwa mfano masharti ya kuajiriwa, vizuizi vya jinsia, ukazi n.k) na timu ya uperembaji lazima iandike iwapo chanzo cha mkopo ni cha kawaida au si cha kawaida.

*Ukusanyaji wa takwimu za ziada.* Timu inaweza kutaka kupata habari juu ya kiwango cha mkopo uliotolewa kwa mwaka, na asilimia ya mikopo iliyorejeshwa. Hii itaonyesha hali ya umuhimu wa chanzo cha mikopo na uwezekano wake wa kuwa endelevu (kwa mfano, endapo mikopo mingi hailipwi, basi chanzo kinaweza kisidumu).

**Jinsi ya kuchambua takwimu**

Orodhesha vyanzo vya mikopo na sifa zake vilivyopatikana kwa watoaji habari wakuu, vyanzo vya mikopo na asilimia ya vyanzo vya mikopo vya kawaida. Piga hesabu ya wastani ya kiwango cha riba kwa aina tofauti tofauti za vyanzo vya mikopo (vya kawaida na visivyo vya kawaida) na baadaye fanya muhtasari wa masharti kulingana na aina ya chanzo cha mkopo.

*Uchambuzi ziada:* Linganisha jinsi orodha, masharti ya kupata, na mabadiliko ya viwango vya riba kwa miaka kadhaa. Linganisha mabadiliko haya na mabadiliko katika *Njia/Mbinu (K20,S14)*, na mabadiliko katika *maendeleo ya biashara na umilikaji (K16)* kuona endapo vina uhusiano. Linganisha pia mabadiliko katika vyanzo na kupatikana kwa mikopo na mabadiliko katika *namna ya maisha ya watu (S29)* na ona kama vina uhusiano.

**Umuhimu wa habari hizi kwa wasimamizi na wadau wengine**
Ugumu katika upatikanaji wa mikopo mara nyingi ni kikwazo katika mustakabali wa nafasi za maendeleo ya jamii za pwani. Kufahamu upatikanaji na sheria za kupata mikopo kwa jamii itawapatia wasimamizi uelewa wa nafasi zilizopo kwa wadau mbalimbali kuendeleza biashara zao. Hii pia itawasaidia wasimamizi kulenga shughuli za usimamizi kwa vikundi ambavyo vina nafasi haba au hawana kabisa nafasi ya kupata mikopo, na hivyo basi wanaweza kudhuriwa zaidi na mabadiliko katika usimamizi kama mabadiliko ni ya kuzuia. Kwa muda ikiwa vyanzo vya mikopo vitatokea, inaweza kuchangia kuleta kustawisha hali za jamii.

## SHUGHULI ZA PWANI NA BAHARINI

### *K18&S12. Shughuli*

**Ni nini**
'Shughuli za pwani na baharini' ni utambulizi wa matumizi ya rasilimali za pwani katika eneo la uchunguzi. Hizi ni shughuli zinazotumia au kuathiri moja kwa moja rasilimali za pwani au zisizotumia au kuathiri moja kwa moja. Hizi zinaweza kujumuisha, kwa mfano: uvuvi, biashara ya samaki, utalii, kilimo, usafiri baharini, kilimo, , uchimbaji wa matumbawe, uchimbaji wa mchanga, uzoaji wa mchanga chini ya maji, uchimbaji wa mafuta na gesi, vituo vya kijeshi, ukataji mikoko, ufyekaji wa misitu, viwanda na uhifadhi.

### NGAZI YA JAMII: K18

| Shughuli za pwani na baharini |
|---|
| *uvuvi* |
| *utalii* |
| *ufugaji wa viumbe baharini* |

**Jinsi ya kukusanya takwimu**
Takwimu juu ya shughuli za pwani na baharini zinapatikana kwa kuwahoji watoaji habari wenyeji kama vile viongozi wa vijiji, wafanyaji biashara, wavuvi, wafanyaji biashara za samaki na waongozaji watalii ili kutambua shughuli za pwani na baharini katika eneo hilo. Uangalizi pia unafanywa ili kutambua shughuli za matumizi katika eneo hilo. Orodha inakusanywa ya shughuli za pwani na baharini na kuandikwa katika *Chanzo pili/Mwangozo wa mahojiano* kama inavyoelezwa.

Kwa vile baadhi ya shughuli za pwani na baharini zinaweza kuwa za msimu, kufanyika nyakati hafifu au kufanyika mbali kabisa na nchi kavu, ni muhimu kutumia utaratibu wa njia mbili ikijumuishwa uangalizi kwa nyakati mbalimbali na kuwahoji watoaji habari wakuu mbalimbali ili kuhakikisha kuwa shughuli mbalimbali za pwani na baharini zinatambuliwa.

*Ukusanyaji wa takwimu za ziada:* Shughuli za pwani na baharini zinaweza kutambuliwa katika ramani ya eneo la uchunguzi. Kwa mfano, maeneo ya hoteli yanaweza kutambuliwa kwa kuyawekea rangi moja na maeneo ya kupigia mbizi rangi nyingine. Takwimu zinaweza kuonyeshwa kwenye ramani kwa njia ya ujumla au kwa namna ya pekee. Ni muhimu pia kuonyesha misimu ya shughuli kwa vile shughuli zingine, kama vile uvuvi na utalii, zinaweza kubadilika ndani ya mwaka mzima.

Timu ya uperembaji inaweza pia kuuliza kuhusu kuwepo kwa shughuli haramu, kama vile uwindaji wa samaki na madawa ya kulevya. Kwa vile shughuli hizi ni vigumu kuzipata kutoka kwa uchunguzi.

**Jinsi ya kuchambua takwimu**
Andika takwimu kutoka kwa watoa habari maalum mbalimbali na uangalizi halafu kamilisha jedwali ndani ya *karatasi ya uchambuzi wa mahojiano/chanzo pili* kama inavyoonyeshwa.

*Uchambuzi wa ziada:* Inaweza kuwa muhimu kuelezea kwa ufupi shughuli kuu za pwani na baharini katika eneo la uchunguzi.

### NGAZI YA KAYA: S12

| Shughuli za pwani na baharini |
|---|
| *uvuvi* |
| *utalii* |

**Jinsi ya kukusanya takwimu**
Mhojiwa anaulizwa kutaja matumizi yote ya rasilimali za pwani na baharini kwa wanakaya. Habari hii inaandikwa ndani ya jedwali la *mwangozo wa uchunguzi* kama inavyofafanuliwa.

*Ukusanyaji wa takwimu za ziada:* Timu ya uperembaji inaweza pia kutaka kuuliza kuhusu kuwepo kwa shughuli haramu, kama vile uwindaji wa samaki na madawa ya kulevya. Ni lazima ifahamike kwamba habari hii inaweza kupatikana toka kwa watoaji habari wakuu(angalia *K18*).

**Jinsi ya kuchambua takwimu**

Takwimu kutoka kaya zote zilizochunguzwa zinachambuliwa na kuwekwa katika madaraja kulingana na shughuli muhimu zaidi katika kaya zote. Shughuli iliyotajwa zaidi na kaya zote ipewe daraja la kwanza, ikifuatiwa na shughuli iliyotajwa ya pili kwa umuhimu zaidi n.k. Habari hii inaandikwa ndani ya karatasi ya uchambuzi wa uchunguzi kama inavyoonyeshwa.

*Uchambuzi wa ziada:* Inaweza ikawa vizuri kuelezea kwa ufupi shughuli tofauti tofauti za pwani na baharini za kaya katika jamii.

**Umuhimu wa habari hizi kwa wasimamizi na wadau wengine**

Utambuzi wa shughuli za pwani na baharini ni muhimu kwa msimamizi kupata ufahamu wa matumizi mbalimbali ya rasilimali za pwani na baharini, kama misafara mikubwa ya meli na umwagaji mkubwa wa taka unaweza kupingana na shughuli muhimu za sekta ya utalii.

Kuzidi kuelewa matumizi ya pwani na baharini kutaiwezesha jamii kuchangia vizuri zaidi kwenye maamuzi ya usimamizi, hususan migongano katika matumizi kunapotokea.

## *K19&S13. Bidhaa na Huduma*

**Ni nini**

Bidhaa na huduma za pwani na baharini ni mazao halisi yanayozalishwa kutokana na shughuli zilizotambuliwa za pwani na baharini. Hizi ni pamoja na zile bidhaa zinazoweza kuondolewa kama vile kamba mti, miti ya mikoko, mazao ya matumbawe na mchanga, na zile huduma zisizoondoa chochote baharini kama vile kupiga mbizi, kuogelea, utalii wa kutumia mashua zenye vioo, kufanya utalii kwenye misitu ya mikoko na uvuvi wa michezo.

### NGAZI YA JAMII: K19

**Jinsi ya kukusanya takwimu**

Takwimu juu ya bidhaa za pwani na baharini na huduma zinapatikana kwa kuwahoji watoaji habari wakuu kwa shughuli zinazowahusu.(kwa mfano wavuvi wa muda mrefu, raisi wa chama cha wenye mahoteli, wahudumu wa muda murefu wa mashua za kuzamia, viongozi wa waongozaji watalii) pamoja na watoaji habari wakuu wengine wenye ufahamu mwingi katika shughuli hizi (kama vile, maafisa wa serikali). Ni muhimu vile vile kuangalia shughuli za pwani na ushahidi wake halisi kwa habari zaidi na kama sahihisho kwa habari zilizopatikana kutoka kwenye mahojiano.

| Shughuli za Pwani na Baharini | Bidhaa na Huduma za Pwani na Baharini |
|---|---|
| Uvuvi | Kamba mti |
| | Chewa, Mjombo |
| Utalii | Hoteli |
| | Upigaji mbizi |
| Ufugaji wa viumbe baharini | Chaza |

Kwa kila shughuli mojawapo ya pwani na baharini, mtoaji habari mkuu anaulizwa kutambua bidhaa za pwani na baharini anazozalisha. Kwa mfano, kwa utalii bidhaa zinaweza kujumuisha pia hoteli na upigaji mbizi. Orodha ya bidhaa na huduma zinaandaliwa na kuandikwa ndani ya *chanzo kati/mwongozo wa mahojiano* kama ilivyo fafanuliwa.

Kwa vile baadhi ya bidhaa na huduma za pwani na baharini zinaweza kuwa za msimu, zinaweza kufanyika nyakati dhaifu au kufanyika mbali na nchi kavu, ni muhimu kutumia utaratibu wa njia nyingi, pamoja na kuangalia kwa nyakati mbalimbali na kuwahoji watoaji habari wakuu mbalimbali ili kuhakikisha kwamba bidhaa na huduma zote za pwani na baharini zimetambuliwa.

**Jinsi ya kuchambua takwimu katika ngazi ya jamii**

Tengeneza muhtasari wa habari kutoka kwa watoaji habari wakuu mbalimbali na uangalizi katika jedwali moja ndani ya karatasi ya uchambuzi wa mahojiano/chanzo pili kama inavyoonyeshwa.

*Uchambuzi wa ziada*: Kwa nyongeza inaweza kuwa ya manufaa, kwa mujibu wa jedwali hilo hapo juu kutoa maelezo mafupi juu ya bidhaa na huduma za pwani na baharini zinazozalishwa.

**NGAZI YA KAYA: S13**

| Shughuli za Pwani na Baharini | Bidhaa na Huduma za Pwani na Baharini |
|---|---|
| Uvuvi | Chewa, Mjombo |
| | Pweza |
| | Kamba |
| Utalii | Maendeleo ya hoteli |
| | Upigaji mbizi |
| | Uvuvi wa michezo |

**Jinsi ya kukusanya takwimu**
Mhojiwa anaulizwa kutaja bidhaa na huduma zote zinazozalishwa na shughuli za pwani na baharini za kaya. Habari hii inaandikwa ndani ya jedwali la *mwongozo wa uchunguzi kama* inavyofafanuliwa.

**Jinsi ya kuchambua takwimu**
Takwimu kutoka kaya zote zilizochunguzwa zinachambuliwa na kuwekwa kwa madaraja kulingana na bidhaa na huduma muhimu zaidi kutoka kwa kila shughuli katika kaya. Bidhaa na huduma zilizotajwa zaidi na kaya zote zipewe daraja la kwanza, zikifuatiwa na bidhaa na huduma za pili kwa kutajwa kwa wingi zaidi n.k. Habari hii inaandikwa ndani ya *karatasi ya uchambuzi wa uchunguzi* kama inavyoonyeshwa.

*Uchambuzi wa ziada:* Inaweza ikawa vizuri kuelezea bidhaa na huduma za pwani na baharini kwa kaya katika jamii kwa maelezo mafupi.

**Umuhimu wa habari hizi kwa wasimamizi na wadau wengine**
Habari juu ya bidhaa na huduma za baharini na pwani za kaya ni za muhimu kwa kuelezea athari kwa ujumla za usimamizi, hususan uuzaji na uzalishaji kwa kaya katika eneo la uchunguzi. Kwa sababu ya matokeo ya hatua za usimamizi, kunaweza kutokea mabadiliko katika bidhaa na huduma za baharini na pwani zinazotolewa katika eneo, zikiwa na athari zinazofaa na zisizofaa kwa kaya. Kwa mfano, endapo eneo la bahari lililozuiliwa shughuli za uvuvi linasababisha kuongezeka kwa shughuli za utalii katika eneo hilo, basi itatazamiwa kuwa thamani ya shughuli za upigaji mbizi zitaongezeka na kwahivyo wanakaya wengi watahamia kwenye shughuli za upigaji mbizi.

## *K20&S14. Njia/Mbinu*

**Ni nini**
Njia/mbinu zinaelezea njia ya kufanya kitu mahsusi au aina ya huduma inayotumiwa (kwa mfano, mitego, nyavu nyumba za wageni, uzamiaji) kwa kila huduma ya pwani na baharini.

**NGAZI YA JAMII: K20**

**Jinsi ya kukusanya takwimu**
Takwimu juu ya njia au mbinu zinapatikana kwa kuwahoji watoaji habari wakuu ambao ni wawakilishi wa makundi tofauti tofauti ya wadau (kwa mfano, raisi wa chama cha wavuvi, meneja wa shughuli ya muda mrefu ya uchimbaji wa mchanga). Kwa kuongezea, ni muhimu kutumia utaratibu wa njia nyingi, pamoja na kuangalia kwa nyakati mbalimbali na kufanya mahojiano na watoaji habari wakuu mbalimbali.

| Shughuli za pwani na baharini | Bidhaa na huduma za pwani na baharini | Njia/mbinu za msingi |
|---|---|---|
| Uvuvi | Kamba mti | Mitego |
| | Chewa | Mishipi |
| Utalii | Hoteli | Nyumba za wageni (zenye vyumba 1-7) |
| | Uzamiaji | Upigaji mbizi |
| Ufugaji wa viumbe baharini | Chaza | Mishipi/kamba |

Maswali muhimu ya kuuliza ni ni njia gani zinatumika kwa kila bidhaa na huduma. Kwa mfano kwa bidhaa za samaki (kama vile chewa, kamba mti), maitikio yanaweza kujumuisha mitego, nyavu, mishipi, uvuvi wa kutumia mikuki au uokotaji. Kwa huduma za hoteli chini ya shughuli za utalii maitikio yanaweza yakawa kutoka nyumba za kulala wageni (zenye vyumba 1-7) hadi nyumba za wageni zenye huduma za vyakula (vyumba 5-50) hadi hoteli/mahali pa pwani ambapo watu wengi hutembelea (>vyumba 50). Kwa ufugaji wa viumbe baharini maitikio yanaweza kuwa mabwawa, kamba, au vizimba. Kwa biashara ya samaki, maitikio yanaweza kuwa uuzaji wa samaki nyumba kwa nyumba kwa miguu au baiskeli au uuzaji wa samaki kitaifa kwa kutumia magari yenye barafu. Kwa usafirishaji wa baharini, majibu yaweza kuwa ujenzi wa bandari, usafirishaji wa bidhaa au mashua za michezo. Hii ni mifano tu. Timu ya uperembaji itahitaji kuunda madaraja ya majibu muhimu kulingana na sehemu inayohusika. Kwa mfano, kama kuna hoteli kubwa

pekee, basi timu itaweza kuamua kupanga maitikio kwa mujibu wa mahoteli endapo yanaweka gharama zote pamoja. Matokeo ya habari hii yaandikwe ndani ya jedwali la *chanzo pili/mwongozo wa mahojiano* kama inavyoonyeshwa hapa.

*Ukusanyaji wa takwimu za ziada:* Kwa kila moja ya aina hizi za matumizi, timu ingetaka kuuliza juu ya kiwango cha matumizi, kama vile idadi ya mitego na mishipi. Nambari hizi zinaweza baadaye kulinganishwa kwa kipindi fulani kuona kama viwango vimeongezeka, vimepungua au vimebakia kama vilivyokuwa mwanzoni.

Kwa takwimu za uvuvi, timu inaweza kuhitaji kuongeza safu nyingine ili kuzidi kuelezea aina za uvuvi kwa kuzingatia makundi yafuatayo:

*Uvuvi wa kiwango kikubwa* - kutumia vyombo vya nguvu, vifaa vya mashine, vinavyotumia umeme, mgawanyo wa kazi kwa vibarua, bidhaa zinapatikana ulimwenguni kote, uvuvi katika maji makuu.

*Viwanda* - Uwekezaji mkubwa, kutumia vyombo vya nguvu, vifaa vya mashine, vinavyotumia umeme, mgawanyo wa kazi kwa vibarua, bidhaa zinapatikana ulimwenguni kote, uvuvi katika eneo la maji makuu ya kitaifa.

*Uvuvi wa kiwango cha kati* - Mashua ndogo, mashine ndogo, vifaa ambavyo ni nusu vya mashine au vyote ni vya mashine ambavyo vinafanya kuunganishwa na wahudumu, vibarua au wafanya kazi wa kudumu, zana za kutumia mashine au bila mashine, masoko ya ndani na nje, uvuvi katika bahari ya ndani (maji haba).

*Uvuvi mdogo* - Mashua ndogo, mashine ndogo, vifaa ambavyo ni nusu vya mashine au vyote ni vya mashine ambavyo vinafanya kuunganishwa na wahudumu, vibarua au wafanyakazi wa kudumu, zana za kutumia mashine au bila mashine, masoko ya ndani na nje, uvuvi katika bahari ya ndani (maji haba).

*Shughuli za kujipatia kipato cha kutwa* - wafanyikazi pekee, vikundi vya familia au vya kijamii, watumishi ni vibarua, mashua ndogo, zisizonguvu, zisizomashine, zana zinazounganishwa na mhudumu, bidhaa kwa matumizi ya nyumbani, uvuvi katika maji haba.

**Jinsi ya kuchambua takwimu**

Tengeneza muhtasari wa takwimu kutoka kwa mahojiano na uangalizi ili kukusanya orodha ya njia/mbinu zilizotumika katika eneo la uchunguzi. Andika habari hii ndani ya karatasi ya uchambuzi wa mahojiano/chanzo pili kama inavyoonyeshwa.

*Uchambuzi wa ziada:* Linganisha matokeo kwa kipindi fulani ili kuelezea mababiliko ya njia/mbinu. Linganisha mabadiliko katika aina ya matumizi na mabadiliko katika hali ya rasilimali na *viwango na aina za athari (K25)* ili kuona ikiwa njia/mbinu zinafungamana na hali na athari. Linganisha mabadiliko katika njia/mbinu na mabadiliko kwenye *makazi (S11)* na ona kama zina uhusiano.

## NGAZI YA KAYA: S14

**Jinsi ya kukusanya takwimu**

Mhojiwa anaulizwa kutambua njia/mbinu mahususi au maendeleo yanayotumika kwa kila aina ya bidhaa na huduma ya pwani na baharini. Habari hii inaandikwa ndani ya jedwali la *muongozo wa uchunguzi* kama inavyoonyeshwa.

| Shughuli ya Pwani na Baharini | Bidhaa na Huduma za Pwani na Baharini | Njia/mbinu |
|---|---|---|
| Uvuvi | Chewa | Mtego<br>Mshipi<br>Sumu |
| | Pweza | Mikuki (njoro)<br>Mishipi |
| | Kamba | Uvuvi wa kukokota |
| Utalii | Maendeleo ya hoteli | Nyumba za wageni (aina zote zimeunganishwa) |
| | Uzamiaji | Kutumia mitungi ya gesi |
| | Uvuvi wa michezo | Mashua ya watu 25 |

**Jinsi ya kuchambua takwimu**

Takwimu kutoka uchunguzi wa kaya zote zinachambuliwa na kuwekewa madaraja kulingana na umuhimu zaidi wa bidhaa na huduma za pwani na baharini kwa kila shughuli inayofanywa katika kaya. Bidhaa na huduma zilizotajwa mara nyingi zaidi na kaya lazima ziorodheshwe kwanza, zikifuatiwa na zile zilizotajwa zaidi kwa mara ya pili n.k. Habari hii inaandikwa ndani ya karatasi ya uchambuzi wa uchunguzi kama inavyoonyeshwa.

*Uchambuzi wa ziada*: Inaweza ikawa vizuri kuelezea bidhaa na huduma za pwani na baharini kwa kaya katika jamii kwa maelezo mafupi.

**Umuhimu wa habari hizi kwa wasimamizi na wadau wengine**

Habari juu ya njia/mbinu inatumika mahsusi kwa kuelezea madhara, kama vile ya ukataji mikoko, kwa rasilimali za pwani na baharini. Kwa kufuatilia habari hii kwa muda fulani, msimamizi anaweza pia kuona ni kwa jinsi gani njia/mbinu hizi zimeathiriwa na usimamizi uliopo. Kwa mfano, iwapo mpango wa usimamizi umeanzisha kampeni ya kupanda mikoko na bado ukataji wa mikoko unaendelea kuorodheshwa kama njia/mbinu, kwahivyo hii inaonyesha kwamba kampeni hiyo haizuii uendelezaji wa kukata mikoko. Habari hii inasaidia pia kuelezea umadhubuti wa mipango ya usimamizi.

Kuelewa njia/mbinu zipi zinafanyika katika eneo la uchunguzi ni muhimu sana kwa kujenga ushirika wa wadau na mpango wa uhamasishaji wa usimamizi wa pwani. Wasimamizi wanahitaji kufahamu jinsi watu wanavyofungamana na rasilimali ili wawe na uwezo wa kufanyakazi pamoja nao na kuwasiliana nao kuhusiana na athari kwenye rasilimali.

Habari hii itawawezesha wadau kuwa na taswira nzuri ya umuhimu wa njia mbalimbali zinazotumika katika eneo la mafunzo. Hii inaweza kusaidia kutatua mizozo inayohusiana na matumizi, kwa kuelewa kiwango cha masuala kwa mfano yanayosababishwa na zana maalum za kuvulia, migongano inaweza kutatuliwa na wadau wenyewe au kupendekeza kwa wasimamizi suluhisho juu ya jinsi ya kutatua baadhi ya masuala yanayoleta migongano.

## *K21. Thamani ya Bidhaa na Huduma*

**Ni nini**

Thamani ya bidhaa na huduma za pwani na baharini ni uhusiano na/au thamani halisi ya fedha kwa kila bidhaa katika soko.

**Jinsi ya kukusanya takwimu**

Takwimu juu ya thamani ya bidhaa ya pwani na baharini hupatikana kwa kuwahoji watoaji habari wakuu wenyeji kama vile wavuvi, wanunuzi, wafanyabiashara, waendesha mahoteli na waendeshao shughuli za uzamiaji. Wanaulizwa kuweka thamani (ya juu, ya kati au ya chini) kwa kila bidhaa na huduma ya pwani na baharini. Thamani ya juu, ya kati na ya chini itahitaji kuelezwa kwa uhalisi mwanzoni kabisa na timu ya uperembaji wa eneo la uchunguzi ili kuhakikisha uthabiti wa maitikio. Kwa mfano thamani ya juu inaweza kuwekwa kwenye kamba mti kama wanatakikana zaidi na wana thamani kubwa ya fedha katika soko la nchini na soko la kimataifa. Thamani ya kati inaweza kuwekwa kwa maendeleo ya hoteli endapo inahusu kiasi kidogo tu cha nyumba za wageni. Thamani ya chini inaweza kuwekwa kwa eneo la mikoko iliyokatwa ambalo halina uwezo wa kukaliwa na ndege na kwahivyo lina nafasi ndogo ya biashara za kitalii unaozingatia mazingira safi. Habari hii inaandikwa ndani ya jedwali la chanzo pili/ mwongozo wa mahojiano kama inavyoonyeshwa.

| Shughuli za Pwani na Baharini | Bidhaa na Huduma za Pwani na Baharini | Thamani ya Bidhaa na Huduma |
|---|---|---|
| Uvuvi | Kamba mti | Ya juu |
| | Chewa | Ya juu |
| Utalii | Hoteli | Kati |
| | Uzamiaji | Chini |
| Ufugaji viumbe baharini | Chaza | Kati |

**Jinsi ya kuchambua takwimu**

Fanya muhtasari wa takwimu kutoka kwa watoaji habari wakuu mbalimbali katika jedwali ndani ya karatasi ya uchambuzi wa mahojhiano/chanzo pili kama inavyoonyeshwa. Maana ya thamani ya juu, ya kati na ya chini lazima zionyeshwe.

*Uchambuzi wa ziada:* Inaweza kusaidia kutoa maelezo ya thamani ya bidhaa na huduma za pwani na baharini.

**Umuhimu wa habari hizi kwa wasimamizi na wadau wengine**

Thamani ya bidhaa na huduma za pwani na baharini ni muhimu kwa kuelezea athari kwa jumla ya usimamizi kwa jamii katika eneo la uchunguzi pamoja na maisha ya watu, masoko, uzalishaji na utoshelezi wa chakula. Kwa mfano, endapo mamlaka ya usimamizi yanaanza kuendeleza bidhaa kutoka kwenye chama cha ushirika wa ufugaji viumbe baharini kilichoanzishwa na mamlaka, basi itatazamiwa kwamba thamani ya bidhaa hizi itaongezeka kadiri mahitaji yatakavyoongezeka.

Thamani ya bidhaa na huduma za pwani na baharini ni muhimu pia kwa kuelezea umuhimu wa kusimamia eneo kwa matumizi endelevu. Kwa mfano, iwapo (upigaji mbizi) uzamiaji kwa kutumia mitungi ya gesi unaingiza kiasi kikubwa cha wageni toka nje na thamani kubwa kutokana na mahitaji makubwa ya vyumba, migahawa na waendeshaji wa shughuli za uzamiaji, msimamizi wa pwani ana sababu za kuweka juhudi za usimamizi katika kuhakikisha kwamba kuwepo kwa matumbawe na uvuvi katika eneo

kunakuwa endelevu. Tofauti na endapo matumbawe yamevunjwa na wavuvi wa mabomu na yanakuwa na thamani ndogo kwa shughuli za uzamiaji, msimamizi atakuwa na wakati mgumu kuelezea umuhimu wa matumbawe katika uzamiaji.

Thamani ya bidhaa na huduma za pwani ni muhimu pia kwa kuelezea ni rasilimali zipi ziko katika msongo mkubwa wa kuvunwa na zinaweza labda kuhitaji kuangaliwa kipekee na wasimamizi. Thamani ni kipimo cha umuhimu wa bidhaa. Kwa vile bei inashawishi tabia ya mwanadamu, msongo wa uvunaji unauwezekano wa kuwa na nguvu kubwa kwa bidhaa yenye thamani kubwa. Samaki mwenye thamani kubwa kwa mfano, atahitaji uangalizi mkubwa na jitihada katika uvuvi kuliko samaki mwenye thamani ndogo na kwahivyo atahitaji uangalizi maalum kutoka kwa msimamizi wa pwani.

Thamani ya bidhaa na huduma za pwani na baharini ni muhimu pia kwa kuelewa kiwango cha kipato cha kaya na hali yao ya maisha. Kama, kwa mfano, thamani ya bidhaa inabadilika kutoka kuwa ya juu hadi kuwa ya chini, basi kutatazamiwa kipato cha pesa na maisha ya watu kushuka.

## *K22&S15. Masoko lengwa ya Bidhaa na Huduma*

**Ni nini**

Masoko lengwa ya bidhaa na huduma ni utambulisho wa soko ambapo kila bidhaa kwa kawaida huuzwa.

### NGAZI YA KAYA: K22

**Jinsi ya kukusanya takwimu**

Takwimu juu ya masoko lengwa ya bidhaa na huduma za pwani na baharini hupatikana kwa kuwahoji watoaji habari wakuu wenyeji kama vile wavuvi, wanunuzi, wenye mahoteli na wanaoendesha shughuli za kuzamia. Hawa watoaji habari wakuu wanaweza kutumiwa kupata habari juu ya masoko ya msingi kwa kila bidhaa na huduma ya pwani na baharini.

| Shughuli za Pwani na Baharini | Bidhaa na Huduma za Pwani na Baharini | Soko lengwa la Bidhaa na Huduma (Ya msingi) |
|---|---|---|
| *Uvuvi* | *Kamba mti* | *Kimataifa* |
| | *Chewa* | *Kimkoa* |
| *Utalii* | *Hoteli* | *Kimataifa* |
| | *Uzamiaji* | *Kimataifa* |
| *Ufugaji viumbe baharini* | *Chaza* | *Kienyeji* |

Hawa watoaji habari wakuu wanaulizwa kuelezea masoko ya msingi ambapo kila bidhaa au huduma huuzwa (kimataifa, kitaifa, kimkoa au kienyeji). Matokeo ya habari hii inaandikwa ndani ya jedwali la mwongozo wa mahojiano/chanzo pili kama inavyoonyeshwa.

*Ukusanyaji wa takwimu za ziada*: Kwa njia nyengine, mtoaji habari mkuu anaulizwa kuorodhesha masoko yote kwa kila bidhaa au huduma na kuyawekea madaraja kulingana na ubora wa kila soko. Hii ni muhimu kwa kuelewa kiwango halisi cha masoko. Zaidi ya hayo, timu ya uperembaji inaweza kutaka kujua habari juu ya utaratibu wa ufanyaji biashara katika masoko. (kwa mfano, je samaki wanauzwa kwenye minada, kuwekewa bei na vyama vya ushirika n.k.) kwa kila aina ya bidhaa na huduma zinazotolewa.

**Jinsi ya kuchambua takwimu**

Fanya muhtasari wa takwimu kutoka kwa watoaji habari wakuu mbalimbali katika jedwali ndani ya karatasi ya uchambuzi wa mahojiano/chanzo pili kama inavyoonyeshwa.

*Uchambuzi wa ziada:* Inaweza ikawa muhimu kuelezea, kwa kuzingatia jedwali hilo hapo juu, soko kwa kila bidhaa au huduma. Chati ya mtiririko inaweza kuonyesha vizuri zaidi mtiririko wa bidhaa au huduma kutoka chanzo hadi sokoni.

### NGAZI YA KAYA: S15

**Jinsi ya kukusanya takwimu**

Kwa kila bidhaa na huduma ya pwani na baharini ambayo kaya inajihusisha nayo, mhojiwa anatakiwa kutambua soko la msingi ambako inauzwa (kimataifa, kitaifa, kimkoa au kienyeji). Maitikio yanaandikwa ndani ya jedwali la mwongozo wa uchunguzi kama inavyoonyeshwa. Timu ya uperembaji inahitaji kufafanua mwanzoni kabisa aina za mfumo wa masoko (Kimataifa, kitaifa, kimkoa au kienyeji) ili kuhakikisha uthabiti wa maitikio.

| Shughuli za Pwani na Baharini | Bidhaa na Huduma za Pwani na Baharini | Njia/mbinu | Soko lengwa |
|---|---|---|---|
| Uvuvi | Chewa | Mitego<br>Mshipi<br>Sumu | Kimkoa |
| | Pweza | Uvuvi wa kukokota<br>Mshipi | Kienyeji |
| | Kamba | Kukokota | Kimkoa |
| Utalii | Maendeleo ya hoteli | Nyumba za wageni mchanganyiko | Kimataifa |
| | Uzamiaji | Uzamiaji wa kutumia mitungi ya gesi | Kitaifa |
| | Uvuvi wa michezo | Mashua za watu 25 | Kienyeji |

**Jinsi ya kuchambua takwimu**

Orodhesha bidhaa na huduma halafu piga hesabu ya asilimia ya wahojiwa ambao wamesema kila bidhaa au huduma iliyouzwa kwenye masoko ya kimataifa, kitaifa, kimkoa au kienyeji. Habari hii iandikwe ndani ya karatasi ya uchambuzi wa uchunguzi kama inavyoonyeshwa. Maelezo kuhusu mfumo wa masoko (kimataifa, kitaifa, kimkoa, au kienyeji lazima yaandikwe.

| Bidhaa na Huduma za Pwani na Baharini | % Waliosema masoko ya kimataifa | % Waliosema masoko ya kitaifa | % Waliosema soko la kimkoa | % Waliosema soko la kienyeji |
|---|---|---|---|---|
| Chewa | 0% | 30% | 40% | 30% |
| Pweza | 0% | 15% | 35% | 50% |
| Kamba | 20% | 20% | 35% | 35% |
| Maendeleo ya | 60% | 35% | 3% | 2% |
| hoteli Uzamiaji | 50% | 40% | 8% | 2% |
| Uvuvi wa michezo | 10% | 10% | 30% | 50% |

*Uchambuzi wa ziada:* Inaweza kufaa kuelezea kwa kifupi masoko tofauti tofauti ambapo bidhaa na huduma huuzwa

**Umuhimu wa habari hizi kwa wasimamizi na wadau wengine**

Habari kuhusu masoko lengwa ni ya manufaa kwa kuelezea athari kwa jumla za usimamizi kwa jamii, hususan uuzaji wa bidhaa, uzalishaji na upatikanaji wa vyakula. Kwa mfano, uwekezaji katika miundombinu ya jamii, kama vile barabara kuelekea miji mikuu, inaweza kupelekea kufikika zaidi kwenye masoko ya kitaifa, kimkoa na kimataifa.

Kwa vile kipato na maisha ya watu katika jamii yanauhusiano na masoko, mfumo wa soko la samaki ni muhimu kwa vile unatoa ufahamu wa wapi bidhaa za baharini zitokazo katika eneo zinauzwa. Kigezo hiki kina ruhusu uchambuzi wa mabadiliko kwa muda fulani katika masoko ya bidhaa kuu za baharini. Inaonyesha uhusiano wa wazalishaji wenyeji na wafanyibiashara pamoja na masoko mbalimbali, kwa mfano ufangamano wa masoko ya kimataifa ambayo yanaweza kuathiri shughuli za uvunaji.

Masoko yaliyolengwa yanaweza pia kufaa kama kiashiria cha kiwango cha msongo uliowekwa kwenye rasilimali. Kwa mfano, wavuvi wanaweza kuongeza juhudi katika uvuvi wa samaki wa thamani kubwa kwa ajili ya masoko ya kimataifa. Inaweza pia kuonyesha kwa kipindi fulani juu ya mabadiliko ya masoko kwa bidhaa za baharini. Athari ya hatua za usimamizi inaweza kukadiriwa kwa kuona mabadiliko katika masoko. Kwa mfano, mikakati ya usimamizi inaweza kusababisha kuwepo samaki wa thamani kubwa ambao wanaweza kuuzwa katika masoko ya kitaifa, au kimkoa katika eneo husika.

Kufahamu vyema ufungamano wao na masoko mbalimbali kutawapatia wadau habari bayana za mabadiliko katika nafasi za biashara.

## *K23. Utaratibu wa matumizi*

**Ni nini**
Utaratibu wa matumizi unahusika na sehemu na nyakati za shughuli za pwani na baharini.

**Jinsi ya kukusanya takwimu**

| Shughuli za Pwani na Baharini | Bidhaa na Huduma za Pwani na Baharini | Njia/Mbinu ya (msingi) | Eneo | Wakati | Majira |
|---|---|---|---|---|---|
| Uvuvi | Kamba mti | Mtego | Ghuba | Maji mafu | yote |
| | Chewa | Mishipi | Miamba | Maji mafu | Majira 1 |
| | Pweza | Mikuki | Miamba | Bamvua dogo | yote |
| Utalii | Hoteli | Nyumba ya wageni ya vyumba (1 – 7) | Pwani | | Majira 2 |
| | Uzamiaji | Uzamiaji wa kutumia mitungi ya gesi | Miamba | Maji mafu | Majira 2 |
| Ufugaji wa viumbe baharini | Chaza | Mshipi | Ghuba | | |

Takwimu juu ya taratibu za matumizi zinakusanywa kwanza kutoka kwa vyazo pili, ikiwa ni pamoja na ofisi za jamii na za mijini, ambazo zinaweza kuwa na ramani zinazoonyesha sehemu za shughuli mbalimbali katika eneo hilo. (kwa mfano, ramani ya maeneo ya kilimo, utafiti wa uvuvi unaoonyesha maeneo ya kuvulia). Baadaye, uhojaji kwa watoaji habari wakuu unafanywa pamoja na wawakilishi wa shughuli mbalimbali (kwa mfano, mkuu wa chama cha wenye hoteli, mwenyekiti wa wauzaji samaki). Utaratibu wa kutumia uchoraji ramani shirikishi unaweza pia kutumiwa (angalia *Mwongozo wa GCRMN, Sura ya 3: Ukusanyaji wa takwimu, mbinu ya kuleta ufahamu kutumia picha/michoro, ramani*). Hatimaye, uangalizi unatumika kuelezea na kuhakiki taratibu za matumizi.

Habari inakusanywa juu ya eneo na wakati/majira ya kila shughuli kulingana na bidhaa au huduma na zinaandikwa ndani ya jedwali la chanzo pili/ mwongozo wa mahojiano kama inavyoonyeshwa.

*Ukusanyaji wa takwimu za ziada:* Timu ya uperembaji inaweza kuweka kumbukumbu za maeneo ya shughuli mbalimbali katika ramani ya msingi, ambayo itatoa habari zaidi juu ya maeneo kuliko kuonyesha tu miamba na ghuba. Timu pia inaweza kuuliza kuhusu mabadiliko katika taratibu za matumizi kwa mwaka mzima na sababu za mabadiliko hayo.

**Jinsi ya kuchambua takwimu**
Elezea sehemu za shughuli ambazo umezipata kutoka kwa watoaji habari wakuu na vyanzo pili. Ziandike ndani ya karatasi ya uchambuzi wa mahojiano /chanzo pili kama inavyoonyeshwa.

*Uchambuzi wa ziada:* Kwa kulinganisha maeneo ya shughuli mbalimbali, timu ya uperembaji inaweza kuona maeneo yanayoingiliana na hivyo kuwepo na uwezekano wa kusababisha migongano. Linganisha maeneo kwa kipindi fulani kuona jinsi utaratibu wa matumizi unavyobadilika. Maelezo mafupi yanaweza kuandaliwa kuelezea shughuli, maeneo yanayotumika, na jinsi yalivyobadilika kwa kipindi fulani.

**Umuhimu wa habari hizi kwa wasimamizi na wadau wengine**
Sawa na *njia/mbinu (K20)*, habari juu ya taratibu za matumizi ni muhimu kwa kuelezea athari kwa rasilimali za pwani na baharini. Kwa kuelewa maeneo shughuli zinapofanyika, msimamizi anaweza kwa vizuri zaidi kukisia athari. Kwa mfano, kama maendeleo ya hoteli yanatokea karibu na miamba ya matumbawe, kuna uwezekano mkubwa wa kutokea athari kutoka kwa mabaki ya maji taka yanayotiririka. Kiasi cha eneo pia ni kiashiria cha kiwango cha athari. Hii ni hususan muhimu kwa vile habari kuhusu *njia/mbinu* zinawezesha kuelewa shughuli zinazoendelea lakini siyo kwa kiasi gani.

Kwa kufanya uperembaji wa habari hii kwa muda fulani, msimamizi anaweza pia kuona athari iliyosababishwa na shughuli za usimamizi. Kwa mfano, kama mpango wa usimamizi wa pwani umeanzisha kampeni ya upandaji mikoko na bado ukataji wa mikoko unaendelea kuandikwa kama shughuli, msimamizi anaweza kuangalia ukubwa wa eneo linalokatwa na kuona endapo limeongezeka, limepungua, au limebaki kama lilivyokuwa miaka iliyotangulia. Kama limepungua, basi mpango ulioanzishwa wa usimamizi umekuwa na mafanikio. Habari hii pia inasaidia kuelezea mafanikio ya mipango ya usimamizi wa pwani.

Hatimaye, kwa kuweka ramani ya taratibu za matumizi, wasimamizi wanaweza kwa uzuri zaidi kuelewa matatizo hususan migogoro juu ya upatikanaji wa rasilimali na matumizi yanayofanana miongoni mwa makundi ya wadau. Hii inaweza kusaidia kuelezea endapo hatua, kama vile kutenga sehemu za shughuli ni sahihi kwa eneo hilo.

Kwa kufahamu vizuri taratibu za matumizi na tabia za kipekee za maeneo ambako shughuli zinafanyika, wadau watafahamu athari zao kwa mazingira ya pwani na mwelekeo wa biashara zao hapo baadaye. Wadau wanaweza kuchangia vizuri zaidi kwenye maamuzi ya usimamizi katika ulinzi wa maeneo nyeti.

## *K24. Kiwango cha Matumizi kwa Watu wa Nje*

**Ni nini**

Kiwango cha matumizi kwa watu wa nje inahusu idadi ya watu wa nje wanaotumia rasilimali za pwani ikilinganishwa na idadi ya wenyeji wanaotumia rasilimali hizo katika eneo la uchunguzi. Kwa mfano, kama kuna wavuvi wa nje 1000 na wavuvi wenyeji kumi tu, kwahivyo kiwango cha matumizi cha watu wa nje kiko juu zaidi. Watu wa nje ni watu ambao si wakazi wa eneo la uchunguzi (au wanaishi katika eneo kwa misingi ya majira yaani wanakuja kwa vipindi). Wanaweza wakawa wanatoka jamii jirani au kutoka nchi jirani.

**Jinsi ya kukusanya takwimu**

Hii habari inapatikana kwa kufanya mahojiano na watoaji habari wakuu, kama vile viongozi wa jamii na maafisa wa miji pamoja na wawakilishi kutoka makundi ya wadau mbalimbali.

| Shughuli za pwani na baharini | Bidhaa na huduma za pwani na baharini | Njia/mbinu (Msingi) | Kiwango cha matumizi ya watu wa nje |
|---|---|---|---|
| Uvuvi | Kamba mti | Mtego | Chini (C) |
| | Chewa | Mishipi | Chini (C) |
| Utalii | Hoteli | Nyumba za wageni zenye vitanda (1 – 7) | Juu (J) |
| | Uzamiaji | Uzamiaji wa kutumia mitungi ya gesi | Juu (J) |
| Ufugaji wa viumbe baharini | Chaza | Mshipi | Kati (K) |

Watoaji habari wakuu wanaulizwa kiwango cha sasa cha matumizi ya watu wa nje kwa kila shughuli ya pwani na baharini kwa utaratibu wa kutumia kipimo cha juu, kati na chini. Kipimo hicho kitahitaji kutolewa maelezo kwa kila eneo la uchunguzi, lakini kiwango cha juu kinaweza kuwa na maana ya matumizi makubwa kwa watu wa nje, kama vile idadi ya juu ya uvuvi unaofanyika katika eneo la uchunguzi hufanywa na watu wa nje, kati ikiwa na maana ya matumizi ya kadiri kufanywa na watu wa nje, kama vile watalii wachache wa kimataifa, na chini inaweza kuwa na maana ya matumizi madogo yanafanywa na watu wa nje, kama vile nyumba ya wageni moja kati ya ishirini zilizopo katika eneo la uchunguzi inamilikiwa na mgeni. Kiwango cha matumuzi (cha juu, cha kati, na cha chini) kitahitaji kitolewe maelezo maalum mapema na timu ya uchunguzi ili kuhakikisha kwamba kunakuwa na uthabiti wa maitikio. Majibu yanaandikwa ndani ya jedwali la chanzo pili/mwongozo wa mahojiano kama inavyoonyeshwa. Angalia pia *umiliki wa biashara (K16).*

*Ukusanyaji wa takwimu za ziada*: Watoaji habari wakuu wanaweza kuulizwa kutambua wanakotoka watu wa nje.

**Jinsi ya kuchambua takwimu**

Unganisha takwimu kutoka kwa watoaji habari wakuu ili kuamua kiwango cha matumizi ya watu wa nje kwa kila shughuli na ingiza katika jedwali ndani ya karatasi ya uchambuzi wa mahojiano /chanzo pili kama inavyoonyeshwa. Maana ya juu, kati na chini lazima zielezwe.

*Uchambuzi wa takwimu za ziada:* Linganisha viwango hivi kwa kipindi fulani. Inaweza kuwa muhimu kutoa maelezo juu ya kiasi cha matumizi ya watu wa nje na jinsi kilivyobadilika kwa kipindi fulani. Linganisha habari hii na habari kutoka ngazi ya kaya juu ya makazi. Itakuwa pia ni muhimu kulinganisha na *kiwango cha uhamiaji (K6)* na *hali ya makazi (S11).*

**Umuhimu wa habari hizi kwa wasimamizi na wadau wengine**

Habari juu ya viwango vya matumizi ya watu wa nje ni muhimu kwa kuanzisha ushirika wa wadau na mipango ya uhamasishaji. Watu ambao si wakazi, mara nyingi husahauliwa kwasababu hawaonekani kwa urahisi. Kwa kuelewa idadi ya watu wanaokuja kutoka maeneo mengine, wasimamizi wanaweza wakaona umuhimu wa kujenga uhusiano na watu kutoka nje ya jamii. Iwapo msimamizi

anafahamu wapi wanakotoka watu wa nje, anaweza akalenga maeneo hayo. Katika hali ambazo kuna watumiaji kutoka nje ya nchi (kwa mfano, vyombo vya uvuvi vya nje), msimamizi anaweza kuamua kufanya kazi kupitia ofisi za forodha na uhamiaji. Katika hali zingine inaweza kuwa ni hali tu ya kupanua mipango ya elimu ili kuzifikia jamii jirani.

Matumizi ya watu wa nje pia ni muhimu kwa kufahamu matatizo ya usimamizi wa pwani. Kwa mfano, ongezeko la idadi ya wageni toka nje linaweza kuwa chanzo cha migongano katika jamii.

Habari hii inaweza pia kuwa muhimu kwa kugundua thamani na umuhimu wa rasilimali. Kama watu kutoka nje ya eneo la uchunguzi wanatumia rasilimali, basi hii inaonyesha kwamba rasilimali hizo ni muhimu kwa sehemu kubwa kuliko jamii iliyo karibu. Hii inaweza kuwa muhimu kwa kuwapa taarifa wanasiasa na wananchi kwa jumla juu ya sababu za kuhitaji kufanya usimamizi wa rasilimali.

## *K25. Viwango na Aina za Athari*

**Ni nini**

Kwa pamoja, hiki ni kipimo cha fikra za watu na aina za athari za shughuli za pwani na baharini juu ya rasilimali za pwani na baharini. Haya sio makadirio ya kisayansi ya viwango na aina za athari, bali ni orodha tu juu ya fikra za watu.

| Shughuli za Pwani na Baharini | Bidhaa na huduma za Pwani na Baharini | Njia/Mbinu (za msingi) | Kiwango cha athari | Aina athari (kuu) |
|---|---|---|---|---|
| Uvuvi | Kamba mti | Mtego | Chini | Uvuvi wa kupindukia |
| | Chewa | Mshipi | Kati | Uvuvi wa kupindukia |
| Utalii | Hoteli | Nyumba za wageni (vyumba 1-7) | Kati | Uchafuzi wa mazingira |
| | Uzamiaji | Uzamiaji kwa kutumia mitungi ya gesi | Chini | Uharibifu kutokana na nanga |
| Ufugaji wa viumbe baharini | Chaza | Mshipi | Chini | Virutubisho |

**Jinsi ya kukusanya takwimu**

Takwimu hukusanywa kwa kuwahoji watoa habari wakuu au vikundi maalum vya wahojiwa ambapo huweza kujumuisha viongozi wa jamii na maofisaa, watu ambao wameishi katika jamii hiyo kwa miaka mingi na watu wengine ambao wanaweza kutoa maoni kwa niaba ya jamii.

Watoa habari wakuu wanaulizwa kutambua, kutumia vipimo vya juu/ kati/ chini/ hakuna, kiwango cha athari kwa kila shughuli ya pwani na baharini kulengana na bidhaa na huduma. Japo vitabidi vibadilishwe kwa kila eneo la uchunguzi, kiwango cha juu kinaweza kumaanisha athari nzito juu ya rasilimali isiyoweza kurekebishika, kama vile ukataji na uharibifu wa maeneo ya mikoko; kiwango cha kati kinaweza kumaanisha athari za wastani juu ya rasilimali, kama vile ukataji wa mikoko; na kiwango cha chini kinaweza kumaanisha madhara madogo madogo juu ya rasilimali, kama vile asilimia ndogo ya maeneo ya mikoko kuingiliwa; na hakuna inaweza kumaanisha kuwa hakuna athari. Viwango vya athari (Juu, Kati, Chini) vinahitaji kutolewa maelezo halisi na timu ya uchunguzi wa eneo hilo ili kuhakikisha uthabiti wa maitikio.

Aina kuu za athari zinaweza kuelezwa kwa ufupi. Kwa mfano, ikiwa maendeleo ya hoteli yanasababisha uharibifu au uchafuzi wa mazingira, basi uchafuzi huo ukaelezwa. Matokeo ya habari hizi yaandikwe katika jedwali la *chanzo pili/mwongozo wa mahojiano* kama ilivyoonyeshwa.

*Ukusanyaji wa takwimu za ziada*: Aina za athari zinaweza kuelezwa kwa undani zaidi ili kubainisha athari za moja kwa moja na zile zisizokuwa za moja kwa moja. Kwa mfano, umwagaji wa maji machafu una athiri moja kwa moja na ubora wa maji, na pia kilimo cha sehemu za miinuko huweza kusababisha chengachenga za mchanga hasa majira ya mvua.

**Jinsi ya kuchambua takwimu**

Takwimu zinafanyiwa muhtasari ili kuonyesha kwa ujumla viwango na aina za athari na kuziingiza ndani ya jedwali katika karatasi ya *uchambuzi wa mahojiano/chanzo pili* kama ilivyoonyeshwa. Maana ya viwango vya athari (Juu, Kati, na Chini) lazima zielezwe.

*Uchambuzi wa ziada*: Matokeo haya yanalinganishwa na matokeo kutoka miaka iliyopita ili kubaini mabadiliko katika viwango na aina za athari. Mabadiliko hayo yanalinganishwa na hali ya rasilimali ili kuona kama kuna uhusiano.

Takwimu zinazofanana na hizi zinakusanywa kama sehemu ya uchunguzi ambapo watu wanaulizwa wataje athari tano wanazofikiria

ndizo kuu kwa rasilimali za pwani na baharini. Mlingano kati ya matokeo unaruhusu kuhakikisha kwa usahihi wa takwimu. Shughuli zilizobainishwa na watu zinatakiwa zionyeshwe juu ya jedwali lililojazwa na watoaji habari maalum. Kama kuna tofauti kubwa sana baina ya matokeo, basi watoaji bahari maalum lazima waulizwe ili waeleze kwa uwazi. Sensa kamili ya uchunguzi inaweza kuwa muhimu ili kueleza kwa usahihi fikra za watu.

**Umuhimu wa habari hizi kwa wasimamizi na wadau wengine**

Sawa na *njia/mbinu (K20) na utaratibu wa matumizi (K23)*, habari kuhusu viwango na aina za athari inatumika sana hasa katika kuonyesha athari kwa rasilimali za pwani. Wanajamii, hasa wale watu wanaotumia moja kwa moja rasilimali, mara nyingi ndio walio na ufahamu mwingi kuhusu mambo yanayoathiri rasilimali wanazotumia kwa kawaida. Habari hii inaweza kuwa ya umuhimu kwa kutambua matumizi yanayohitaji uchunguzi wa kisayansi. Kwa mfano, wanajamii wanaweza kuona umwagikaji mafuta na gesi kuwa na athari ya juu kwa sababu wameona kwa uhakika umwagikaji kidogo. Athari hii inaweza kuachwa na uchunguzi wa kisayansi unaofanyika mara moja kwa mwaka.

Kwa kufuatilia habari hii kwa kipindi fulani, msimamizi anaweza kuona athari zinazotokana na usimamizi kwa shughuli hizi na kwa hivyo kuona mafanikio ya usimamizi. Kwa mfano, kama mpango wa usimamizi wa pwani ulianzisha mpango wa kupunguza matumizi ya dawa za wadudu na kemikali nyengine za kilimo katika sehemu za miinuko, na kama bado haya yanaendelea kutambuliwa kama aina ya athari, basi hii inatoa fikra kwamba pengine mpango huo wa usimamizi haukufanikiwa.

Hatimaye habari hizi ni za umuhimu sana kwa kuanzisha mipango ya uhamasishaji na kutafuta kuwashirikisha wadau. Kama wanajamii hawatilii maanani kuwepo kwa athari juu ya rasilimali za pwani, basi itakuwa vigumu kuwahusisha katika usimamizi wa pwani. Kama wanajamii wanachukulia shughuli moja au mbili tu kuwa ndizo zinazoathiri rasilimali, ilhali utafiti wa kisayansi unadhihirisha ya kuwa kuna athari nyengine, basi mpango wa uhamasishaji unahitajika kuanzishwa ili kuongezea ufahamu wa shughuli zote zinazoathiri rasilimali.

## *K26&S16. Matumizi ya Bidhaa na Huduma*

**Ni nini**

Kigezo hiki ni muafaka zaidi kwa shughuli zinazoondoa bidhaa (kwa mfano, uvuvi, ufugaji wa viumbe baharini).

### NGAZI YA JAMII: K26

**Jinsi ya kukusanya takwimu**

Takwimu juu ya matumizi ya bidhaa na huduma za pwani na baharini katika kaya zinapatikana kwa kuwahoji watoa habari wakuu, kama vile maofisaa wa jamii na wafanyabiashara. Watoa habari maluum wanaulizwa kutambua na kuwekea madaraja matumizi ya jumla ya kila bidhaa na huduma. Wanaulizwa kama raslimali ni kwa ajili ya matumizi kibinafsi, starehe au kuuza. Mtu binafsi au 'matumizi binafsi' inamaanisha matumizi katika kaya, kama vile samaki kwa ajili ya chakula; kustarehe kunamaanisha mchezo/tafrija, na kuuza kunamaanisha kuuza kwa kupata fedha au kufanya mabadilishano ya bidhaa. Maitikio haya yanaandikwa katika jedwali la Chanzo pili/ mwongozo wa mahojiano kama inavyoonyeshwa.

| Shughuli za Pwani na Baharini | Bidhaa za Pwani na Baharini | Matumizi ya Kaya (ya msingi) |
|---|---|---|
| Uvuvi | Kambamawe | Mauzo |
| | Chewa | Matumizi binafsi |
| Utalii | Hoteli | Mauzo |
| | Uzamiaji | Mauzo |
| Ufugaji viumbe baharini | Chaza | Mauzo |

*Ukusanyaji wa takwimu za ziada:* Kama upatikanaji wa chakula ni shida, basi wahojiwa maluum wanaweza kuulizwa maswali yanayohusiana na upatikanaji wa chakula kama vile iwapo kuna vyakula mbalimbali vinavyouzwa ndani ya mwaka mzima, na kama bidhaa za baharini zinazovuliwa hapo zinapatika kwa bei rahisi.

**Jinsi ya kuchambua takwimu**

Fanya muhtasari wa takwimu kutoka kwa wahojiwa mbalimbali ndani ya jedwali katika *karatasi ya uchambuzi wa mahojiano/chanzo pili* kama inavyoonyeshwa.

*Uchambuzi wa ziada:* Takwimu kama hizi zinakusanywa kama sehemu ya uchunguzi. Kulinganisha kati ya matokeo kunaruhusu kufanya uhakiki wa takwimu. Kama kuna tofauti kati ya matokeo, basi ingekuwa vyema kuwaona wahojiwa maluum ili kuelezea sababu za tofauti hizi. Lau sivyo, uchunguzi kamili (mahojiano kwa kaya zote na si sampuli tu) lazima ufanyike ili kuelewa kwa usahihi idadi ya watu katika eneo la uchunguzi).

## NGAZI YA KAYA: S16

### Jinsi ya kukusanya takwimu

Kila mhojiwa anaulizwa koorodhesha matumizi muhimu ya kaya kwa kila bidhaa ua huduma.

| Shughuli za Pwani na Baharini | Bidhaa na Huduma za Pwani na Baharini | Matumizi ya Kaya |
|---|---|---|
| Uvuvi | Chewa | Matumizi binafsi |
| | Pweza | Mauzo |
| | Kamba | Mauzo |
| Utalii | Maendeleo ya mahoteli | Mauzo |
| | Uzamiaji | Mauzo |
| | Uvuvi wa michezo | Shughuli ya mchezo |

*Ukusanyaji wa takwimu za ziada*: Kama upatikanaji wa wa chakula ni jambo la kushughulikiwa, basi wahojiwa wanaweza kuulizwa maswali yanayohusu upatikanaji wa chakula. Wahojiwa wanaweza kuulizwa kuwekea madaraja vyanzo vya vyakula vyenye protini kulingana na bei (kwa mfano, bei ya chini kwa kilo=1) na uone jinsi samaki na bidhaa nyengine muhimu zinazopatikana zinavyotumika katika madaraja ya kaya. Wahojiwa pia wanaweza kuulizwa ni mara ngapi kwa wiki au kwa mwezi wanatumia bidhaa zitokanazo na bahari kama vile samaki ikilinganishwa na vyanzo vyengine vya kawaida vya protini (mfano, nyama ya ng'ombe na mbuzi). Umajira wa shughuli za baharini lazima uzingatiwe wakati wa kuchunguza bei za bidhaa za pwani na matumizi yake. Maswali kuhusu upatikanaji wa bidhaa za baharini zinazotumika katika kaya kwa mwaka mzima yanaweza pia kuulizwa, hasa kama ni vyanzo rahisi vya protini.

### Jinsi ya kuchambua takwimu

Sawa na kigezo cha mpangilio wa soko katika kaya, orodhesha bidhaa na huduma na upige hesabu ya nambari na asilimia ya wahojiwa ambao walisema kwa kila bidhaa na huduma ni kwa matumizi binafsi, michezo au mauzo. Habari hizi zinaandikwa katika karatasi ya uchambuzi wa uchunguzi.

Kama maswali juu ya wingi wa matumizi ya bidhaa za baharini yanaulizwa, weka maitikio katika makundi muafaka kwa mara za matumizi (kwa mfano, zaidi ya mara tatu kwa wiki, chini ya mara tatu kwa wiki, mara moja au mbili kwa mwezi, chini ya mara moja kwa mwezi lakini kwa kawaida, katika hafla maalum, hapana kamwe). Fanya hivyo hivyo pia katika vyanzo vyengine vya protini. Baada ya hapo fanya mahesabu ya asilimia za kaya katika kila kundi la aina mbalimbali za vyanzo vya protini vinavyochunguzwa. Linganisha wingi wa matumizi ya nyama ya kawaida na samaki.

Angalia mabadiliko kulengana na wakati. Linganisha mabadiliko ya wingi wa matumizi ya samaki na vyanzo vyengine vya protini dhidi ya hali halisi ya *maisha ya watu katika jamii (S29)* na uone ikiwa kuna uhusiano.

*Uchambuzi wa ziada*: Inaweza kuwa ya manufaa kutoa maelezo juu ya matumizi mbali mbali ya huduma na bidhaa za pwani na baharini katika kaya na jamii na vyanzo mbalimbali vya protini na bei zake katika kiwango cha jamii.

### Umuhimu wa habari hizi kwa wasimamizi na wadau wengine

Habari juu ya matumizi katika kaya ya bidhaa na huduma za pwani na baharini zinatoa ufahamu juu ya utegemezi wa kaya katika rasilimali za pwani na baharini kwa chakula na kipato. Ni muhimu kwahivyo kuelewa masuala ya upatikanaji wa chakula kwa kaya. Habari hii inaweza kutumika kuelewa jinsi mikakati ya usimamizi inavyoweza kuathiri maishilio ya uchumi wa watumizi wa rasilimali na upatikanaji wa chakula katika kaya. Kwa mfano, kama kaya kwa kawaida hutumia kama chakula samaki waliovua, basi matumizi haya yanaweza kuongeza ufahamu wa wasimamizi juu ya utegemezi wa rasilimalia za pwani na jamii nzima.

Kuelewa vyema utegemezi wao wa rasilimali za pwani na baharini kwa ajili ya maishilio (uchumi) na upatikanaji wa chakula, wadau wataweza kusaidia wasimamizi kubuni shughuli nzuri za usimamizi zitakazoweka maanani kiwango cha utegemezi wa rasilimali za pwani.

## *K27. Umbo la Utalii*

**Ni nini**

Umbo la utalii inahusu sifa za watalii wanaotembelea eneo la uchunguzi. Watalii wanaweza kuwa wa kitaifa au kutoka nchi nyengine.

**Jinsi ya kukusanya takwimu**

Takwimu za watalii zinakusanywa katika kiwango cha eneo la uchunguzi. Takwimu za watalii zinaweza kukusanywa kutoka vyanzo mbalimbali, kama vile bodi ya kitaifa ya utalii, bodi za mtaa za utalii, idara ya uhamiaji, afisi ya hesabu za watu, mashirika yasiyo ya kiserikali, biashara (mfano, mahotelini), na sehemu zenye vivutio vya watalii (mfano, sehemu tengefu za baharini, mbuga za kitaifa za wanyama). Nchi nyingi zitachangamanisha takwimu za utalii na safari, na kuziwasilisha kama taarifa. Takwimu za ziada zinaweza kupatikana kutoka kwa watoa habari maalum kama vile mkurugenzi wa bodi ya utalii, mkurugenzi muuzaji wa hoteli na watoaji huduma za usafirishaji wa watalii.

Maswali ya kuuliza ni:

Ni wageni wangapi kwa jumla waliopo kwa mwaka? _________

Ni watalii wangapi hutembea kutoka nchi zifuatazo?

(nchi hii)__________; (andika jina la nchi)______; (andika jina la nchi)_____

(andika jina la nchi)_______ ;(andika jina la nchi)________

Ni watalii wangapi hutembea miezi ifuatayo?

Januari___; Februari_____; Machi _____; Aprili_______; Mei_____; Juni _____

Julai _____; Agosti_____; Septemba_____;Octoba ______Novemba_______; Disemba_____.

Ni watalii wangapi hufika kwa kutumia njia zifuatazo za usafiri?

Usafiri wa anga ______; usafiri wa barabara ______; usafiri kwa meli______; na njia nyenginezo _______

Ni asilimia ngapi ya watalii walio katika umri wa miaka ifuatayo.? 0-18______; 19-30_______; 31-50_______; zaidi ya 50 ______

Ni asilimia ngapi ya watalii ni wanaume ua wanawake? Wanaume________; wanawake______;

Ni asilimia ngapi ya watalii wanavutiwa na mambo yafuatayo?

Maumbile ya asili______; ufukwe_______; kuogelea/kuzamia _______; uvuvi ______; utamaduni _____; nyenginezo________;

*Ukusanyaji wa takwimu za ziada:* Timu ya uperembaji inaweza kutaka kukusanya takwimu katika kiwango cha kitaifa kwa ajili ya ulinganisho. Takwimu za ziada zinaweza kukusanywa kama vile wastani wa kipindi cha kukaa, matumizi wastani ya kila siku, pahali palipo kusudiwa kufikwa na aina za malazi.

**Jinsi ya kuchambua takwimu**

Nyingi ya takwimu hizi huenda zikawa zimeshafanyiwa uchambuzi tayari na kupatikana katika taarifa za mwaka. *Karatasi ya uchambuzi wa mahojiano /chanzo pili* inatoa taswira ya utalii katika eneo la uchunguzi.

*Uchambuzi wa ziada*: Kama takwimu za utalii kulengana na wakati zipo, mwendo na mabadiliko ya tabia za utalii katika eneo la uchunguzi zinaweza kuchambuliwa .

**Umuhimu wa habari hizi kwa wasimamizi na wadau wengine**

Taswira ya utalii ni muhimu kwa wasimamizi ili kuelewa athari na nafasi zitokanazo na utalii, kama vile kiwango cha msongo juu ya rasilimali za pwani na baharini. Habari kuhusu mabadiliko katika muda fulani zinaweza kutumiwa katika kuyakinisha ikiwa msongo unazidi, unapungua, au kama unabakia vilevile. Mlinganisho na vigezo shughuli (K18), utaratibu wa matumizi (K23), na viwango na aina za athari (K25) unaweza kufaa katika kuelezea jinsi mabadiliko yanavyoathiri hali halisi ya rasilimali. Pia, ingekuwa muhimu kwa

wasimamizi kufanya maamuzi katika shughuli nyenginezo zinazohusiana na rasilimali ikiwa utalii unazorota na jamii inapoteza faida zitokanazo na shughuli za kitalii.

Takwimu zinazohusiana na idadi ya watu (umri, utaifa, jinsia) inaweza kuashiria utofauti wa mahitaji kwa bidhaa na huduma za kitalii. Kwa mfano, vijana wanauwezekano kuwa wakakamavu kuliko watalii wazee, na kwa hivyo uwezekano wa kuweka msongo mkubwa kwa rasilimali. Sawa na hayo, kufahamu vivutio vya watalii pamoja na majira pia ni muhimu kwa kutabiria ni rasilimali zipi zitakuwa na msongo mkubwa wakati gani.

Kufahamu vyema vivutio vya watalii pia kutasaidia wadau kubadilisha biashara zao kulengana na mahitaji. Itakuwa pia fursa kwa wasimamizi, wanaoelekeza watalii, wanaoelekeza uvuvi n.k, kufanya kazi kwa pamoja na kubuni mikakati kabambe ya kupunguza msongo wa rasilimali na kuwahamasisha watalii juu ya masuala yanayohusiana na mazingira ya pwani na baharini ya eneo hilo.

## UTAWALA

### *K28. Bodi ya Usimamizi*

**Ni nini**

Bodi ya usimamizi ni taasisi inayoangalia/simamia namna usimamizi wa rasilimali za pwani unavyofanyika na kuhakikisha kuna uwazi katika mchakato wa upangaji, uundaji na utekelezaji wa sheria na kanuni. Bodi za usimamizi zinaweza kuwa serikali, mashirika yasiyo ya kiserikali au mashirika ya kijamii, na zinaweza kufanya kazi katika ngazi ya kimataifa, kitaifa, kimkoa, kiwilaya au ngazi ya vijiji. Kunaweza kuwapo kwa bodi nyengine za usimamizi katika eneo la uchnguzi kwa shughuli mbalimbali za pwani kama vile usimamizi wa ukanda wa pwani, uvuvi, ufugaji wa viumbe baharini, mikoko, utalii, usafirishaji baharini na maendeleo ya makazi.

**Jinsi ya kukusanya takwimu**

Habari za bodi za usimamizi zinaweza kupatikana kwa kusoma mipango ya usimamizi ya shughuli mbalimbali. Habari hii pia inaweza kupatikana kwa kuwahoji watoa habari maalum wenye ufahamu mwingi juu ya usimamizi wa rasilimali za pwani au shughuli za pwani (kwa mfano, wawakilishi wa taasisi za serikali, viongozi wa kuchaguliwa, wawakilishi wa mashirika yasiyo ya kiserikali). Ni muhimu kuthibitisha kuwepo na jina la kila bodi ya usimamizi kwa kila shughuli ya pwani kwa kutambua na kumhoji mtu anayehusika na ufanyikazi wa bodi hiyo ya usimamizi. Habari kuhusu ikiwa bodi ya usimamizi ipo (ndiyo au hapana) na jina la bodi ya usimamizi zinaandikwa katika jedwali la chanzo pili/mwongozo wa mahojiano kama inavyoonyeshwa.

| Shughuli za Pwani* | Bodi ya Usimamizi (Ndiyo/Hapana) na Jina |
|---|---|
| Uvuvi | N – Idara ya Uvuvi |
| Utalii | N – Mamlaka ya Utalii |
| Ufugaji wa viumbe baharini | H |

**Orodhesha kulingana na shughuli zilizotambuliwa katika shughuli (K18)*

*Ukusanyaji wa takwimu za ziada*: Watoa habari maalum wanaweza pia kuulizwa kutambua mamlaka ya viongozi wakuu wa kila bodi ya usimamizi kwa kila shughuli ya pwani.

**Jinsi ya kuchambua takwimu**

Fanya muhtasari wa takwimu kutoka kwenye mipango ya usimamizi, watoa habari maalum na watu wengine wanaohusika katika jedwali ndani ya karatasi ya uchambuzi wa mahojiano/chanzo pili kama inavyoonyeshwa.

**Umuhimu wa habari hizi kwa wasimamizi na wadau wengine**

Habari kuhusu bodi za usimamizi ni muhimu katika kufahamu kwa jumla matokeo au athari za usimamizi kwa jamii, hasa juu ya utawala. Utambuzi wa bodi yenye mamlaka ya kisheria ya kutoa maamuzi juu ya shughuli za pwani utamwezesha msimamizi kuelewa vizuri safu za shughuli zinazofanyika katika eneo hilo, kulinganisha na bodi nyengine za usimamizi, kufanya kazi kwa uwazi zaidi katika mchakato wa usimamizi na kufanikiwa zaidi katika usimamizi.

Pia utambuzi wa bodi za usimamizi utawapatia wale wanaoathiriwa na hatua za usimamizi watu wenye mamlaka wa kushauriana nao.

## *K29. Mpango wa Usimamizi*

**Ni nini**

Mpango wa usimamizi unatoa mikakati ya muelekeo juu ya programu ya usimamizi wa rasilimali za pwani. Mpango wa usimamizi ni waraka unaoonyesha malengo makuu ya programu ya usimamizi pamoja na madhumuni yake , muundo wa mfumo wa usimamizi na itifaki ya hatua za usimamizi.

**Jinsi ya kukusanya takwimu**

Habari juu ya mpango wa usimamizi zinaweza kupatikana kwa kuwahoji watoa habari maalum kutoka kwa mamlaka zinazohusika za kitaifa, kimkoa na mamlaka za serikali za mitaa zilizo na wajibu wa kusimamia rasilimali za pwani. Kunaweza kuwa na mipango mingi ya usimamizi katika eneo la uchunguzi kutegemea na shughuli zilizopo, ikiwa ni pamoja na mpango wa uwiano wa ukanda wa pwani,mpango wa usimamizi wa uvuvi, mpango wa kuendeleza pwani, mpango wa usimamizi wa mikoko, na /au mpango wa kuendeleza utalii. Inaweza kufaa kuomba nakala za mipango husika ili kuweza kuelewa ni shughuli gani zinazoshughulikiwa.

| Shughuli za Pwani* | Mpango wa Usimamizi (Ndiyo/Hapana) |
|---|---|
| uvuvi | N |
| utalii | N |
| ufugaji wa viumbe baharini | H |

* Orodhesha kulingana na shughuli zilizotambuliwa katika shughuli (K18)

Kwa kila shughuli ya pwani, tambua kama (Ndiyo au Hapana) mpango wa usimamizi upo na andika ndani ya jedwali la *chanzo pili/mwongozo wa mahojiano* kama ilivyoonyeshwa.

*Ukusanyaji wa takwimu za ziada*: Habari juu ya vitengo vya mpango wa usimamizi (kwa mfano, kutia nguvu, elimu) zinaweza pia kukusanywa unapoulizia juu ya mpango.

**Jinsi ya kuchambua takwimu**

Andika takwimu kutoka kwa watoa habari mbalimbali na vyanzo pili ndani ya jedwali katika *karatasi ya uchambuzi wa mahojiano/chanzo pili* kama inavyoonyeshwa.

*Uchambuzi wa ziada:* Ni muhimu kutoa maelezo ya mpango kwa kila shughuli ya pwani. Ni muhimu pia kulinganisha mabadiliko ya kuwepo kwa mipango ya usimamizi kwa wakati na mabadiliko katika taratibu za matumizi na hali halisi ya rasilimali ili kuona kama kuna uhusiano.

**Umuhimu wa habari hizi kwa wasimamizi na wadau wengine**

Kujua kama mipango ya usimamizi ya shughuli mbalimbali ipo inasaidia kuelewa kwa jumla athari za usimamizi katika eneo la uchunguzi, hasa juu ya utawala. Kuwepo na kutekelezwa kwa mipango ya usimamizi kunawajulisha wasimamizi kwamba usimamizi wa rasilimali za pwani unaongozwa na malengo na madhumuni ili kufikia matokeo fulani yanayotarajiwa (mfano, uhifadhi na ulinzi), kwamba kuna mkakati wa msingi kuwezesha kufikia malengo na madhumuni haya na kwamba mpango mzima unatekelezwa na nguvu za kisheria.

Uchambuzi wa kulinganisha kuwepo kwa mipango ya usimamizi na vigezo vyengine vya utawala (kwa mfano, sheria za kawaida na umilikaji) na taratibu za matumizi ya rasilimali na hali halisi ya rasilimali ni muhimu kwa kuelezea ikiwa hizi hatua za utawala zinashawishi tabia na hali halisi ya rasilimali.
Kufahamu kuwepo kwa mpango wa usimamizi kwa shughuli mbalimbali kutawawezesha wadau kutumia mipango hii, na pamoja na wasimamizi, kueleza athari za usimamizi katika eneo la uchunguzi.

## *K30. Sheria wezeshi*

**Ni nini**

Sheria wezeshi ni kuwepo kwa sheria za kawaida kutoka serikalini ili kuupa usimamizi wa rasilimali za pwani msingi thabiti wa kisheria ili kwamba mpango,muundo wa usimamizi, sheria na kanuni, na taratibu za kutilia nguvu zinaweza kutambuliwa, kuelezwa, kuheshimiwa na kutekelezwa. Kwa mfano, sheria au kanuni za kitaifa za uvuvi inachukuliwa kuwa wezeshi kwa kuwa inaeleza wazi namna uvuvi utakavyofanyika na kusimamiwa nchini.

**Jinsi ya kukusanya takwimu**
Habari kuhusu sheria wezeshi zinapatikana kwa kuwahoji watoa habari maalum kutoka kwa mamlaka zinazohusika za kitaifa, kimkoa na mamlaka za serikali za mitaa zilizo na wajibu wa kusimamia rasilimali za pwani. Wakati wa mahojiano ingefaa kuomba nakala za nyaraka za sheria wezeshi ili kujua sheria wezeshi iliyopo.

| Shughuli* | Sheria Wezeshi (Ndiyo/Hapana) |
|---|---|
| uvuvi | N |
| utalii | H |
| ufugaji wa viumbe baharini | H |
| * Orodhesha kulingana na shughuli zilizotambuliwa katika shughuli (K18) | |

Sheria wezeshi inaweza kuwepo katika ngazi ya kimataifa, kitaifa, kimkoa/kiwilaya na kimtaa. Namna ya utekelezaji wa sheria juu ya usimamizi wa rasilimali za pwani utatofautiana kutoka nchi moja hadi nyengine. Taratibu za kisheria zinaweza kutegemea mambo mengi ikiwamo aina ya serikali, fedha zilizopo, mifumo ya kiutawala, hali ya mgawanyo wa madaraka, mahakama na utoaji wa maamuzi na, aina ya rasilimali na shughuli za pwani.

Hojaji na kupitia nyaraka kunafanyika ili kujua kama zipo (ndiyo au hapana) sheria zinazowezesha kusaidia mpango wa usimamizi kwa kila shughuli. Habari hii inaandikwa katika jedwali la chanzo pili/mwongozo wa mahojiano kama inavyoonyeshwa.

**Jinsi ya kuchambua takwimu**
Andika habari kutoka kwa watoa habari mbalimbali na vyanzo pili ndani ya jedwali katika *karatasi ya uchambuzi wa mahojiano/chanzo pili* kama inavyoonyeshwa.

*Uchambuzi wa ziada:* Ni muhimu kutoa maelezo mafupi kuhusu sheria wezeshi kwa kila shughuli ya pwani. Linganisha mabadiliko katika kuwepo kwa sheria wezeshi kwa wakati fulani na mabadiliko katika utaratibu wa matumizi ya rasilimali na hali halisi ya rasilimali ili kuona kama kuna uhusiano.

**Umuhimu wa habari hizi kwa wasimamizi na wadau wengine**
Sheria wezeshi ni muhimu ili kufahamu athari za jumla zinazotokana na usimamizi kwa jamii zilizomo katika eneo la uchunguzi, na hasa juu ya utawala. Ufahamu wa sheria wezeshi ni muhimu ili kuhakikisha kuwa mipango ya usimamizi na mikakati inapata usaidizi wa kisheria katika kufanikisha utekelezaji wake. Ufahamu wa sheria wezeshi utahakikisha kwamba kila hatua ya usimamizi inayochukuliwa inapata usaidizi wa kisheria. Shida zinazohusu athari zinazotokana na hatua za usimamizi zinaweza kulinganishwa kwa kufungamanishwa na mpango wa usimamizi na sheria wezeshi.

Uchambuzi wa kulinganisha kuwepo kwa sheria wezeshi na vigezo vyengine vya utawala (kwa mfano, sheria za kawaida na umilikaji) na utaratibu wa matumizi ya rasilimali na hali halisi ya rasilimali ni muhimu ili kujua kama hatua za kiutawala zinaleta mabadiliko katika tabia na hali halisi ya rasilimali.

Kuboresha ufahamu wa sheria zilizopo kutasaidia washikadau kufanya shughuli wakizingatia sheria.

## *K31. Nyenzo za Usimamizi*

**Ni nini**
Nyenzo za usimamizi inamaanisha watu na fedha (vitu au vifaa) vinavyotumika kutekeleza shughuli za mpango wa usimamizi.

| Shughuli za Pwani* | Idadi ya watumishi | Bajeti |
|---|---|---|
| uvuvi | 5 | 1,000 |
| utalii | 25 | 25,000 |
| ufugaji wa viumbe baharini | 0 | 0 |
| *Orodhesha kulingana na shughuli zilizotambuliwa katika Shughuli (K18) | | |

**Jinsi ya kukusanya takwimu**
Habari juu ya nyenzo za usimamizi zinaweza kukusanywa kwa kumhoji msimamizi au mkurugenzi wa kila bodi ya usimamizi katika eneo la uchunguzi. Msimamizi au mkurugenzi anaombwa kutoa jedwali la watumishi litakaloonyesha mgawanyo wa watumishi kwa programu au shughuli. Idadi ya watumishi (wa muda, wa kudumu, wakujitolea) kwa kila shughuli au programu wanatambuliwa. Mahali pasipo na jedwali la watumishi, linaweza kutengenezwa pamoja na msimamizi au mkurugenzi kwa kutambua programu au shughuli zote za bodi ya usimamizi na baadaye kutambua watumishi. Msimamizi au mkurugenzi anaulizwa pia juu ya bajeti ya bodi ya usimamizi na utekelezaji wa mpango wa usimamizi. Maitikio yanaandikwa kwenye jedwali katika *karatasi ya mwongozo wa mahojiano/chanzo pili.*

*Ukusanyaji wa takwimu za ziada:* Habari za ziada zinaweza kukusanywa kwa kuangalia bajeti iliyotolewa kwa kila shughuli binafsi kama elimu, au udhibiti. Habari inaweza pia kupatikana juu ya utaalam na vifaa vilivyotolewa kwa shughuli mbalimbali za usimamizi.

**Jinsi ya kuchambua takwimu**

Andika habari kutoka kwa watoa habari maalum tofauti ndani ya jedwali kwenya *karatasi ya uchambuzi/chanzo pili* kama ilivyoonyeshwa.

*Uchambuzi wa ziada:* Maelezo juu ya mgawo uliopo wa watumishi na bajeti kwa usimamizi wa pwani yanaweza kutolewa.

**Umuhimu wa habari hizi kwa wasimamizi na wadau wengine**

Kufahamu nyenzo za usimamizi ni muhimu ili kujua athari za usimamizi kwa jamii katika eneo la uchunguzi, hasa juu ya utawala. Kwa mfano, kufahamu watumishi waliopangwa kwa kila programu au shughuli ni muhimu ili kufahamu umuhimu wa shughuli mbalimbali, na pia kukadiria idadi na wingi wa shughuli fulani, kama vile doria. Kiwango cha nyenzo za usimamizi pia ni kiashiria cha ufanisi wa usimamizi, na uwezo wake wa kufikia malengo na kutekeleza mpango wa usimamizi.

Habari hii itakuwa muhimu kwa wadau wengine kutambua vyema umuhimu unaopewa usimamizi wa rasilimali za pwani na baharini, na rasilimali ambazo wanazitegemea kwa maishilio (uchumi).

## *K32. Umilikaji na Utaratibu wa Kawaida*

**Ni nini**

Umilikaji wa kawaida unahusika na haki ya matumizi kuhusiana na shughuli za pwani. Umilikaji wa kawaida huandikwa kuwa sheria. Kwa mfano, umilikaji wa kawaida ni haki ya kumruhusu mvuvi kutumia eneo fulani kuvua.

Taratibu za kawaida huandikwa kuwa sheria na hueleza hasa shughuli zinazoruhusiwa na zilizokatazwa na washikadau na mamlaka za serikali juu ya matumizi ya rasilimali za pwani. Kanuni huweka namna ya haki za matumizi. Kwa mfano, kwa wavuvi wenye haki ya kuvua katika eneo fulani, taratibu ya kawaida ni kwamba wanaweza kutumia uvuvi wa mishipi tu kuvua katika eneo hilo.

Kwa kigezo hiki tunaangalia kanuni na taratibu zile zinazo tumika katika shughuli za kila siku ili kusaidia watumiaji kutoa maamuzi juu ya matumizi ya rasilimali za pwani kuhusu lini, wapi na jinsi gani ya kutumia rasilimali. Kanuni na sheria hizi ni kwa shughuli za pwani tu na zinaweza kuwekwa na mamlaka inayohusika na usimamizi wa shughuli za pwani.

**Jinsi ya kukusanya takwimu**

Sheria za kawaida kuhusu umilikaji zinaweza kupatikana kutoka vyanzo pili kama vile sheria zilizoandikwa za kitaifa, kimkoa au za kijiji. Sheria hizi zimeandikwa na kuchapishwa kisheria na seikali. Sheria hizi zinajumuisha sheria au kanuni za kitaifa za uvuvi, sheria za mazingira zinazohusu uvunaji wa mikoko, matumizi ya matumbawe na sheria kuhusu uendelezaji wa makazi ya pwani. Habari za ziada zinaweza kupatikana kwa kuwahoji watumishi wa serikali katika taasisi zinazohusika na usimamizi wa kila shughuli ya pwani.

| Shughuli za Pwani* | Umiliki wa Kawaida na Taratibu (Ndiyo/Hapana) | Sheria na Kanuni zinazohusika (Ndiyo/Hapana) |
|---|---|---|
| uvuvi | N | N |
| utalii | H | H |
| ufugaji wa viumbe baharini | N | H |

* Orodhesha kulingana na shughuli zilizotambuliwa katika shughuli (K18)

Sheria na kanuni za shughuli za pwani zipatikane toka ngazi ya taifa, mkoa na serikali za mitaa. Kwa kila shughuli ya pwani tambua upo (Ndiyo au Hapana) kama upo mpangilio au mipangilio ya sheria za kawaida katika ngazi ya kijamii. Habari hizi ziandikwe ndani ya jedwali la mwongozo wa mahojiano/chanzo pili kama ilivyoonyeshwa.

**Jinsi ya kuchambua takwimu**

Fanya muhtasari wa takwimu kutoka kwa watoa habari maalum tofauti na vyanzo pili ndani ya jedwali kwenye *karatasi ya uchambuzi wa mahojiano/chanzo pili* kama inavyoonyeshwa hapa chini.

*Uchambuzi wa ziada:* Ni muhimu kutoa maelezo juu ya sheria na kanuni za kawaida kwa kila shughuli ya pwani. Linganisha mabadiliko katika kuwepo kwa *mpango wa usimamizi (K29)* kwa muda na mabadiliko katika *utaratibu wa matumizi (K23)* na *ufahamu wa hali halisi ya rasilimali (S19)* kuona kama kuna uhusiano.

**Umuhimu wa habari hizi kwa wasimamizi na wadau wengine**

Kanuni na sheria za kawaida zinasaidia kuelewa kwa jumla athari za usimamizi kwa jamii hasa juu ya utawala. Umiliki juu ya rasilimali za pwani waweza kuwa na mamlaka kamili juu ya matumizi na mgawanyo wa rasilimali kwa vikundi, kama vile vikundi vya wavuvi, ama kutokuwa na mamlaka ya matumizi kabisa kisheria. Kwa msimamizi, ni muhimu sana kufahamu habari hii ili kuweza kubuni na kutekeleza mipango sawia na mizuri ya usimamizi, na athari kufahamika na kufanyiwa kazi.Ni muhimu kufahamu uwepo na uwezo wa kanuni na taratibu za kawaida za matumizi zilizopo ambazo wadau, pamoja na mamlaka ya usimamizi,wanazo juu ya rasilimali za pwani katika eneo ili kwamba vyombo vya usimamizi viweze kufanya kazi kwa ufanisi.

Kigezo hiki kinasaidia kufahamu viwango vya udhibiti vilivyopo juu ya shughuli za watu katika eneo la pwani na, ni kwa kiasi gani watu wanaweza kukubali sheria za ziada za kusimamia shughuli za pwani na kuathiriwa na sheria hizi.Watumiaji wa rasilimali wanaweza kuhalifu sheria ikiwa hawazifahamu kanuni na sheria hizo au kama wanaona hazina maana.

Kulinganisha kuwepo kwa sheria na kanuni za kawaida na utaratibu wa matumizi ya rasilimali na hali halisi ya rasilimali hiyo inasaidia kujua kama hatua hizi za usimamizi zinaleta mabadiliko juu ya tabia na afya ya rasilimali.

Kwa kufahamu sheria na kanuni za kawaida,wadau wataweza kufanya shughuli zao kwa kuzizingatia. Zaidi ya hivyo, wadau wanaweza kusaidia kuchangia kuongezeka kwa upatanifu wa sheria hizi za kawaida na sheria na kanuni za umilikaji zisizokuwa za kawaida, mila na desturi.

## *K33. Umilikaji na Utaratibu usio Rasmi, Mila na Desturi*

**Ni nini**

Katika jamii nyingi za pwani, kuna mifumo miwili ya usimamizi wa rasilimali za pwani. Mfumo wa usimamizi usio rasmi uliotungwa na kutekelezwa na jamii ya watumiaji wa rasilimali, mara nyingi huambatana na mfumo rasmi wa usimamizi wa serikali. Mifumi hii isiyo rasmi inaweza kuwa rahisi au migumu, inayokubalika kirahisi au kutunzwa kwa uangalifu. Mila na desturi za matumizi na usimamizi wa rasilimali za pwani ni vitendo vinavyoangazia ujamaa na mila za watu, tabaka au muundo wa jinsia wa jamii. Zinaweza kujumuisha kwa mfano, kumchagua mvuvi mzee kuongoza shughuli za uvuvi, kuongoza maombi kabla ya kuanza kuvua, mbinu ya kutatua migogoro au utoaji wa maamuzi.

Kanuni na taratibu zisizo rasmi ni zile kanuni ambazo hazikuandikwa, matendo (ya kimila na kitamaduni yanayowapa watu haki ya kutumia rasilimali au inaeleza mahsusi matendo yanayoruhusiwa na yale yaliyokatazwa na watumiaji wa rasilimali kwa kuhusiana na shughuli za pwani. Pia inaonyesha kiwango cha kukubalika kwa kanuni hizo zisizo rasmi.

**Jinsi ya kukusanya takwimu**

| Shughuli ya pwani* | Mila na Desturi | Mipangilio ya Taratibu zisizo rasmi | Kanuni zisizo rasmi | Kiwango cha kukubali /kutii(Juu, Kati, Chini) |
|---|---|---|---|---|
| Uvuvi wa chewa | Kufungwa kwa eneo au musimu wakati chewa wanataga mayai | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| * Orodhesha kulingana na shughuli zilizotambuliwa katika *shughuli (K18)* | | | | |

Habari kuhusu umilikaji na taratibu usiokuwa rasmi kwa kila shughuli ya pwani zinaweza kupatikana kwa mchanganyiko wa kuwahoji watoa habari maalum na uangalizi. Watu wanaofaa kuwa watoa habari maalum ni pamoja na watu maarufu katika jamii na maafisa

wa serikali. Watoa habari maalum wanaulizwa watoe maelezo mafupi juu ya mila/desturi, kanuni na utaratibu wa umilikaji usiokuwa rasmi kwa kila shughuli kama ilivyoonyeshwa katika jedwali la mwogozo wa mahojiano/chanzo pili hapa chini. Baadaye wanaulizwa kwa kila kanuni na taratibu za umiliki, mila/desturi waonyeshe kiwango cha kukubali ambapo, kiwango cha kukubali kwa jamii (Juu, Kati au Chini). Uangalizi ni muhimu pia kwa sababu habari zinazopatikana kwa kuwahoji watu tu zinaweza zisionyeshe hali halisi ya mambo. Watumiaji wa rasilimali wanaweza kuangaliwa wakati wanapofanya shughuli kuona kama wanatekeleza zile kanuni na taratibu kama ilivyoelezwa.

Wakati wa kukusanya habari juu ya tawala zisizo rasmi, ni ifahamike kwamba inaweza kuchukua muda mwingi kuelewa hasa mipangilio hii. Hii inaweza kulazimu kutumia muda wa ziada kukaa na wanajamii ili kujifunza kwa kiundani mifumo hii. Ni muhimu pia kwa timu ya uperembaji kufahamu ni makundi gani (watumiaji, umri, jinsia, wasio wenyeji) wanakubaliana au hawakubaliani na taratibu na kanuni zisizorasmi, mila na desturi.

**Jinsi ya kuchambua takwimu**
Andika habari kutoka kwa watoa habari maalum ndani ya jedwali katika karatasi ya uchambuzi wa mahojiano/chanzo pili.

*Uchambuzi wa ziada:* Ni muhimu kutoa maelezo mafupi juu ya kanuni na taratibu za umilikaja zisizo rasmi, mila na desturi zinazohusiana na matumizi za rasilimali ya pwani na usimamizi kwa kila shughuli .

**Umuhimu wa habari hizi kwa wasimamizi na wadau wengine**
Mila na desturi za usimamizi na matumizi ya rasilimali za pwani na taratibu na kanuni zisizo rasmi zinasaidia kufahamu athari ya usimamizi kwa jamii na kwa kufahamu umuhimu wa rasilimali na matumizi yake kiutamaduni. Ufahamu wa kanuni na taratibu zisizo rasmi ni muhimu, kwa kuwa watumiaji wanaweza kuziona taratibu hizi zinawafaa zaidi kuliko kanuni na sheria na hivyo kutojali au kutotilia maanani sheria rasmi na amri zake. Kufahamu kwa taratibu na kanuni zisizo rasmi kutamwezesha msimamizi kuandaa mpango wa usimamizi unao heshimu mila na desturi na kuwa msingi wa kujengea hatua za kisheria. Hii inaweza kukubalika zaidi na watumiaji wa rasilimali, na kuletea kuinua kiwango cha kukubali sheria. Kwa kufahamu mila na desturi msimamizi ataweza kutambua na kuziwianisha ndani ya mipango ya usimamizi ili kupunguza au kuondoa athari kwa shughuli za kijamii na kitamaduni katika jamii. Kufahamu kama kanuni na taratibu hizi zinaheshimiwa na nani kutamwezesha msimamizi kufahamu vyema ikiwa mguso wa kuziunganisha kanuni na taratibu hizo katika mipango aliyoitengeneza.

Pia taratibu na kanuni zisizo rasmi zinaweza kutoa mbinu ya namna ya kuhifadhi maliasili, kama vile majira yasiyoruhusiwa kuvua, maeneo ya tambiko, na hii inaweza kuwa sehemu moja ya mpango wa usimamizi wa eneo hilo ambao utaenda kukamilisha mipango rasmi ya usimamizi.

Kufahamu vizuri taratibu na kanuni za umilikaji zisizo rasmi, mila na desturi za makundi mengine ya washikadau, kutasaidia kuboresha mahusiano na heshima kati ya wadau kama migogoro ni tatizo katika eneo la uchunguzi. Kwa kutoa habari juu ya taratibu na kanuni zisizo rasmi, mila na desturi, wadau wanaweza kuhakikisha msimamizi anazielewa ili aziunganishe katika mipango ya usimamizi.

## *K34. Vivutio kwa jamii*

**Ni nini**
Kivutio kwa jamii inahusika na kuwepo kwa mipango ya kuvutia jamii iweze kujihusisha kikamilifu katika usimamizi mzuri wa rasilimali za pwani na baharini. Hivi vyaweza kuwa fedha/ushuru (kwa mfano, asilimia ya fedha wanazotozwa watalii zinatolewa kwa hazina ya jamii), hazina za jamii, mikopo midogo.

**Jinsi ya kukusanya takwimu**
Habari zinakusanywa kutoka kwa watoa habari maalum kama vile wawakilishi wa wadau, wasimamizi wa shughuli za pwani, mwenyekiti wa ushirika wa mahoteli, mwenyekiti wa ushirika wa wavuvi n.k.

Wahojiwa wanaulizwa kuorodhesha vivutio vilivyopo na ambavyo wanavipata au ambavyo vimeanzishwa ili kuongeza faida za kuhifadhi kwa jamii na/au kuongeza ushiriki wa wadau katika shughuli za usimamizi.

**Jinsi ya kuchambua takwimu**
Andika habari kutoka kwa watoa habari maluum katika jedwali ndani ya *karatasi ya uchambuzi/chanzo pili* kama ilivyoonyeshwa hapa chini.

| Kundi la wadau | Faida kutoka kwa<br>Kutoa kwa | Aina ya Kivutio |
|---|---|---|
| Hoteli Kubwa | Kutoa | 30USD kwa kitanda/usiku kwa hazina ya jamii |
| Wavuvi | Faida | Punguzo la bei kwa ununuzi wa mitego na kupunguza matumizi ya juya kutoka Idara ya Uvuvi. |
| | | |

*Uchambuzi wa ziada*: Linganisha mabadiliko katika vivutio kwa jamii na mabadiliko katika *viwango vya athari*, mabadiliko katika *mbinu/njia (K20)* na mabadiliko katika *utaratibu wa matumizi (K23)* kwa miaka kadhaa.

**Umuhimu wa habari hizi kwa wasimamizi na wadau wengine**

Kufahamu kuwepo kwa mipango ya vivutio kwa jamii inasaidia kufahamu athari za usimamizi wa rasilimali katika eneo la uchunguzi. Wasimamizi watafahamu kama aina fulani ya kivutio kinafaa zaidi na kama inasaidia katika kuongeza ushiriki wa wadau katika shughuli za usimamizi.

Kufahamu kuwepo kwa mipango hii kutaongeza matumizi ya vivutio hivyo kwa uwazi zaidi katika jamii na kutoa nafasi kwa wadau kuweza kuvitumia. Kuongeza ufahamu wa wadau wa vivutio hivi kutawezesha wadau kuviulizia na kushiriki.

## *K35&S17. Ushirikishwaji na Kuridhika kwa Wadau*

**Ni nini**

Ushirikishwaji na kuridhika kwa wadau ni kipimo cha kiasi gani watu wanashirikishwa katika shughuli za usimamizi wa pwani (kutoa maamuzi na utekelezaji) na namna wanavyoridhishwa na kiwango cha ushirikishwaji wao. Shughuli za utekelezaji ni pamoja na udhibiti wa sheria, uhamasishaji na uperembaji.

### NGAZI YA JAMII (K35)

**Jinsi ya kukusanya takwimu**

Habari juu ya ushirikishwaji wa wadau (kutoka pasipo na ushirikishwaji mpaka kiwango cha juu kabisa cha ushirikishwaji) na kuridhika (Juu, Kati, Chini) zinaweza kupatikana kwa kuwahoji watoa habari maalum na maafisa wa jamii, viongozi, mashirika ya wadau, watumishi wa maeneo ya usimamizi na wawakilishi wa vikundi vya kuhojiwa maalum vya wadau. Kama inavyoonyeshwa

| Kundi la Wadau* | Shughuli** | Ushirikishwaji wa wadau (1 mpaka 5)*** | Kiwango cha kuridhishwa na ushirikishwaji (J/K/C) |
|---|---|---|---|
| Wavuvi | Kutoa maamuzi | 3 | J |
| | Uperembaji | 1 | K |
| | Udhibiti | 2 | C |
| Wachuuzi wa samaki | Kutoa maamuzi | 1 | K |
| | Uperembaji | 1 | J |
| | Udhibiti | 1 | K |
| | | | |
| | | | |

*Tengeneza orodha kulengana na makundi ya wadau yaliyotamuiliwa katika *wadau (K2)*
***Tengeneza orodha ya Shughuli za usimamizi kama ilivyo katika mpango uliopo wa usimamizi (K29)*
***1=Hakuna ushirikishwaji, 5=Ushirikishwaji kikamilifu

katika jedwali la *chanzo pili/mwongozo wa mahojiano* hapo chini, wahojiwa wanaulizwa habari juu ya kiwango cha ushirikishwaji wa wadau katika kutoa maamuzi ya usimamizi wa pwani na utekelezaji wa shughuli (1=Hakuna ushirikishwaji; 5=Ushirikishwaji kikamilifu) na kama wanaridhishwa na kiwango chao cha ushirikishwaji (Juu, Kati, Chini*).*

*Ukusanyaji wa takwimu za ziada:* Taarifa za ushirikishwaji wa wadau zinaweza kupatikana pia kwa kuangalia kwenye mikutano ya usimamizi wa pwani kuona kama wadau wanahudhuria na kutoa maoni yao, na kuona kama bodi ya usimamizi inakubali maoni hayo. Timu ya uperembaji inaweza kuchunguza kwa nini watu hawaridhishwi na kiwango cha ushirikishwaji na ni namna gani inaweza kubadilika.

**Jinsi ya kuchambua takwimu**

Andika taarifa kutoka kwa watoa habari maluum na uangalizi katika jedwali kwenye *karatasi ya uchambuzi wa mahojiano/chanzo pili*.

*Uchambuzi wa takwimu wa ziada:* Ni muhimu kutoa maelezo ya viwango na aina ya ushirikishwaji katika usimamizi wa pwani.

## NGAZI YA KAYA: S17

**Jinsi ya kukusanya takwimu**

Takwimu za ushirikishwaji katika usimamizi wa pwani zinapatikana kwa kumuuliza kila mhojiwa:

Kwa kipimo cha 1 mpaka 5 (1=hakuna ushirikishwaji, 5=Ushirikishwaji kikamilifu), ni kwa kiasi gani unashiriki katika shughuli za usimamizi wa pwani kwa:

kutoa maamuzi? _____
Uperembaji?
uhamasishaji?
udhibiti na doria?

Kwa kipimo cha 1 mpaka 3 (1=Chini, 2=Kati, 3=Juu), ni kwa kiasi gani unaridhishwa na kiwango chako cha kushiriki katika shughuli za usimamizi wa pwani kwa:

kutoa maamuzi? _____
uperembaji? _________
uhamasishaji?
udhibiti na doria?

Orodha ya shughuli za usimamizi itabadilika kulengana na shughuli zilizopewa kipaumbele na usimamizi (angalia mpango wa usimamizi uliopo).

*Ukusanyaji wa takwimu za ziada:* Wahojiwa wanaweza pia kuulizwa: "Je, unaweza kushiriki katika utoaji wa maamuzi/shughuli za usimamizi wa pwani?", na "Je ungependa kuona ushirikiano aina gani?" Kama hawaridhishwi na kiasi cha ushirikishwaji ni vyema kuwauliza wahojiwa "Kwa nini" au "Je, ni vipi ushirikishwaji waweza kuboreshwa?" Maswali haya yanaulizwa ili kujua kama watu wanafamu kuwa wanayo nafasi ya kushiriki katika kutoa maamuzi na shughuli za usimamizi wa pwani na namna gani wangependa kushiriki katika siku za mbele.

**Jinsi ya kuchambua takwimu**

Piga hesabu ya asilimia ya wahojiwa kutoka kwa uchunguzi kwa kila kipimo cha ushirikishwaji na kuridhishwa na andika katika karatasi ya uchambuzi wa mahojiano kulingana na shughuli. Tafuta kwa kila kiwango cha ushirikishwaji na kwa kila shughuli iliyoorodheshwa, asilimia ya viwango vya kuridhishwa, yaani Juu, Kati, na Chini (angalia karatasi ya uchambuzi wa mahojiano).

*Uchambuzi wa takwimu wa ziada:* Linganisha matokeo haya kila baada ya muda ili kuona kama kiwango cha ushirikishwaji na kuridhishwa vinaongezeka, kupungua au vinabaki vile vile. Linganisha matokeo haya na taarifa za *mitazamo ya watu juu ya hali halisi ya rasilimali na matishio (S19 na S20)* na *ufahamu wa kanuni na sheria (S21)* kuona kama kuna uhusiano. Kwa mfano, kama watu hawafahamu juu ya sheria na kanuni na hawajali sana juu ya uharibifu wa rasilimali, basi hawatakuwa na mvuto wa kushiriki katika shughuli za usimamizi. Unaweza kufanya mazungumzo mafupi juu ya ushirikishwaji na kuridhika, na kama kumekuwa na mabadiliko kwa wakati na ufungamanishe na mitazamo ya watu.

**Umuhimu wa habari hizi kwa wasimamizi na wadau wengine**

Kushiriki kikamilifu kwa wadau katika shughuli za usimamizi wa pwani kunaweza kuchangia sana katika kuboresha ufanisi wa

shughuli za usimamizi wa pwani. Kama wadau wanashirikishwa katika kutoa maamuzi na utekelezaji na kujisikia kuwa shughuli ni zao, ni hakika kuwa wataunga mkono shughuli za usimamizi wa pwani. Uungaji mkono wa wadau ni muhimu kwa mafanikio ya usimamizi wa pwani.

Kwa kufuatilia ushirikishwaji kwa kipindi fulani, msimamizi ataweza kufahamu ufanisi wa programu katika kuwashirikisha wadau katika usimamizi, ambalo mara nyingi ndilo lengo la usimamizi. Kufuatilia kiwango cha kuridhika kwa wadau katika kushiriki kwao katika mchakato wa usimamizi wa pwani kutampa msimamizi pia marejesho juu ya kuridhishwa kwa wadau na mipango ya usimamizi na hivyo uwezekano wao wa kuendelea kuunga mkono.

Kiwango cha ushirikishwaji ni muhimu kufahamu umuhimu wa rasilimali za pwani kwa wanainchi. Jinsi watu wanavyo thamini rasilimali, ndivyo ulivyo uwezekano wao wa kushiriki katika usimamizi. Kuna sababu nyingine pia, kama vile hali ya hatari (kwa mfano, umwagikaji wa mafuta), lakini kwa jumla kiwango cha ushirikishwaji kinaweza kutumika kuonyesha umuhimu wa rasilimali.

Kufuatilia kiwango cha ushirikishwaji na kuridhishwa na ushirikishwaji kutawapa wadau nafasi ya kufanya marejesho kwa wasimamizi juu ya mchakato wa usimamizi. Kutawasaidia washikadau kumsaidia msimamizi kuelekeza nguvu kwa wadau maalum.

## *K36. Mashirika ya Kijamii na ya Wadau*

**Ni nini**

Mashrika ya kijamii na ya wadau ni njia ya uwakilishi wa watumiaji wa rasilimali na wadau katika usimamizi wa rasilimali za pwani na kushawishi mwelekeo wa utoaji maamuzi na usimamizi.

**Jinsi ya kukusanya takwimu**

Habari juu ya mashirika ya kijamii na ya wadau zinapatikana kutoka vyanzo pili na mahojiano na watoa habari maluum au wawakilishi wa makundi maluum ya wahojiwa, ikiwa ni pamoja na watumishi katika ofisi zinazohusika na usimamizi, watumishi wa serikali, viongozi katika jamii, wafuasi wa mashirika mengine katika jamii, wavuvi maarufu, wawakilishi wa mashirika ya kidini na wawakilishi wa mashirika yasiyo ya kiserikali.

Kama inavyoonyeshwa katika jedwali la *chanzo pili/mwongozo wa mahojiano*, kwa kila shirika habari zinakusanywa kama ni shirika lililoruhusiwa rasmi au si rasmi, na kazi zake muhimu. Watoa habari maalum wanaulizwa kama shirika linaushawishi katika masuala ya usimamizi wa pwani, masuala ya kijamii, masuala yote ya usimamizi wa pwani na ya kijamii, au halina ushawishi.

| Shirika la Kijamii | Rasmi au si Rasmi | Kazi Muhimu | Ushawishi (juu ya usimamizi wa pwani; masuala ya kijamii; yote; halina ushawishi |
|---|---|---|---|
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |

**Jinsi ya kuchambua takwimu**

Fanya muhtasari wa habari kutoka kwa watoa habari maluum, makundi maalum ya wahojiwa, na vyanzo pili katika jedwali kwenye karatasi ya uchambuzi wa mahojiano/chanzo pili.

*Uchambuzi wa ziada:* Tambua idadi ya mashirika ya kijamii na ya wadau, yawe rasmi au si rasmi, na kazi yao/wajibu wao. Piga hesabu ya asilimia ya mashirika yasiyo rasmi na yaliyo rasmi.

**Umuhimu wa habari hizi kwa wasimamizi na wadau wengine**

Kuyafahamu mashirika ya kijamii na ya wadau kutawasaidia wasimamizi kuboresha ushirikishwaji na uwakilishi wa wadau katika shughuli za usimamizi na utoaji maamuzi. Matokeo yanahitaji kutafsiriwa dhidi ya misingi ya kiwango cha kijamii au utendaji wa pamoja ndani ya nchi au eneo. Kuyafahamu mashirika kutampa msimamizi kutambua makundi mbalimbali yatakayoathiriwa na mikakati ya usimamizi na kushughulikia athari hizi kwa kushirikiana na mashirika hayo.

Kwa kuwa na ufahamu mzuri wa mashirika ya wadau, wadau watakuwa na ufahamu mzuri wa kiwango cha uwakilishi wao katika shughuli za usimamizi wa rasilimali za pwani na uwezo wa kushawishi utoaji maamuzi. Inaweza kuonyesha uhitaji wa utendaji kazi kwa pamoja.

Kwa mfano, ukosefu wa utendaji kazi kwa pamoja katika maeneo fulani ya pwani ya Kenya na Tanzania kumetambuliwa kama kikwazo kwa maendeleo ya maishilio/kiuchumi.

## *S18. Uanachama katika Mashirika ya Wadau*

**Ni nini**

Uanachama katika mashirika ya watumiaji wa rasilimali una maana ya uanachama rasmi au uanachama usio rasmi. Mashirika ya wadau yanajumuisha watumiaji wa moja kwa moja (kwa mfano, ushirika wa wavuvi, vilabu vya wazamiaji) pamoja na watu ambao shughuli zao huathiri rasilimali (kwa mfano, ushirika wa wasimamizi wa mwitu,ushirika wa mahoteli), na watu wasiotumia au kuathiri rasilimali, lakini wanahusika katika usimamizi (kwa mfano, mashirika ya mazingira).

**Jinsi ya kukusanya takwimu**

Takwimu za uanachama katika mashirika ya wadau zinapatikana kwa kuuliza kila mhojiwa:

Katika kaya yako kuna mwanachama wa shirika lolote? _____
Shirika/mashirika gani? ________________________________

*Ukusanyaji wa takwimu za ziada:* Timu ya uperembaji pia yaweza kuuliza juu ya uanachama katika mashirika ya kiraia (kwa mfano, kanisa, shirika la vijana, kikundi cha wanawake) kupata ufahamu juu ya ushirikishwaji wa jamii kwa ujumla.

**Jinsi ya kuchambua takwimu**

Piga hesabu ya asilimia ya wahojiwa ambao ni wanachama angalau wa shirika/kundi moja. Halafu orodhesha mashirika yaliyotajwa na upige hesabu ya asilimia ya wahojiwa waliosema ni wanachama wa kila shirika. Andika habari hii katika karatasi ya uchambuzi wa uchunguzi.

Asilimia ya waliotaja wana uanachama angalau katika shirika moja: ____82%___

| Mashirika yenye wanachama | % Wahojiwa kwa shirika |
|---|---|
| Ushirika wa Wavuvi _ | 67% |
| Ushirika wa Michezo Baharini | 32% |
| Ushirika wa Kitalii | 10% |
| Kikundi cha wenye Biashara ya Viumbe Baharini | 25% |

*Uchambuzi wa ziada*: Linganisha matokeo kwa kipindi fulani kuona jinsi uanachama unavyobadilika. Linganisha asilimia za uanachama wa mashirika mbalimbali ya wadau na *kazi (K7)* kuona kama pana mahusiano (kwa mfano, ikiwa asilimia 90 ya watu wote katika jamii ni wavuvi, basi kuna asilimia kubwa pia ya uanachama katika chama cha wavuvi). Maelezo mafupi ya uanachama yanaweza kutolewa, jinsi inavyohusiana na muundo wa shughuli za wanakijiji na inavyo badilika na muda.

**Umuhimu wa habari hizi kwa wasimamizi na wadau wengine**

Kama mashirika yaliyotajwa yanajihusisha katika usimamizi wa pwani, basi uanachama unaweza kuwa kiashiria muhimu cha ushirikishwaji wa wadau katika usimamizi. Kwa mfano, kama chama cha wavuvi kimefunga maeneo fulani yasitumike kwa uvuvi, basi uanachama mkubwa inaonyesha ushirikishwaji mkubwa katika usimamizi.

Kulinganisha kati ya uanachama na kazi za wanakijiji ni muhimu kufahamu kama kundi fulani lina wanachama wengi zaidi. Makundi yenye wanachama wengi zaidi ni ya umuhimu mkubwa, au chama hiki kinachukuliwa kuwa na ufanisi na manufaa zaidi. Kama kazi iliyo na ajira ndogo lakini inaonekana kuwa na wanachama wengi yawezekana kuwa watu wasioajiriwa katika shughuli hiyo lakini wanaipenda. (kwa mfano,watu wakihama kutoka kazi ya uvuvi na kwenda utalii, watu wanaweza kuendelea kuwa wanachama wa ushirika wa wavuvi kwa sababu wanaipenda ). Ni muhimu kuongea na watoa habari maluum kupata maelezo ya matokeo haya.

Kubadilika kwa uanachama kwa vipindi fulani ni muhimu ili kujua mabadiliko katika vipaumbele na mapendeleo ya watu. Kwa mfano, kuongezeka kwa uanachama katika mashirika ya mazingira, kunaonyesha watu kuvutiwa au kupendezewa zaidi na shughuli za uhifadhi. Ni muhimu pia kuongea na watoa habari maalum kueleza matokeo haya.

### *K37. Nguvu na Ushawishi*

**Ni nini**
Nguvu na ushawishi inahusu ni watu wapi au vikundi vipi katika jamii vyenye ushawishi hasa kuhusiana na kufikia, utumiaji na udhibiti wa rasilimali za pwani na baharini.

**Jinsi ya kukusanya takwimu**
Habari juu ya nguvu na ushawishi zinapatikana kwa kuwahoji watoa habari maluum au makundi maalum ya wawakilishi. Hawa watajumuisha wawakilishi wa wadau mbalimbali ambao wanaufahamu na uzoefu wa njia za udhibiti na ufikiaji wa rasilimali katika jamii. Jinsia na umri aghalabu huwa ni vitu muhimu, na uchaguzi wa makundi na/au watoa habari maluum lazima uzingatie mambo haya.

*Ukusanyaji wa takwimu za ziada:* Timu pia inaweza kupenda kujua kama kuna migogoro kati ya wadau.

Watoa habari maluum/makundi au wadau wataulizwa juu ya shughuli zilizotambuliwa (K18):

Orodhesha mashirika au watu binafsi ambao wanahusika katika kutoa maamuzi juu ya shughuli zako (yaani wapi ufanyie, lini, namna gani, na nani anayeruhusiwa kufanya shughuli hii)?___________________

Ni nani (shughuli, umri, jinsia) mwingine ambaye lazima umushauri ili shughuli iweze kufanyika, kupanuliwa, au kubadilishwa? ______________

Unapata wapi habari za rasilimali za pwani na baharini (kwa mfano, mashirika yasiyo ya kiserikali, makundi ya kijamii, magazetini)?________________

**Jinsi ya kuchambua takwimu**
Fanya muhtasari wa habari katika karatasi ya uchambuzi wa mahojiano/chanzo pili na weka katika madaraja makundi, watu binafsi, na vyanzo vya habari kulingana na mara ngapi zimetajwa (zilizotajwa zaidi ndizo zilizo na nguvu zaidi, na kwa hivyo daraja la juu).

**Umuhimu wa habari hizi kwa wasimamizi na wadau wengine**
Makundi ya watu/watu binafsi walio na nguvu na ushawishi katika jamii ni muhimu sana kwa mafanikio ya shughuli yoyote katika jamii hiyo, aidha wanahusika moja kwa moja na rasilimali za pwani na baharini au la. Hivyo basi, kuyafahamu makundi hayo kutamwezesha msimamizi kuhakikisha kwamba yanazingatiwa katika maamuzi ya usimamizi na kuongeza ufanisi katika usimamizi.

Kupambanua ni nani wenye nguvu/uwezo na ushawishi kutawasaidia wanajamii kuchuja michakato kutoa maamuzi ili kuboresha shughuli za usimamizi.

## MITAZAMO NA UFAHAMU

### *S19. Ufahamu wa Hali ya Rasilimali*

**Ni nini**
Ufahamu wa hali ya rasilimali ni kipimo cha watu wanavyofikiria juu ya hali ya rasilimali za pwani.

**Jinsi ya kukusanya takwimu**
Takwimu juu ya ufahamu wa hali ya rasilimali zinapatikana kwa kumuuliza kila mhojiwa:

Unawezaje kueleza hali ya sasa ya rasilimali zifuatazo kwa kutumia kipimo cha nzuri sana (5), nzuri (4), wastani (3), mbaya (2), mbaya sana (1) (tengeneza orodha ya rasilimali kulengana na rasilimali zinazopatikana katika eneo husika): mikoko ---------------------, miamba ya matumbawe ------------------, maji baridi --------------------------, misitu ya juu ----------------------------, nyasi bahari -----------------------

**Jinsi ya kuchambua takwimu**
Kwa kila rasilimali piga hesabu ya asilimia ya maitikio kwa kila kiwango cha kipimo na andika katika karatasi ya uchambuzi wa uchunguzi.

| RASILIMALI* | ASILIMIA YA WAHOJIWA WALIOELEZEA HALI YA RASILIMALI KUWA: | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | Nzuri sana (5) | Nzuri (4) | Si Nzuri wala Mbaya (3) | Mbaya (2) | Mbaya sana (1) |
| Mikoko | 3% | 10% | 30% | 34% | 23% |
| Mwamba wa Matumbawe | 5% | 12% | 34% | 30% | 23% |
| Maji baridi | 2% | 15% | 62% | 15% | 6% |
| Misitu ya bara | 40% | 30% | 20% | 8% | 2% |
| Nyasi bahari | 12% | 18% | 30% | 27% | 2% |
| *tengeneza orodha ya rasilimali kulengana na eneo husika | | | | | |

*Uchambuzi wa ziada:* Baadhi ya maitikio yanaweza kuunganishwa kurahisisha tafsiri. Kwa mfano, kama 23% ya wahojiwa wanasema mikoko iko katika hali mbaya sana na 34% wanasema iko katika hali mbaya, basi hii yaweza kuunganishwa na kusema "zaidi ya asilimia hamsini ya wahojiwa wanasema mikoko iko katika hali mbaya au mbaya sana." Hii ni rahisi kueleweka kuliko kuorodhesha asilimia kwa kila hali. Kwa kuongezea, maelezo mafupi yaweza kutolewa kuelezea ufahamu wa watu juu ya hali ya rasilimali. Fuatilia matokeo haya kwa muda kujua mabadiliko ya uelewa wa watu juu ya rasilimali. Linganisha matokeo haya na yale ya uchunguzi wa kisayansi kupata uhakika wa uelewa wa watu juu ya hali ya rasilimali.

**Umuhimu wa habari hizi kwa wasimamizi na wadau wengine**

Habari kuhusu ufahamu wa hali ya rasilimali ni muhimu kuweza kujua matishio ya rasilimali. Kwa kufahamu ni rasilimali gani zilizo katika hali mbaya, wasimamizi wataweza kufahamu matishio makuu ya rasilimali kwa kuwa matishio mengi yanahusiana na aina maalum ya rasilimali. Kwa mfano, kama mikoko, matumbawe ya mwamba na nyasi bahari zinaonekana kuwa katika hali mbaya sana kuliko misitu ya bara na maji baridi, basi shughuli zilizojikita katika bahari kama vile uvuvi na usafiri wa kutumia vyombo zaweza kuwa na athari kubwa zaidi kuliko shughuli za juu/bara.

Habari hizi ni muhimu pia ili kuwezesha kuanzisha mipango ya ufahamu na uhamasishaji na kutafuta ushirikishwaji wa wadau. Kama wanajamii hawaoni kama rasilimali ziko katika hali ya hatari, basi itakuwa vigumu kuwashirikisha katika shughuli za usimamizi. Kama wanajamii wanaziona rasilimali ziko katika hali nzuri, wakati utafiti wa kisayansi unadhihirisha kwamba zinadidimia, basi mpango wa ufahamu na uhamasishaji itabidi uanzishwe ili kuongezea ufahamu wa watu juu ya hali ya rasilimali.

Kwa kufuatilia habari hizi kwa muda, msimamizi anaweza kuona athari/mguso wa usimamizi juu ya mitazamo na ufahamu wa watu. Kwa mfano, kama mpango wa usimamizi wa pwani ulianzisha kampeni ya ufahamu na uhamasishaji juu ya afya duni ya rasilimali za pwani na bado wahojiwa wanaendelea kusema hali ya rasilimali ni nzuri, inaonyesha kuwa mpango haujafanikiwa.

Ufahamu wa watu juu ya hali ya rasilimali ni muhimu pia ili kuanzisha mipango ya utafiti na Uperembaji wa vitu vyote vilivyo na visivyokuwa na uhai. Wanajamii, hasa watu ambao hutumia rasilimali moja kwa moja, ndio mara nyingi walio na ufahamu mkubwa wa hali halisi ya rasilimali. Habari hizi zinaweza kusaidia na kuwa kama mwongozo wa agenda ya kisayansi, hasa mahali ambapo takwimu za kisayansi zinakosekana.

## *S20. Ufahamu wa Matishio*

**Ni nini**

Ufahamu wa matishio ni kipimo cha watu wanavyofikiria kuwa ni nini matishio makuu ya rasilimali za pwani.

**Jinsi ya kukusanya takwimu**

Takwimu za ufahamu wa matishio hupatikana kwa kuuliza kila mhojiwa :

Ni yapi matishio matano makuu ya afya ya rasilimali za pwani?
. ______________;. ___________; . ___________; . ___________; . ___________

**Jinsi ya kuchambua takwimu**

Kwa misingi ya takwimu kutoka uchunguzi wote, orodhesha matishio makuu. Piga hesabu ya asilimia ya wahojiwa kwa kila tishio kama inavyoonyeshwa katika orodha hii na andika katika karatasi ya uchambuzi wa uchunguzi kama ifuatavyo:

| Matishio yaliyotambuliwa | Asilimia ya waliolitaja |
|---|---|
| Maji machafu | 53% |
| Uvuvi uliokithiri | 30% |
| Uharibifu wa nanga | 26% |

**Angalia maitikio hayafiki 100% kwa sababu wahojiwa wanaweza kuorodhesha mpaka matishio matano.*

*Uchambuzi wa ziada:* Unganisha matishio inapobidi/kufaa. Kwa mfano, kama baadhi ya watu wanasema "uharibifu wa nanga" na wengine wanasema "shughuli za boti" basi "uharibifu wa nanga" unaweza kujumuishwa na "shughuli za boti" kwani ni mambo yanayofanana. Fuatilia mambo haya kwa muda kuona jinsi ufahamu wa matishio unavyobadilika.

Linganisha matokeo haya na takwimu kutoka kwa mahojiano/chanzo pili juu ya *viwango na aina ya athari (K25).* Matishio yaliyoorodheshwa hapo juu pia yapewe viwango kama "juu" katika majibu ya *"viwango na aina ya athari"*. Kama kuna tofauti kubwa basi rudi kwa watoa habari maluum ili kufahamu sababu. Kama tofauti haziwezi kuelezeka, basi yaweza kuwa ni muhimu kufanya hojaji kwa kaya zote. Ni muhimu kuelezea yale watu wanayoyaona ni matishio kutoka sehemu zote mbili.

Linganisha matokeo haya na uchunguzi wa kisayansi juu ya matishio kwa hali ya rasilimali kujua kwa uhakika ufahamu wa watu juu ya matishio.

**Umuhimu wa habari hizi kwa wasimamizi na wadau wengine**

Habari za ufahamu juu ya matishio ya rasilimali ni muhimu kwa kutambua matishio/athari zinazokabili rasilimali za pwani. Wanajamii, hasa wanaotumia rasilimali moja kwa moja ndio wenye ufahamu zaidi juu ya matishio kwa rasilimali. Habari hizi zaweza kusaidia kuongoza agenda ya kisayansi hasa mahali ambapo hakuna takwimu za kisayansi, kwa kutambua shughuli ambazo nizipewe vipaumbele.

Kwa kufuatilia habari hizi kwa muda, msimamizi anaweza kufahamu mguso wa usimamizi kwa shughuli za pwani. Kwa mfano, kama mpango wa usimamizi umezuia kuvua na bado watu wanaendelea kuona uvuvi kama tishio, basi yaonyesha kuwa mpango huo haujafanikiwa kikamilifu. Uchunguzi zaidi wa kisayansi utasaidia kuonyesha kama ni sahihi.

Na hatimaye, habari hizi ni muhimu sana kwa kutengeneza mpango wa ufahamu na uhamasishaji na kutafuta ushirikishwaji wa wadau. Kama wanajamii hawaoni kuwepo athari juu ya rasilimali za pwani, basi itakuwa vigumu kuwashirikisha katika shughuli za usimamizi wa pwani. Kama wanajamii wanaona shughuli moja au mbili tu ndizo zenye athari juu ya rasilimali, ilhali uchunguzi wa kisayansi unaonyesha kuwepo kwa athari nyengine, basi mpango wa ufahamu na uhamasishaji unatakikana kuanzishwa ili kuongeza ufahamu wa shughuli zote zenye kuathiri rasilimali.

## *S21. Ufahamu wa Sheria na Kanuni*

**Ni nini**

Ufahamu wa kanuni na sheria hupima ujuaji wa watu kama sheria na kanuni za rasilimali za pwani zipo.

**Jinsi ya kukusanya takwimu**

Takwimu za ujuaji wa sheria na kanuni hupatikana kwa kuuliza kila mhojiwa:

Je, kuna sheria na kanuni zinazohusiana na shughuli zifuatazo?: (tengeneza orodha ya shughuli sawa na zile za *shughuli (K18).*

(Jibu Ndiyo au Hapana): Uvuvi _____; Mikoko _____; Viumbe bahari _____; uekezaji katika mahoteli _____;

Maendeleo ya makazi _____; Michezo ya baharini _____; Usafirishaji baharini _____

Ili kuelewa ufahamu, timu ya uchunguzi yenyewe lazima ifahamu sheria na kanuni zilizopo. Hii inaweza kujulikana kwa kumuuliza msimamizi au kwa kuangalia taarifa zilizokusanywa katika *"umilikaji na taratibu za kawaida (K32)"* na *"kanuni zisizo rasmi na umiliki (K33)"* Wekea duara rasilimali zenye sheria na kanuni ili kulinganisha na maitikio.

**Jinsi ya kuchambua takwimu**

Piga asilimia ya wahojiwa waliosema zipo sheria na kanuni kwa kila shughuli, na andika katika *karatasi ya uchambuzi wa uchunguzi*.

*Uchambuzi wa ziada:* Linganisha asilimia na zile zilizozungushiwa duara. Shughuli zilizozungushiwa duara (zina kanuni na sheria) lazima ziwe zinafahamika zaidi ya shughuli nyingine. Shughuli zinazofahamika zaidi, na bado hazina uthibiti zinaonyesha kuna kutokueleweka na jamii. Shughuli ambazo zimezungushiwa duara na zina ufahamu mdogo zinaonyesha jamii haitambui kuna kanuni na sheria. Maelezo mafupi yanaweza kutolewa juu ya kanuni na sheria, utiifu na udhibiti kutoka kwenye matokeo ya vigezo viwili vinavyofuata.

**Umuhimu wa habari hizi kwa wasimamizi na wadau wengine**

Habari hizi ni muhimu sana ili kuweza kutengeneza mpango wa ufahamu na uhamasishaji na kutafuta ushirikishwaji wa wadau. Kama wanajamii hawafahamu uwepo wa kanuni na sheria, ni vigumu kwao kuweza kuzifuata. Itakuwa vigumu pia kushirikisha wanajamii katika shughuli za usimamizi wa pwani. Kufahamu kiwango cha ufahamu cha wadau juu ya sheria ni muhimu katika kuandaa mipango ya ufahamu na uhamasishaji. Elimu ni msingi wa kukubali sheria. Hivyobasi, ni muhimu kwa wasimamizi kuzijua kanuni na sheria zisizofahamika na jamii ili mpango wa ufahamu uweze kulenga sheria hizo. Kuperemba ufahamu wa jamii wa kanuni na sheria ni muhimu ili kujua athari ya usimamizi wa pwani juu ya mitazamo na ufahamu.

## *S22. Utii wa Sheria*

**Ni nini**

Utii wa sheria hupima ni kwa kiwango gani watu huonekana wanakubaliana na sheria. Habari juu ya ufahamu wa watu na kiwango wanachokubali sheria na kanuni zitafungamana na kiwango cha ufahamu wao wa kanuni na sheria hizi.

**Jinsi ya kukusanya takwimu**

Takwimu za utii wa sheria hupatikana kwa kumuuliza kila mhojiwa:

Kwa kipimo cha 1 mpaka 5 (1=Hawakubaliani, 5=Wanakubaliana kikamilifu); ni kwa kiwango gani watu wanakubaliana na sheria na kanuni za usimamizi wa pwani?_____

*Takwimu za ziada:* Wahojiwa wanaweza kuulizwa ni shughuli au sheria gani watu wanakubaliana nazo au hawakubaliani nazo.

**Jinsi ya kuchambua takwimu**

Piga hesabu ya asilimia ya wahojiwa kwa kila kipimo cha vile wanavyodhaniwa kukubaliana na sheria na kanuni, na andika katika karatasi ya uchambuzi wa uchunguzi.

*Uchambuzi wa ziada:* Baadhi ya asilimia zinaweza kujumuishwa ili kurahisisha tafsiri. Kwa mfano, kama asilimia 23 ya wahojiwa wanasema kuna ukubali wa sheria kikamilifu na asilimia 42 wanasema kuna ukubali mdogo wa sheria, basi hii yaweza kuunganishwa kusema, "asilimia 65 ya wahojiwa wanaona kupo kukubali kwa kiwango kidogo mpaka kukubali kabisa". Hii ni rahisi kueleweka kuliko kuorodhesha asilimia kwa kila ukubali. Linganisha matokeo haya kila baada ya muda kujua kama ukubali unaongezeka, kupungua au kubaki vilevile. Unaweza kutoa maelezo juu ya ukubali, himasheria, na sheria na kanuni kutoka kwa vigezo vya nyuma na vile vifuatavyo. Linganisha mabadiliko katika utiifu wa kanuni na sheria na mabadiliko katika *ushirikishwaji na kuridhika kwa wadau (S17)* na angalia kama vigezo hivyo viwili vina uhusiano.

**Umuhimu wa habari hizi kwa wasimamizi na wadau wengine**

Habari za ukubali wa sheria ni muhimu ili kufahamu ushirikishwaji wa wadau na kutambua matatizo ya usimamizi wa pwani. Kutokubali sheria kuna madhara si kwa rasilimali tu, bali pia kwa kupata ushirikiano wa wadau. Kama inaonekana kwa ujumla kuwa hakuna ukubali wa sheria, basi itakuwa vigumu watu kukuamini, kukuunga mkono, kushirikiana nawe au kukubali sheria.

Kwa kuperemba habari hizi kila baada ya muda, msimamizi anaweza kuona mguso wa usimamizi juu ya mitazamo na ufahamu wa watu. Kama ukubali unaanza kuongezeka, basi hii lazima ionekane katika ufahamu wa watu juu ya kukubali sheria. Kama sivyo, basi msimamizi atalazimika kuwasilisha mabadiliko ya ukubali sheria kwa wananchi (kwa mfano, toa taarifa za kupungua kwa ukiukaji katika eneo lililotengwa katika majarida).

## *S23. Himasheria*

**Ni nini**

Himasheria hupimwa kwa jinsi watu wanavyoona ni kwa kiasi gani sheria zinatekelezwa. Hii inafanana na ukubali wa sheria, isipokuwa ukubali unahusika na tabia za watu (yaani watu kuzingatia sheria). Himasheria inahusu shughuli za usimamizi kama vile doria, kutoza faini na kunyang'anya zana mbaya. Habari za ufahamu wa watu wa kiasi sheria na kanuni zinatekelezwa zinafungamana sana na kiwango cha ufahamu wa watu cha sheria na kanuni.

**Jinsi ya kukusanya takwimu**

Takwimu za udhibiti hupatikana kwa kumuuliza kila mhojiwa:
Kwa kipimo cha 1 mpaka 5 (1=Hakuna himasheria; 5=Kuna himasheria kikamilifu), ni kwa kiasi gani kanuni na sheria zinatekelezwa?

*Ukusanyaji wa takwimu za ziada:* Wahojiwa wanaweza waulizwe maswali maalum kuhusu udhibiti kama, "Ni kwa kiasi gani sheria zinatekelezwa kwa kila shughuli ya pwani na baharini?", Ni mara ngapi wahalifu wamekamatwa wakivunja sheria?" na "Ni jambo gani moja ambalo chombo cha usimamizi chaweza kufanya kuboresha udhibiti?"

**Jinsi ya kuchambua takwimu**

Piga hesabu ya asilimia ya wahojiwa kwa kila kipimo cha himasheria, na andika katika *karatasi ya uchambuzi wa uchunguzi.*

*Uchambuzi wa ziada:* Baadhi ya asilimia zaweza kujumuishwa ili kurahisisha tafsiri kama ilivyoelezwa kwenye ukubali wa sheria. Linganisha matokeo haya baada ya muda kuona kama udhibiti unaongezeka, kupungua au unabaki vilevile. Maelezo mafupi yanaweza kutayarishwa kuzungumzia himasheria, ukubali wa sheria na kuwepo kwa kanuni na sheria kutokana na vigezo viwili vya nyuma. Linganisha mabadiliko katika udhibiti na mabadiliko katika *ushirikishwaji na kuridhika wa wadau (S17)* na uone kama kuna uhusiano.

**Umuhimu wa habari hizi kwa wasimamizi na wadau wengine**

Habari za udhibiti ni muhimu kwa kufahamu matatizo ya usimamizi wa pwani. Udhibiti ni baadhi ya vile vielelezo vya usimamizi vinavyoonekana sana, na kwa hivyo ni muhimu katika kujua ufahamu wa watu juu ya ufanisi wa usimamizi. Kukosekana kwa udhibiti kuna madhara si kwa rasilimali tu, bali pia kwa kupata usaidizi wa wadau. Sawa na ukubali wa sheria, kama inafahamika kwa jumla kuwa sheria hazitekelezwi, basi itakuwa ni vigumu watu kukuamini, kukuunga mkono, kushirikiana nawe au kukubali sheria. Pia kwa kuperemba habari hizi kila baada ya muda, msimamizi anaweza kuona athari ya usimamizi juu ya utawala kwani udhibiti ni sehemu yake muhimu. Hii itawapatia fursa wadau kutoa marejesho kwa wasimamizi juu ya ufanisi wa usimamizi wao.

## *S24. Ufahamu wa Matatizo na Masuluhisho ya Usimamizi wa Pwani*

**Ni nini**

Ufahamu wa matatizo na masuluhisho ya usimamizi wa pwani hupima yale watu wanafikiria ni matatizo yanayokabili usimamizi wa pwani pamoja na utatuzi wake.

**Jinsi ya kukusanya takwimu**

Takwimu juu ya vigezo hivi hupatikana kwa kumuuliza kila mhojiwa:

Mbali na matishio, ni matatizo gani makuu mawili yanayokabili shughuli za usimamizi wa pwani katika jamii?

______________________; ____________________

Unaona kuna masuluhisho gani kwa matatizo haya?

______________________; ____________________

**Jinsi ya kuchambua takwimu**

Kwa kuzingatia takwimu kutoka uchunguzi wote, orodhesha matatizo makuu yanayokabili usimamizi wa pwani. Piga hesabu ya asilimia ya wahojiwa waliotaja kila tatizo. Weka matatizo katika makundi yanayopasa, hasa matatizo maalum. Kwa mfano, kama asilimia 4 ya wahojiwa walisema ni migogoro kati ya wavuvi katika jamii X na Y, na asilimia 12 waliona migogoro kati ya wavuvi kwa jumla, basi hii inaweza kuunganishwa ili kurahisisha. Andika habari hii katika karatasi ya uchambuzi wa uchunguzi.

*Uchambuzi wa ziada:* Linganisha matokeo kila baada ya muda fulani kuona jinsi matatizo ya usimamizi yanavyobadilika. Maelezo juu ya watu wanavyofikiria kuhusu matatizo na masuluhisho na jinsi yamebadilika na wakati yanaweza kutolewa.

**Umuhimu wa habari hizi kwa wasimamizi na wadau wengine**

Habari za watu wanavyoyaona matatizo ya usimamizi wa pwani na usuluhishi ni muhimu ili kufahamu yale watu wanafikiria yafanywe na wasimamizi wa pwani, na hii inaweza kumsaidia msimamizi kutambua vipaumbele vya usimamizi. Kutokana na mtazamo wa uhusiano kati ya msimamizi na jamii, matatizo yanayofikiriwa na masuluhisho yanaweza kuwa muhimu zaidi hata kuliko athari na suluhisho zilizotambuliwa na uchunguzi wa kisayansi, kwani haya yanaihusu sana jamii na lazima usimamizi uonyeshe kuyashughulikia, au lazima ifahamishe jamii matatizo halisi kama kuna tofauti kubwa.

## *S25. Ufahamu wa Matatizo ya Jamii*

**Ni nini**

Ufahamu wa matatizo ya jamii hupima mambo ambayo watu wanafikiria ni matatizo yanayokumba jamii.

**Jinsi ya kukusanya takwimu**

Takwimu za vigezo hivi zinapatikana kwa kumuuliza kila mhojiwa:

Ni matatizo gani matatu makuu yanayokumba jamii?

________________________; ________________________; ___________________________

*Ukusanyaji wa takwimu za ziada:* Wahojiwa pia wanaweza kuulizwa ni masuluhisho gani wanayofikiria kwa matatizo ya jamii. Ni muhimu kwa timu ya uperembaji kueleza wazi kuwa matatizo haya huenda yasitatuliwe kwa misingi ya uperembaji huu. Bali hii ni njia ya kusaidia wasimamizi kuyaweka wazi na kutafuta utatuzi wa polepole kwa kushirikiana na jamii.

**Jinsi ya kuchambua takwimu**

Kwa kuzingatia takwimu kutoka uchunguzi wote, orodhesha matatizo makuu yanayoikabili jamii. Piga hesabu ya asilimia ya wahojiwa waliotaja kila tatizo. Weka matatizo katika makundi yanayopasa, hasa matatizo maalum. Kwa mfano, kama 4% ya wahojiwa walisema hakuna utulivu, na 12% walisema usalama kwa jumla, basi haya yaweza kuunganishwa ili kurahisisha. Andika taarifa hii katika karatasi ya uchambuzi wa uchunguzi.

*Uchambuzi wa ziada:* Linganisha matokeo kwa muda ili kuona mabadiliko ya matatizo katika jamii. Maelezo mafupi ya ufahamu wa watu juu ya matatizo na utatuzi wake na jinsi yalivyobadilika yanaweza kutolewa.

**Umuhimu wa habari hizi kwa wasimamizi na wadau wengine**

Habari za matatizo ya jamii zinaweza kuwasaidia wasimamizi kuyaelewa matatizo makuu yanayoikabili jamii (kwa mfano, lishe duni, kukosa umeme) ambayo mpango wa usimamizi unaweza au usiweze kuyatatua. Masuala ya ukosefu wa usalama, kwa mfano (binafsi au ya umilikaji wa ardhi), yanaweza kuathiri kiwango cha kujitolea cha jamii katika kusimamia rasilimali za pwani na baharini.

Kueleza waziwazi matatizo yanayokumba jamii kutaiwezesha jamii kuhakikisha kwamba wasimamizi wanawaelewa na kuwajali watumiaji wa rasilimali za pwani na baharini.

## *S26 & S27. Changamoto na Mafanikio katika Usimamizi wa Pwani*

**Ni nini**

Mafanikio na changamoto katika usimamizi wa pwani hupima mawazo ya watu juu ya nini kimefanyika vyema na nini hakikufanikiwa kwa usimamizi wa pwani katika jamii.

**Jinsi ya kukusanya takwimu**

Takwimu za mafanikio na changamoto zinapatikana kwa kumuuliza kila mhojiwa:

Ni mambo gani mawili ambayo unafikiria yamefanyika vyema juu ya usimamizi wa pwani katika jamii?

__________________________; ___________________________

Ni mambo gani mawili ambayo hayakufanyika vizuri juu ya usimamizi wa pwani katika jamii?

________________________: _________________________.

*Ukusanyaji wa takwimu za ziada:* Waulize wahojiwa waeleze maitikio yao kuhusu maswali ya hapo juu.

**Jinsi ya kuchambua takwimu**

Kwa kuzingatia takwimu kutoka uchunguzi wote, orodhesha yale mambo ambayo yamefanyika vizuri kama ilivyosemwa na wahojiwa. Piga hesabu ya asilimia ya wahojiwa waliosema kwa kila jambo. Weka mambo hayo katika makundi yanayopasa. Fanya hivyo hivyo kwa changamoto katika usimamizi wa pwani. Andika habari hizi katika karatasi ya uchambuzi wa uchunguzi.

*Uchambuzi wa ziada:* Linganisha matokeo kwa muda kuona jinsi mafanikio na changamoto yalivyobadilika. Linaganisha na *ufahamu wa matatizo katika usimamizi wa pwani (S24)* kuona matokeo. Maelezo mafuti juu ya watu wanavyoona mafanikio na changamoto katika usimamizi wa pwani yanaweza kutolewa.

**Umuhimu wa habari hizi kwa wasimamizi na wadau wengine**

Habari za matatizo na changamoto katika usimamizi wa pwani zinatoa ufahamu juu ya chimbuko na ufumbuzi unaokabili usimamizi wa pwani. Zinasaidia pia kuelewa ufahamu na fikra za watu juu ya usimamizi wa pwani, na zinaweza kusaidia kuelezea juu ya ukubali wao wa kushiriki katika usimamizi. Kama mpango wa usimamizi unaonekana umekuwa ukifanya vizuri, basi watu watakuwa tayari kufanya kazi na mpango huo. Habari hii pia inaweza kutoa ufahamu wa mafanikio ya mpango, au kuangazia kutoeleweka kwa usimamizi, na kwamba msimamizi anaweza baadaye kuyashughulikia kwa kuieleza jamii kwa undani.

Hii hutoa fursa kwa wadau kutoa marejesho kwa wasimamizi juu ya mafanikio na mapungufu ya mpango.

## *S28. Thamani Isiyouzika na Isiyotumika*

**Ni nini**

Thamani ya rasilimali za pwani isiyouzika na isiyotumika ni vipimo vya jinsi watu wanavyofikiria juu ya thamani ya rasilimali za pwani ambazo haziuzwi sokoni (manufaa yasiyouzwa) na thamani ya rasilimali kwa sehemu ya jamii ambayo haitumii rasilimali (isiyotumiwa).

Thamani isiyo ya sokoni ni thamani ya rasilimali (kwa mfano samaki) na huduma (kwa mfano, uzamiaji) sizizouzwa katika soko lolote. Hii ni pamoja na matumizi ya moja kwa moja, kama vile wazamiaji ambao wamesafiri kwenda kuzamia kwa njia binafsi; na matumizi yasiyo ya moja kwa moja, kama vile usaidizi wa kibayolojia kwa njia ya malisho, mazalia ya samaki, hifadhi ya kingo za bahari kutokana na mawimbi. Thamani isiyo ya matumizi haiambatani na matumizi yoyote (thamani ya kufahamu kuwa rasilimali ipo na inaweza kutumiwa watu wakiihitaji hata kwa vizazi vijavyo), na thamani ya kuwepo (thamani ya kufahamu kuwa rasilimali ipo katika hali fulani).

**Jinsi ya kukusanya takwimu**

Dhana za thamani isiyouzika na isiyotumika ni za kidhahania na kufikirika. Kwa kawaida, mtaalam wa kiuchumi lazima afanye uchunguzi wa vigezo hivi kwa kuwa mbinu za uchumi zilizotumika ni ngumu. Kwa kutambua kuwa wataalam hawa hawapatikani katika maeneo mengi, mwongozo huu *(SocMon)* unapendekeza njia ya kupima mtazamo wa watu kwa kuzingatia kipimo.

Njia hii hutumia msururu wa maswali yanayolenga ufahamu wa watu juu ya thamani za moja kwa moja zisizouzika (usaidizi wa kazi za kibayolojia) na thamani zisizotumika zinazohusiana na kuwepo kwa rasilimali. Hizi zinaweza kujumuisha maelezo kuhusu uzuri, kuhusu kuangalia bahari kwa vizazi vijavyo, kuhusu "kutumia wakati kustarehe kwenye maji", na kuhusu bidhaa na huduma nyengine zisizochukulika ambazo mazingira ya pwani yaliyonawiri yanaweza kutoa.

Yafuatayo ni maelezo yaliyopendekezwa, ambayo yatatumika kwa rasilimali na shughuli kwa kila eneo. Kila mhojiwa anaulizwa kuonyesha ni kwa kiasi gani anakubaliana au hakubaliani na msururu wa maelezo haya. Wahojiwa wanaulizwa kama: wanakubaliana sana (5), wanakubaliana (4), hawakubaliani au kutokubaliana (3) kutokubaliana (2), au kutokubaliana kabisa (1) na kila maelezo.

_____(a) Miamba ni muhimu kwa kukinga nchi kavu dhidi ya mawimbi (thamani isiyouzika na isiyo ya moja kwa moja).

_____(b) Siku za mbeleni hali ya uvuvi itakuwa nzuri kama tutafyeka matumbawe (thamani isiyouzika na isiyo ya moja kwa moja)

_____(c) Matumbawe yana manufaa tu kwa wavuvi au wazamiaji (thamani isiyotumika).

_____(d) Nataka vizazi vijavyo wafurahie mikoko na matumbawe (kurithi thamani isiyotumika).

_____(e) Matumbawe ni muhimu tu ikiwa unavua au kuzamia. (kuwepo thamani isiyotumika)

_____(e) Uvuvi lazima uzuiliwe katika maeneo fulani hata kama maeneo hayo yanavuliwa ili kuruhusu samaki na matumbawe kukua (thamani ya kuwepo).

_____(F) Lazima tuzuie uekezaji katika baadhi ya maeneo ya pwani ili vizazi vijavyo waweze kupata mazingira ya asili. (thamani ya kurithi).

_____(G) Nyasi bahari hazina thamani kwa watu (thamani ya kuwepo).

Angalia kwamba maelezo yameandikwa ili kwamba kukubaliana na baadhi kutaonyesha imani sahihi, wakati kukubaliana na nyengine kutaonyesha kinyume. Hii ilifanyika ili kudhibiti maitikio pale ambapo mhojiwa aidha atakataa au kukubalina na yote. Maelezo haya yamepangwa kwa mtawanyiko kwa kuzingatia utofauti huu.

*Ukusanyaji wa takwimu za ziada:* Baadhi ya shughuli au bidhaa zinazohusiana na bahari zinaweza kuwa na thamani za kimila kwa jamii.
Wahojiwa waulizwe kuorodhesha shughuli au vitu katika jamii (kwa mfano, uvuvi, hekalu, mwamba) na wazipange katika makundi kulengana na umuhimu wake wa kimila kwa jamii. Hii ni muhimu hasa ili kutambua shughuli na vitu ambavyo vinaweza kuwa si muhimu kiuchumi lakini bado vinachukuliwa kuwa sehemu muhimu ya maisha ya jamii. Kwa mfano, katika maeneo ambayo utalii unachukuwa mahali pa uvuvi, jamii bado inaweza kuona uvuvi kama sehemu ya jamii, hata kama hauendelei kuwaingizia kipato.

Maswali ya wazi, kama vile: "Kama matumbawe yakipotea, kwako wewe itakuwaje?", "kama samaki watatoweka, kwako wewe itakuwaje?" na, "Kama sehemu yote ya fukwe itajengwa kwako wewe itakuwaje?", yanaweza kuulizwa ili kupata ufahamu wa umuhimu wa rasilimali na matumizi yake.

**Jinsi ya kuchambua takwimu**
Kwa kila swali: Piga hesabu ya asilimia ya wahojiwa kwa kila kiwango cha makubaliano na andika asilimia hizo ndani ya *karatasi ya uchambuzi wa uchunguzi*. Kufahamu kama wahojiwa wanasema thamani isiyouzika au thamani isiyotumika ya rasilimali, chukulia kwa kiasi gani wanakubaliana na maelezo. Maelezo a, c, e, f na g, yamewekwa kiuyakini. Kama wahojiwa wanakubaliana na maelezo haya, wanathamini rasilimali. Maelezo b, d, na h yamewekwa kiukanushi. Kama wahojiwa wanakubaliana na maelezo haya, hawathamini rasilimali hizo.

*Uchambuzi wa ziada:* Viwango vya makubaliano (kwa mfano, kukubali kabisa na kukubali) vinaweza kuunganishwa kurahisisha tafsiri. Kwa mfano, kama asilimia 23 ya wahojiwa wanakubaliana sana na maelezo a na asilimia 34 ya wahojiwa wanakubali maelezo a, basi hizi zinaweza kuunganishwa na kusema, "zaidi ya asilimia hamsini wanakubali kuwa miamba inasaidia kulinda ardhi dhidi ya mawimbi." Hii ni rahisi kuelewa kuliko kuorodhesha asilimia zote.

Ni muhimu pia kutoa maelezo ya kiasi ambacho watu wanathamini rasilimali hizo. Linganisha matokeo kwa muda kuona kama ufahamu wa watu imebadilika.

**Umuhimu wa habari hizi kwa wasimamizi na wadau wengine**
Habari za thamani isiyouzwa wala kutumika ni muhimu kwa kufahamu jinsi watu wanavyothamini rasilimali. Mara nyingi thamani ya vitu hufikiriwa thamani ya soko, kama vile viwango vya ajira, mapato na faida halisi. Kwa kufahamu pia ufahamu wa watu juu ya mambo haya, wasimamizi wanapata picha halisi ya thamani ya rasilimali. Hii ni muhimu kwa kuonyesha umuhimu wa rasilimali na uhifadhi wake kwa watengenezaji wa sera. Ufahamu huu pia ni muhimu katika kutengeneza mpango wa uhamasishaji kwa sababu wasimamizi wanaweza kuona ni kwa kiasi gani watu wanafikiria rasilimali hutoa bidhaa na huduma zaidi ya zile zinazoweza kuuzwa na kununuliwa. Kufuatilia habari hizi baada ya muda kunaweza kutumika kuona namna mipango ya usimamizi inavyoathiri mitazamo na ufahamu wa watu.

Kufahamu vizuri jinsi watu wanavyothamini rasilimali kutasaidia wadau kufahamiana vizuri na kuboresha uhusiano wao wa kazi. Itakuwa pia nafasi kwa wadau kuelezea umuhimu wa rasilimali (yaani zaidi ya thamani yao ya soko) kwa wasimamizi na kuwasaidia kuboresha uhifadhi wa rasilimali.

## UTAJIRI

Utajiri ni vigumu kuupima na mapato ambayo ni moja ya kiashiria cha utajiri ni baadhi ya vitu vigumu na vinavyohitaji takwimu nyingi ili kupatikana. Huhitaji uchunguzi mrefu ambao mara nyingi hautoi matokeo ya kutosheleza. Kwa sababu hizi, kuna viashiria vya utajiri visivyokuwa vya moja kwa moja vilivyotengenezwa kama vile kipimo cha upatikanaji wa chakula cha kutosha, namna ya matumizi, "mtindo wa maisha kwa vitu" vimetengenezwa. Imependekezwa katika mwongozo huu *(wa SocMon WIO)* kutumia "mtindo wa maisha kwa vitu" kama kiashiria cha utajiri wa kaya kwa kuwa ni rahisi kukusanya takwimu zake na pia kuzifanyia uchambuzi. Kwa viashiria vyengine ambavyo vinaweza kuhitaji utaalam wa mwanasayansi wa kijamii au kiuchumi, maelezo ya maandishi na utaalam huu unapatikana katika kiwango cha kanda.

## *S29. Mtindo wa Maisha kwa Vitu*

**Ni nini**

Mtindo wa maisha kwa vitu ni kiashiria cha hali ya maisha ya jamii na kutumika mara nyingi kama kiashiria cha utajiri. Kinaweza kuhusisha kuchunguza vifaa vya ujenzi wa nyumba (kwa mfano paa, kuta), upambaji wa kaya, (kwa mfano mazulia, vikalio), vyombo vya kutumia umeme (kwa mfano runinga, redio, ungo wa sateliti), na mali za uzalishaji (kwa mfano boti, zana za uvuvi).

**Jinsi ya kukusanya takwimu**

Takwimu hizi hukusanywa kirahisi kwa kuangalia na kuhoji. Kwanza ni muhimu kuwahojii watoa habari maalum kujua vigezo vya utajiri na umaskini. Vitu gani vya kujengea, mapambo gani ya nyumba, vifaa gani vya umeme na vya uzalishaji vinavyoonyesha utajiri au umaskini. Ndipo kwa ngazi ya kaya mhojiwa anaulizwa:

Je, unamiliki nyumba yako? Ndiyo................; Hapana..........................

Ukubwa wa nyumba : idadi ya vyumba.......................................

Halafu habari zifuatazo zinaweza kuangaliwa au kuulizwa:

Aina ya paa: vigae ____; mabati ____; mbao ____; makuti ____; nyasi ____;

Aina ya kuta za nje: vigae ____; tofali/saruji ____; mawe ____; udongo ____; makuti ____; nyasi ____;

Madirisha: vioo ____; mbao ____; framu ____; wazi ____; hakuna dirisha ____;

Sakafu: vigae ____; mbao ____; saruji ____; udongo ____;

Kupata maji: bomba ____; kisima cha jumuiya ____; bwawa/kisima binafsi ____; mto ____;

Nishati: umeme ____; nguvu ya jua ____; betri ____; hakuna ____;

Hii ni orodha iliyorahisishwa ya vifaa vya ujenzi. Katika hali nyengine orodha hii lazima ifanyiwe marekebisho ili kuangazia vitu vya utajiri katika eneo la uchunguzi. Kwa mfano, katika eneo moja "tope" zaweza kuchukuliwa kama ukuta wa kimaskini zaidi. Kwa hivyo orodha lazima igeuzwe iwe:

Kuta: saruji ____; bila saruji ____; mawe ____; mawe na tope ____;, tope ____

Mahali pengine ambapo vifaa vya ujenzi vinachukuliwa kama kiashiria cha utajiri au umaskini lakini nyumba nyingi zimejengwa kwa vifaa vinavyofanana, hali ya vifaa inaweza kuchukuliwa kama kigezo cha kutofautisha utajiri au umasikini. Hivyo kwa kila aina ya paa, kwa mfano (bati, makuti) kunaweza kusema hali mbaya/nzuri.

Kipimo sahihi cha ujenzi kinahitajika kuweza kulinganisha jamii na kwa muda.

Kufahamu mali za uzalishaji mhojiwa anaulizwa:

Je, unamiliki boti yako?____________

Unamiliki boti ngapi?______________

Je, boti imetengenezwa kwa kutumia nini (fibaglasi au mbao)?________

Je, boti inasukumwa na nini? (kasia, tanga au mashine)?________________

Wakati mwingine nyumba sio kipimo kizuri cha hali ya mtu katika jamii, kwa hali hiyo unaweza kuangalia vifaa vya ndani na vya uzalishaji kama mifugo, usafiri, ardhi. Mara nyingine aina ya boti ni kigezo cha utajiri.

*Ukusanyaji wa takwimu za ziada:* Ili kujua mengi zaidi kuhusu hali na utajiri wa mtu katika jamii, wahojiwa wanaweza kuulizwa umilikaji wao wa mali nyengine. Orodha hii inaweza kujumuisha vitu kama vile runinga, redio, majokofu, vikalio, na mali nyengine. Wanaweza pia kuulizwa kuhusu umilikaji wa zana za uvuvi. Kuweka utajiri katika makundi kunaweza pia kutumika kuwauliza wahojiwa waweke makundi ya wadau.

Ni kweli kwamba **mali na vifaa vinavyotumika vitategemea na mahali**, na vile muhimu zaidi vinaweza kutambuliwa na timu yenyewe. Kigezo mara nyengine chaweza kuangaliwa na sehemu nyingine. Kwa mfano, kigezo kilichotambuliwa Madagascar ni muda wa kumaliza shule… Hivyo kuuliza swali juu ya muda wa kumaliza shule ni jambo la maana kule.

**Jinsi ya kuchambua takwimu**

